# Nipashe

Alhamisi Aprili 4, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579883

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com



www.twitter.com/nip

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Hoteli za bilionea wa Ngurdoto kupigwa bei

UKURASA 2




UKURASA 13

# CAG Assad afunguka



• **Ajibu** mapigo ya Bunge, Msekwa atoa ufafanuzi...*Uk.2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**JPM AAGIZA MAKANDARASI WA OVYO WASIPEWE KAZI**

RAIS John Magufuli, ameiagiza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kuacha kuwapa kazi makandarasi wenye...

**UKURASA WA 5**

**WASIOJULIKANA WAUA KATIBU CCM KWA KISU**

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Njia Nne, Mkuranga mkoani Pwani, Jumanne Bakari (55), ameuawa...


## Hatima ya Lema rasmi leo

UKURASA 3



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na wabunge wakifurahia jambo walipokuwa wakizungumza na Peter Mollel maarufu kwa jina la Pierre Konki Liquid (katikati), katika viwanja vya Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

## Spika: Madeni yamewapa wabunge misongo mawazo

UK.3


**MICHEZO** **SIMBA: MUZIKI SASA KWA TP MAZEMBE** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Hatima mali za DECI mwezi ujao

Na Hellen Mwango

HATIMA ya maombi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ya kutaifisha mali za Sh. bilioni 14.3 za Kampuni ya Development Entrepreneurship for Community Initiative (DECI) kuwa mali halali ya serikali au kushindikana, itajulikana Mei 6, mwaka huu.

Uamuzi huo utatolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

Amri hiyo ilitolewa juzi jioni katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Stephen Magoiga baada ya kusikiliza hoja za walalamikiwa dhidi ya waliokuwa wakurugenzi wa DECI Jackson Mtares, Dominick Kigendi, Timotheo Saiguran Ole Loitg'nye na Samuel Mtares.

Maombi hayo namba 42/2019 yalifunguliwa na DPP, Biswalo Mganga, dhidi ya wakurugenzi wa DECI. ambapo walalamikiwa waliwakilishwa na Wakili Majura Magafu.

Juzi mahakama ilisikiza majibu ya hati kinzani ya walalamikiwa kwamba maombi ya DPP hayana ushahidi wa kutosha kuhusu mali zinazoombwa kutaifishwa zilipatikana kwa upatu.

Alidai akaunti zilizowasilishwa na DPP, kati ya hizo moja inamilikiwa na kanisa na ya pili inamilikiwa na mlalamikiwa wa kwanza.

Hata hivyo, hati ya kiapo iliyowasilishwa na DPP hakuna mahali inaonyesha ushahidi kwamba mali zote zimetokana na fedha za ujanjaujanja.

"Mtukufu jaji, hakuna mahali katika maelezo ya awali waliyosomewa walalamikiwa katika kesi ya jinai walikubali mali zilizotajwa zilipatikana isivyo halali, DPP anajaribu kuonyesha kwamba mali zote zilipatikana isivyo halali," alidai Magafu.

"Hakuna ubishi kwamba kuna watu walicheza, lakini walikuwa wanavuna kwa hiyo mali hizi hazikutokana na fedha za upatu," alidai na kuongeza:

"Tunaiomba mahakama itupilie mbali maombi ya DPP kwa sababu hakuna ushahidi wa kuthibitisha kwamba mali hizo zinastahili kutaifishwa na serikali."

Jopo la Jamhuri liliongozwa na DPP Biswalo Mganga akisaidiana na Wakili wa Serikali Mkuu, Paul Kadushi, na Mawakili wa Serikali Waandamizi, Theophil Mutakyawa na Shadrack Kimaro.

Akijibu hoja za walalamikiwa, DPP alidai walalamikaji walikuwa wanaendesha mchezo wa upatu kinyume cha sheria na kwamba mali zote ni mali ya DECI zinafaa kutaifishwa.

Alidai fedha na mali hizo zimethibitika kuwa zilitokana na upatu na ndiyo maana Mahakama ya Rufani katika hukumu yake ilimuelekeza kufungua maombi hayo Mahakama Kuu.

Alidai Deci haikuwa na shughuli nyingine yoyote mbali ya kukusanya fedha, na wajibu maombi hawakupelwka ushahidi wa kupinga hilo, hivyo biashara haramu ya upatu ndiyo ilikuwa kazi yao.

Kuhusu uhusiano wa mali za kanisa na Deci, DPP alidai fedha zilizokuwa katika akaunti ya kanisa zilikuwa za Deci kwa sababu wakàti huo hawakuwa na akaunti kwa kuwa walikuwa hawajakamilisha usajili.

"Wakili anasema Deci ilikuwa inafanya biashara nyingine, lakini hawakuonyesha

INAENDELEA UK. 8

# CAG afunguka kutengwa na Bunge

Na Waandishi Wetu

SIKU moja baada ya Bunge kuazimia kutofanya kazi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, mwenyewe amefunguka na kueleza kuwa huenda uamuzi huo ukasababisha tatizo kubwa zaidi kuliko linavyoonekana hivi sasa.

Prof. Assad aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Shirika la Utangazaji la Tanzania (TBC), kwa njia ya simu.

Juzi, Bunge lilipitisha azimio hilo jijini Dodoma, baada ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuwasilisha taarifa kuhusu shauri dhidi ya Prof. Assad aliyefikishwa mbele yake mwanzoni mwa mwaka huu.

Prof. Assad alikuwa akikabiliwa na tuhuma za kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya chombo hicho cha kutunga sheria.

Akihojiwa na TBC jana asubuhi, Prof. Assad, alisema jambo hilo ni zito na linahitaji tathmini na athari zinazoweza kutokea siku zijazo.

"Tukifanya uamuzi bila kuangalia athari inaweza kuwa na athari badala ya kuwa na ufumbuzi, nafikiri tukae chini tutazame athari ni zipi ili kuepuka matatizo ambayo tunaweza kusababisha."

"Ninaamini kuna watu wenye busara wamezitumia, wasiwasi wangu huenda likawa tatizo kubwa zaidi kuliko linavyoonekana sasa, kunaweza kukawa na mgogoro wa kikatiba kwamba ripoti imeshawasilishwa kwa Rais na mimi siwasilishi ripoti bungeni."

Aliongeza: "Rais atapeleka ripoti zile bungeni katika siku sita zijazo na kama Bunge likikataa kuzipokea hiyo ni tatizo kubwa zaidi, wasiwasi wangu ndio huo," alisema.

Prof. Assad alisema uamuzi huo wa Bunge ni tatizo kubwa zaidi hivyo kwa maoni yake alishauri wahusika wakae chini watafakari athari ni zipi ili kuepuka matatizo ambayo wanaweza kuyatatua.

"Naamini kwamba kuna watu wenye busara na pengine wametoa busara zao, wasiwasi wangu ni kwamba huenda likawa tatizo kubwa zaidi kuliko linavyoonekana hivi sasa," alisema na kuongeza:

"Hii tafsiri kwamba hatutafanya kazi na CAG ni tafsiri pana sana tunatakiwa tuijue vizuri kama nilivyosema mwanzo sijapata hizi habari kwa uhakika, nitazitafuta hata leo nitaongea na watu wangu tutazijua halafu tufanye tathmini kitu gani tunaweza kufanya," alisema.

Kuhusu uamuzi gani atachukua, Prof. Assad alisema hana uamuzi wowote wa kuchukua na kwamba anachokifanya ni dua ili watu waongozwe vizuri wafanye maamuzi yenye faida kwa nchi.

Alisema yeye binafsi ataendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Katiba.

Kuhusu kama anajutia kauli yake aliyoitoa nje ya nchi kuwa Bunge ni dhaifu na kusababisha kuitwa kwenye kamati ya Bunge, Prof. Assad alisema uamuzi kuhusu hilo ulishafanyika kwenye kamati iliyomhoji na majibu yaliyotolewa huko hivyo kama kuna anayeyahitaji ayatafute.

Akieleza kuhusu msimamo wa Bunge, Prof. Assad alisema alisikia taarifa hizo juzi jioni na hajazipitia kwa kina na kuzifanyia tathmini.

"Kimsingi sidhani kama kwa sasa itakuwa busara kusema nina uamuzi huu kwa sababu sijafanya tathmini sawa sawa, pili ninaamini kama Bunge limeamua hivi lina mamlaka ya kufanya uamuzi huo na lina sababu zake," alisema.

"Kimsingi nilikwenda katika Kamati tukazungumza sasa kama suala limefikia hapo kuna kila sababu ya kufanya yale mazungumzo yetu ya Kamati yawe wazi ili kila mtu ajue nimeulizwa kitu gani na kujibu kitu gani na ili kila Mtanzania aweze kufanya tathmini ili wapime kwamba hili suala lilipofika ni sawa sawa au si sawa," alisema.

Alipoulizwa nini tafsiri ya kisheria Bunge kutangaza kutoshirikiana naye, Prof. Assad alisema yeye siyo mwanasheria hivyo hawezi kulijibu.

Alisema Katiba inampa majukumu ya kufanya na majukumu hayo yanatekelezwa na Bunge,

INAENDELEA UK. 8



Mafundi wa kampuni ya ujenzi ya CCECC, wakiendelea na ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua katika Barabara ya Tandale, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Hoteli za bei mbaya za bilionea kupigwa bei

Na Salome Kitomari

BENKI ya Exim imetangaza kuuza mali za aliyekuwa mfanyabiashara maarufu jijini Arusha, Faustine Mrema (64), aliyefariki Julai 30, mwaka 2017, ikiwamo hoteli ya nyota tano ya Ngurdoto.

Hoteli ya Ngurdoto ilikuwa maarufu kwa mikutano ya viongozi wa kiserikali, zikiwamo semina elekezi.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana kwenye vyombo vya habari na kampuni ya uwakili ya Locus Attorneys, liliorodhesha mali zitakazouzwa na kuwataka wenye nia ya kununua kuwasilisha maombi yao hadi Aprili 15, mwaka huu.

Mali zilizoorodheshwa ni hoteli ya kitalii ya Ngurdoto Mountain Lodge Limited, ambayo iko kwenye kiwanja namba 66/1/5 eneo la USA River East Bank, Manispaa ya Arusha. Nyingine ni Impala Hotel Limited iliyopo eneo la Kijenga manispaa ya Arusha, katika kiwanja namba 10.

Pia mali zilizopo kwenye eneo la Impala Hoteli Limited katika kiwanja namba 11 na 12 Kijenge Manispaa ya Arusha.

Kwa mujibu wa tangazo hilo Benki hiyo imemteua Dk. Onesmo Kyauke, kuwa wakala wa uuzwaji wa mali hizo na haijaelezwa sababu ya uamuzi wa kuuza mali hizo.

Aidha, haijaelezwa sababu za uuzwaji mali hizo, lakini imeelezwa kuwa kwa mnunuzi yeyote baada ya ukaguzi wa mali hizo atapaswa kupeleka maombi yake akieleza mali halisi anayotaka kununua yakiwa kwenye bahasha iliyofungwa. Wakati wa uhai wake, Mrema alikuwa anamiliki mali nyingine kama hoteli ya Naura Spring na kampuni za utalii ya Classic Tours & Safaris zilizopo mkoani Arusha na Moshi.

Mfanyabiashara huyo alifariki katika Hospitali ya Garden City nchini Afrika Kusini, wakati akipatiwa matibabu ya saratani ya mifupa.

## HABARI KITAIFA



Rais Dk. John Pombe Magufuli akiwa na mkewe Mama Janeth Magufuli pamoja na viongozi wengine wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mkoa wa Mtwara na wabunge wakati akikata utepe kuashiria uzinduzi wa mitambo itakayotumika katika ujenzi wa barabara ya km 210 Mtwara-Newala-Masasi, sehemu ya Mtwara-Mnivata km 50 katika hafla iliyofanyika Naliendele mkoani humo jana. **PICHA: IKULU**

# JPM aagiza makandarasi wa ovyo wasipewe kazi

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS John Magufuli, ameiagiza Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kuacha kuwapa kazi makandarasi wenye rekodi mbaya hata kama watakuwa wameshinda zabuni.

Amewataka kutumia Sheria Namba 17 ya Mwaka 1997, pamoja na Bodi ya Makandarasi kuwafukuza makandarasi ambao hawatafanya kazi vizuri.

Alitoa maagizo hayo jana mkoani Mtwara, wakati akiweka jiwe la msingi kwenye ujenzi wa mradi wa barabara kutoka Mtwara hadi Mnivata, yenye urefu wa kilometa 50, ikiwa ni sehemu ya barabara kuu kutoka Mtwara-Tandahimba-Newala-Masasi, yenye urefu wa kilometa 210.

"Niwaombe Wizara ya Ujenzi, makandarasi wenye rekodi mbaya msiwape kazi hata kama wameshinda zabuni, tumieni sheria namba 17 ya mwaka 1997, kwa kupitia pia Bodi ya Makandarasi, makandarasi ambao hawatafanya vizuri wafukuzwe," alisema Rais Magufuli na kuongeza:

"Wakatafute kazi zingine, wakavue samaki nchanga na shughuli zingine na siyo kazi za

INAENDELEA UK. 8

# Hatima ya Lema kujulikana leo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

HATIMA ya Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema), kuendelea au kutoendelea kuhudhuria vikao vya Bunge inatarajiwa kujulikana leo, huku mwenyewe akieleza kuwa tayari ameshajua kinachofuata na ameshakata tiketi kurejea Arusha.

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' bungeni jijini Dodoma jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao, alimtaka Lema afike mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhojiwa kuhusu tuhuma zinazomkabili.

"Kama ambavyo Naibu Spika (Dk. Tulia Ackson) alivyoagiza jana (juzi), naagiza suala lake lipelekwe kwenye Kamati ya Maadili na lifikishwe leo leo (jana), ikiwezekana mambo yake kesho (leo) yawe yamekamilika," alisema.

"Kwa hiyo, Kamati ya Maadili saa nane kamili mchana muanze na Mheshimiwa Lema, kuanzia saa saba mchana uwe katika maeneo yale," Spika Ndugai alisisitiza.

Nje ya Ukumbi wa Bunge, Lema aliiambia Nipashe kuwa juzi saa mbili usiku,

INAENDELEA UK. 8

# Spika: Madeni yamewapa wabunge misongo mawazo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema kuna misongo mingi ya mawazo bungeni kutokana na wabunge kukabiliwa na madeni makubwa.

Kiongozi huyo wa Bunge alitoa kauli hiyo bungeni jana asubuhi mara tu baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali'.

Alisema baadhi ya wabunge wamekuwa wakiingia katika msuguano na uongozi wa Bunge na wananchi hawajui kiundani chanzo chake, akibainisha kuwa wengi wao wanakabiliwa na msongo wa mawazo kutokana na madeni makubwa.

Akifafanua zaidi kuhusu changamoto hiyo, Spika Ndugai alimtolea mfano Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema (Chadema) ambaye alisema huenda anakabiliwa na msongo wa mawazo kutokana na deni la Sh. milioni 644.

"Hatumwogopi yeyote, pia niwaambie wananchi mambo mengine hawayaelewi vizuri. Ipo misongo mingi ya mawazo humu ndani, labda ndiyo inasababisha mambo hayo.

"Ninyi ni wawakilishi wa wananchi, mnapokuja hapa (bungeni), lazima muwakumbuke wale mnaowawakilisha, unapotanguliza 'personal interest' (maslahi binafsi) kwamba mimi siogopi... siyo wewe ni wale wale unaowawakilisha, wana haki ya wewe kuwawakilisha.

"Wakati mwingine kati ya wewe na wale (wapigakura) lazima upime kipaumbele ni nani. Ukiweka kipaumbele wewe, kidogo hapo inakuwa siyo sawasawa.

"Hapa kuna msongo wa mawazo. Kwa mfano, yapo mambo ambayo hatusemi ila tuseme kidogo. Mheshimiwa Lema tangu aje hapa bungeni amekopa Sh. milioni 644... (kelele zilisikika kutoka Kambi ya Upinzani wakipinga kitendo cha kutaja deni la Lema). Useme aaah... eseme eeeh... amejipigapiga ameshalipa na sasa hivi anadaiwa Sh. milioni 419.

"Niwaambie waheshimiwa wabunge, Spika Ndugai haogopi. Wanaofikiri sisi dhaifu siyo dhaifu, nilishasema na kurudia; yeyote ambaye anataka kuingia kwenye 18, sisi tupo tayari na yeye. "Tutawapeleka huko kwenye Kamati (ya Maadili) ambayo baadhi walisema ina udhaifu fulani. Lema atakwenda huko, kesho (leo) panapo majaaliwa, tutaifahamu hatma yake na mwingine anayejiona, anaalikwa kwenye mkutano huo."

Spika Ndugai ambaye pia ni Mbunge wa Kongwa (CCM), aliendelea kusisitiza kuwa anataka kuthibitisha Bunge la 11 lina uongozi imara na itathibitika.




# ACT-Wazalendo kuishtaki Tanzania kimataifa

**Na Mwandishi Wetu**

MWANASIASA nguli nchini, Maalim Seif Sharif Hamad, amesema chama chake cha ACT-Wazalendo hakitanyamazia 'figisu' zinazofanywa na taasisi za kusimamia demokrasia kama Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kwamba kitaishtaka serikali kwenye Jumuiya za Kimataifa.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam wiki hii, Maalim Seif alisema mashtaka yanapelekwa kwenye vyombo vya kusimamia haki, usalama na demokrasia vya Afrika.

Alisema, chama hicho licha ya kupewa tishio la kufutwa kinawasiliana na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Rais Paul Kagame wa Rwanda, Mwenyekiti wa Nchi za Jumuiya ya Kusini mwa Afrika (SADC), Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini na Mwenyekiti wa chombo cha kusimamia Siasa, Ulinzi na Usalama (Troika Organ) cha SADC, Rais wa Namibia, Hage Geingob, kuwaelezea kuhusu ukandamizaji wa demokrasia nchini.

Alifafanua kuwa wanamwandikia Kagame kuhusu ukiukaji wa mkataba wa Haki za Binadamu, Demokasia na Uongozi Bora wa EAC ambao Tanzania imeusaini.

Alisema kuna mambo mengi EAC walikubaliana, lakini hayafanyiki na kwamba Kagame ana wajibu wa kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mkataba huo.

Baadhi ya malalamiko kwa mujibu wa Maalim Seif ni kuminywa uhuru wa kutoa maoni.

Kwa upande wa SADC, alisema wanamweleza Mwenyekiti Ramaphosa, ukiukaji wa misingi ya demokarasia na haki za binadamu zikiwamo za kisiasa zilizoko kwenye mkataba wa SADC.

Aidha, alitaja madai ya kukamata wafuasi wa vyama vya upinzani na hofu nyingine zinazotokana na wapinzani kushambuliwa na watu wasiojulikana.

Kadhalika, Maalim Seif, alieleza kuwa kuna sheria za kukandamiza na kudumaza demokrasia na haki za wananchi mojawapo ni Sheria ya Vyama vya Siasa, ya Huduma ya Habari, Takwimu, ya Upatikanaji Habari na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni.

"Sheria hizi ni kandamizi zinazuia uhuru wa raia iwe ni kutoa maoni kwenye vyombo vya habari, mtandaoni na kinyume na ibara ya 18 ya Katiba ya Tanzania," alisema.

Aliongeza kuwa zinazuia kutumia jukwaa lolote kutoa maoni na kwamba wapinzani hawana uhuru wa kujieleza wala kukosoa na mara nyingi sheria hizo zimetumika kukamata watu wanaotumia mitandao kueleza maoni yao.

Aidha, Maalim Seif, aliongeza kuwa wanawasiliana na Troika Organ kwa sababu kuna ukosefu wa usalama ambao unatishia na kuhujumu upinzani na kutoa mfano wa kutishiwa kufutwa ACT- Wazalendo, au kusimamishwa kufanya shughuli za kisiasa kwa mwaka mzima, yeye (Seif) kutishiwa kufungiwa maisha kufanya shughuli za kisiasa.

"Tanzania ni yetu sote. Ni maneno ya mstaafu Benjamin Mkapa, aliyoniambia kwenye muafaka wa pili Zanzibar. Sisi hatuna hati miliki ya Tanzania. Kama raia na viongozi tuendeleze kazi ya waasisi kwa kuweka misingi mizuri ya kiutawala," alisema.

Maalim Seif aliwashauri viongozi kulikumbuka hilo kwa kuwa taifa limekuwa mfano wa usalama na amani, hivyo hakuna sababu ya kuvuruga bali kuimarisha umoja, utaifa na uzalendo.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakikagua baadhi ya bajaji baada ya kuzikamata katika Barabara ya Morogoro, eneo la Ubungo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Lugola awatega polisi dawa za kulevya

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amesema ana taarifa za baadhi ya askari polisi wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya na wengine wanawalinda wafanyabiashara hao ili wasikamatwe.

Lugola alitoa kauli hiyo jana visiwani Zanzibar na kueleza kuwa wanaendelea kuwafuatilia mienendo yao na mwisho watakondolewa kwenye Jeshi la Polisi ili watafute kazi nyingine.

"Baadhi ya askari wangu wanajihusisha na biashara hii ya dawa za kulevya na wengine wanashirikiana na wafanyabiashara wa dawa za kulevya ili wasikamatwe, tunaendelea kuwafuatilia.

"Haiwezekani askari wachache wasio na uadilifu waendelee kuharibu kazi nzuri inayofanywa ndani ya Jeshi la Polisi, lazima tuwabaini na tutawaondoa katika jeshi ili watafute kazi nyingine," alisema Lugola.

Lugola alitoa wito kwa Watanzania wa Bara na Visiwani kwamba vita ya dawa za kulevya ni ya wote, hivyo lazima kila mmoja ashiriki kupambana nayo.

"Wale tutakaowabaini kwamba wanashirikiana na vijana wetu wa Jeshi la Polisi kuendeleza biashara ya dawa za kulevya tutakapowakamata wajue makosa haya hayana dhamana, wataacha familia na watazeekea magerezani," alisema.

Aliwataka wenye tabia kama hizo waache na wakafanye shughuli nyingine za kiuchumi kwa sababu ziko nyingi.

Alisema licha ya dawa za kulevya kuharibu na kuvuruga uchumi, yanaharibu vijana ambao wengi wao huwa mateja na kuchochea kufanya uhalifu mwingine ukiwamo ubakaji, wizi na ujambazi.

"Dawa hizi za kulevya zinaendelea kuwapo Zanzibar kwa sababu miongoni mwenu mnashiriki kwenye biashara hii," alisema Lugola.

## Waandishi 52 wakamatwa, kutekwa 2018

**Na Salome Kitomari**

WAANDISHI wa habari na watetezi wa haki za binadamu 52 nchini wamekamatwa, kushambuliwa na kutekwa kwa kipindi cha mwaka 2018.

Hayo yamo kwenye ripoti ya hali ya watetezi wa haki za binadamu na bango kitita la sheria na sera zinazoathiri nafasi ya asasi za kiraia mwaka 2018, iliyozinduliwa jana jijini Dar es Salaam.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema ripoti hiyo inaonyesha mwaka 2018 kumekuwa na ongezeko kubwa la matukio hayo ambayo ni kinyume cha haki za binadamu, ikiwamo kujeruhiwa na kupotea katika mazingira tatanishi.

Ripoti hiyo ni ya sita toka zianze kutolewa mwaka 2013, hutoa picha ya hali ya nafasi ya asasi za kiraia nchini, ukiukwaji wa haki za binadamu dhidi ya watetezi na hali ya uhuru wa kuzungumza pamoja na ulinzi wa waandishi.

Alisema matukio 52 yaliyoripotiwa dhidi ya watetezi ni ukiukwaji wa haki ikiwamo ukamatwaji, mashtaka mabaya, kutekwa, kushambuliwa, na kufanya shughuli halali za uandishi wa habari kwa uhalifu.

"Takribani watetezi wa haki za binadamu 16 walikamatwa na kushtakiwa kimakosa, kesi mbili walikutwa hawana hatia na zilizobaki zinaendelea mahakamani," alisema.

Olengurumwa alisema ndani ya miaka miwili, 2017-2018 amri za wakuu wa mikoa na wilaya kuwakamata watetezi wa haki za binadamu na raia wengine zimezidi kuongezeka na kwamba watu 17 na watetezi wa haki za binadamu 11 walikamatwa, mwaka 2018.

"Cha ajabu ni kuwa mwaka 2018 hata mawakili walikuwa walengwa kwa kuwa watano walikamatwa kwa amri za wakuu wa wilaya na mikoa. Tunatambua juhudi za Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola na Waziri wa Tamisemi, Suleiman Jafo, kwa kupinga ukiukwaji huu wa haki za binadamu," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya THRDC, Vick Ntetema, alisema watetezi wa haki za binadamu hukusanya taarifa ya ukiukwaji, huchukua hatua kulinda uwajibikaji, hukomesha kutokujali, husaidia utawala bora na sera ya serikali kuchangia utekelezaji wa mikataba ya haki za binadamu, kutoa elimu ya haki za binadamu na mafunzo.

Naye Balozi wa Sweden nchini, Anders Sjoberg, alisema uwapo wa mitandao ya kijamii umesaidia kuongeza uhuru wa wananchi kujieleza ikiwamo kutoa taarifa za matukio ya ukandamizwaji wa watetezi wa haki za binadamu na waandishi wa habari.

## HABARI KITAIFA

# Wasiojulikana walivyomuua katibu CCM

**Na Margaet Malisa,** PWANI

KATIBU wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Njia Nne, Mkuranga mkoani Pwani, Jumanne Bakari (55), ameuawa kwa kuchomwa kisu na watu wasiojulikana usiku wa kuamkia jana.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Kipolisi Kibiti, Onesmo Lyanga, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema mauaji hayo yalitoke saa tatu usiku, ambapo wauaji walimvizia marehemu akiwa njiani akirejea nyumbani kisha kumshambulia kwa kumchoma kisu tumboni na alifariki dunia papo hapo.

Lyanga alisema baada ya askari kufika eneo la tukio walikuta mpini wa kisu kinachodaiwa kutumika kumchoma marehemu.

Kwa mujibu wa Kamanda Lyanga, kufuatia tukio hilo Jeshi la Polisi linafanya uchunguzi ili kuwabaini waliofanya mauaji hayo.

Mwili wa marehemu umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga.



Wafanyakazi wa kampuni ya usafi ya Brecol wakizoa udongo uliotolewa kwenye mitaro ya maji ya mvua kando ya Barabara ya Mandela, eneo la Buguruni Al Hamza, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

## Waziri awajia juu w'biashara sukari

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, amesema kuna taarifa kuwa baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wa sukari wanapenyeza maslahi binafsi katika miradi mikubwa ya serikali.

Masauni aliyasema hayo jana muda mfupi baada ya kutembelea kiwanda na shamba la miwa katika Gereza la Mbigiri, Dodoma ambalo linakadiriwa kuzalisha tani za sukari 200,000 kwa mwaka na kuondoa adha ya kuagiza nje ya nchi.

"Kuna taarifa za baadhi ya wafanyabiashara wakubwa wa sukari kupenyeza maslahi yao binafsi katika miradi hii mikubwa ya serikali ikiwamo shamba hili la miwa hapa Mbigiri, nawaasa waache mara moja kwa kuwa watakapobainika hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kosa la uhujumu uchumi," alisema.

Masauni alisema, serikali imedhamiria kukuza viwanda mbalimbali ikiwamo kiwanda hicho na kuwezesha mamia ya wananchi kupata ajira pamoja na kukuza uchumi wa nchi.

Mkuu wa Gereza Mbigiri, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Shija Fungwe, alisema wafungwa 280 wa gereza hilo wanatumiwa kama nguvu kazi kwenye shamba hilo.

Alisema kazi ya kupanda na ulimaji wa hekta 500 unaendelea na kati ya hizo, hekta 200 zimeshalimwa.

Alisema lengo lao ni ifikapo Juni, mwaka huu wawe wamefikia hekta 700.

Awali, Masauni alielekeza kubadilishwa kwa Mjumbe wa Bodi ya kiwanda hicho, ACP Rocky Mbena, anayewakilisha Jeshi la Magereza.

## Mhandisi aingia matatani tuhuma uhujumu uchumi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MHANDISI wa ujenzi aliyekuwa akisimamia mradi wa ujenzi wa majengo sita ya Hospitali ya Wilaya ya Siha, mkoani Kilimanjaro, ameanza kuchunguzwa kwa tuhuma za uhujumu uchumi.

Uchunguzi huo pia unawahusu wazabuni waliohusika kutoa nondo na tofali zisizo na ubora.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Kilimanjaro, Holle Makungu, alisema mhansisi wa mradi huo aliyekuwa akiusimamia ameondolewa na uchunguzi wa uhujumu uchumi dhidi yake na wote waliohusika wakiwamo wazabuni umeanzishwa.

Alitangaza uamuzi huo jana, wakati akitoa taarifa ya taasisi hiyo ya utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu.

Kwa mujibu wa Makungu, pale uchunguzi huo utakapokamilika hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Katika ufuatiliaji wetu ilibainika kuwa nondo na tofali zilizokuwa zimenunuliwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo zilikuwa chini ya kiwango. Kwa msingi huo tulielekeza nondo na tofali hizo ziondolewe eneo la mradi, wazabuni warudishe fedha zilizokuwa zimetumika kununulia nondo na tofali mara moja.

Mradi huo una thamani ya Sh. bilioni 1.5 ambao umetengewa fedha, unatekelezwa na serikali ya Tanzania, ukihusisha majengo ya utawala, jengo la (mionzi), jengo la dawa, jengo la kufulia, jengo la kuhifadhia maiti na jengo la huduma ya mama na mtoto.

Katika mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Rombo, Takukuru imeeleza kuwa kama ilivyo kwa hospitali nyingine ya aina hiyo, timu yao ya ufuatiliaji imebaini mapungufu katika ujenzi wa ukuta wa jengo la dawa. Hospitali hiyo nayo ilitengewa kiasi cha Sh. bilioni 1.5


JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatano tarehe 04-04-2019 kampuni ya ALBION COMPANY LIMITED itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea MTWARA AIRPORT kupitia NANGURUKURU, gari hilo lenye namba za usajili:
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

T 718 BTC / T 874 CDS

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 23.00 |
| Upana | - | mita | 3.50 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

T 600 BHU / T 441 BVZ

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 23.00 |
| Upana | - | mita | 2.87 |
| Kimo | - | mita | 5.20 |

Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115157002



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**BENKI KUU YA TANZANIA** TAWI LA ARUSHA INATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI YENYE NAMBA YA USAJILI **SU 34159 LAND ROVER 110 PICKUP.**

YEYOTE ATAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI NAMBA **AR/RB/3022/2019**

215156702



MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

**DEBT COLLECTOR AUCTIONEER**
P.O. BOX 75087, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Mobile: + 255 784 622 019, +255 715 622 019, +255 765 999 000 Tel: +255 2184653 Fax +255 0222181477,
Web: www.masetodebtcollectors.co.tz , Email: masetodebtcollectors@yahoo.com or shabani.chuki@yahoo.com

**5th April 2019**

**NOTISI/TANGAZO LA MNADA**

Kwa idhini tuliyopewa na **CRDB BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana ya mdaiwa sugu aliyeshindwa kulipa mkopo wake katika Benki tajwa hapo juu kama atashindwa kulipa deni hilo ndani ya siku 14 tangu kutolewa kwa tangazo hili. Mnada huu utafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | ELIBARIKI KITOI KITOMARI | ELIBARIKI KITOI KITOMARI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI CT NO. 23920 LR MWANZA LO NO.388593 ILIYOKO PLOT NO. 140 BLOCK 'U' NYASUBI, WILAYA YA KAHAMA | 18/04/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, kukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NASI KWA ANUANI ZIFUATAZO:**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**Maseto Auctioneer and debt Collector Ltd,**
**P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787**

215156502

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TRA sasa panueni wigo wa walipakodi

**SERIKALI** yoyote duniani inategemea kodi ili itekeleze majukumu yake ya kuongoza dola na kuwaletea maendeleo wananchi wake.

Bila serikali kukusanya kodi ya kutosha, kamwe haiwezi kuwahudumia wananchi wake; kwa maana ya kuwapa huduma za msingi husuan za kijamii zikiwamo miundombinu, afya, elimu kwa kutaja baadhi.

Pia serikali isiyo makini katika kukusanya kodi haiwezi kujiendesha kwa kulipa mishahara ya watumishi, kugharimia masuala ya ulinzi na usalama na mengineyo. Kodi za serikali hupatikana kwa namna mbalimbali kutokana na vyanzo vilivyopo. Kwa hiyo makusanyo makubwa ya kodi hutegemea na mamlaka husika zinavyobuni vyanzo zaidi vya mapato.

Pale kunapokuwapo na vyanzo vingi makusanyo kuwa makubwa, lakini kinyume chake mapato ni madogo, hivyo serikali kujikuta katika wakati mgumu katika kujiendesha na kutoa huduma za msingi kwa wananchi.

Serikali ya sasa imejitahidi katika makusanyo ya kodi, hali iliyowezesha kuanza utekelezaji wa kasi wa miradi ya maendeleo, ikiwamo ya ujenzi wa mradi wa umeme wa maji wa Stigler's Gorge, reli ya kisasa, ununuzi wa ndege, ujenzi wa barabara za juu, bomba la mafuta na mingine.

Utekelezaji wa miradi hiyo usingewezekana kuanza kama serikali isingeweka mikakati ya dhati ya kuongeza mapato kupitia kodi na nidhamu ya matumizi. Hata hivyo, pamoja na jitihada za kuongeza mapato ikiwamo kuibuliwa kwa vyanzo vipya, bado mapato yanayopatikana hayajaweza kukidhi mpango wa utekelezaji wa miradi zaidi ya maendeleo.

Hali inaonyesha kuna udhaifu nchini ambao unasababisha watu wachache kulipa kodi na wengi kutokuwamo katika mfumo wa ulipaji wa kodi, hivyo kuwaumiza wachache, ambao wanabeba mzigo wa wengi.

Kutokana na hali hiyo, Rais John Magufuli ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Wizara ya Fedha na Mipango kupanua uwigo wa kodi kwa kuongeza idadi ya walipa kodi na kuibua vyanzo vipya vya mapato, pamoja na kujenga mazingira rafiki kwa watu wengi zaidi kulipa kodi ili kuongeza makusanyo.

Rais Magufuli alitoa maelekezo hayo Jumatatu Ikulu jijini Dar es Salaam, na kueleza kutoridhishwa na utendaji wa TRA ambayo mpaka sasa inakusanya kodi kwa walipa kodi milioni 2.7 pekee kati ya Watanzania wote zaidi ya milioni 55, na alisema kwa mtindo huo mamlaka hiyo itakuwa inazidi kuwakamua walipakodi wachache wakati ingeweza kupanua wigo wa kodi na kuweka viwango vya kodi vinavyolipika na vitakavyowavutia watu wengi zaidi.

Kwa kuwa kwa miaka mingi wadau mbalimbali wamekuwa wakishauri serikali kupanua wigo wa vyanzo vya mapato badala ya kutegemea vyanzo vya miaka yote ambavyo ni vinywaji na sigara, kwa kuwa ni wakati mwafaka kwa wataalamu wa serikali kuwa wabunifu kwa kubuni vyanzo vipya ambavyo vitaongeza mapato.

Tunashauri pia TRA ibuni mfumo mpya, ambao utakuwa bora na rafiki, ambao utaongeza idadi ya walipakodi kutoka idadi ya sasa ambayo ni ndogo sana kulinganisha na idadi ya Watanzania inayokadiriwa kuwa zaidi ya milioni 50.

Kwa kufanya hivyo, mapato ya serikali yataongezeka na pengine katika siku za usoni nchi yetu itaondokana na kutegemea fedha za washirika wa maendeleo kwa ajili ya kuchangia bajeti, kutokana na kutokuwa na uhakika na wakati mwingine kutokulipwa au kuchelewa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kupungua ajali barabarani dalili njema kwa uhai wetu

Na Mary Geofrey

**MWISHONI** mwa wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alifungua na kuongoza kongamano la kwanza la kitaifa la Usalama Barabarani lililowahusisha wadau mbalimbali wa masuala ya usafiri na maofisa wa Jeshi la Polisi nchini.

Lengo la kongamano hilo lilikuwa kujadili kwa pamoja na wadau wa usafiri barabarani, kuhusu hali ilivyo sasa na kinachotakiwa kufanyika katika mapambano hayo.

Kundi la wadau hao linajumuisha madereva, wamiliki wa mabasi, Chama cha Kutetea Abiria, asasi za kiraia za kuzuia matukio ya ajali nchini kikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (Tamwa),

Wakati Lugola akifungua kongamano hilo, alitoa takwimu ya kuwapo matukio 3,732 ya ajali mwaka jana, zilizosababisha vifo vya watu 1,788 na majeruhi 3,746.

Alitaja vyanzo vyake na maeneo ya matukio. Hapo inahusisha watembea kwa miguu 259; madereva wa pikipiki 725' waliosababisha ajali kwa mwendokasi 364; madereva wazembe 1,556; walevi 61 na waendesha baiskeli 103.

"Katika kipindi cha mwaka jana pekee jumla ya ajali 3,732 zilitokea nchi nzima ambazo zilisababisha vifo vya watu 1,788 na majeruhi 3,746 na ajali zimesababishwa na uzembe wa madereva, watembea kwa miguu, madereva pikipiki na walevi," anafafanua Lugola.

Ni matukio yanayoonekana kupungua, ikilinganishwa na mwaka 2017, zilitokea ajali 5,574 zilizosababisha vifo vya watu 2,581 na majeruhi 5,489.

Waziri huyo mwenye dhamana ya kusimamia usalama wa raia na mali zao nchini, anaonyesha kuwapo tofauti ya ajali katika miaka hiyo miwili, kwa takwimu za ajali 1,842; vifo 793; majeruhi 1,743.

Ni mafanikio ambayo hayakutokea kama muujiza. La hasha! Ni juhudi za kipekee zilizoongozwa na Jeshi la Polisi, Kitengo cha Usalama Barabarani chini ya Kamanda, Fortunatus Muslim.

Kupitia operesheni aliyoanzisha aliyoibatiza 'Nyakuanyakua' walikamata magari mabovu, madereva wazembe na watumiaji barabara wasiyofuata sheria, pasipo kusahau vyombo vya habari.

Kupungua kwa ajili hizo ziko katika wastani wa asilimia 31. Waziri Lugola anaeleza asilimia 76 ya ajali za barabarani nchini ni matokeo ya makosa ya kibinadamu; asilimia 40 zinawaangukia madereva wazembe.

Waziri Lugola anasema, kupambana na ajali kunaenda sambamba na kudhibiti askari wanaoshirikiana na wahalifu kupokea rushwa. Ahadi yake ataendelea kupambana nao, akinuia kupunguza kama si kumaliza ajali hizo za barabarani.

"Narudia tena maofisa na askari polisi msiotaka kubadilika katika vitendo vya rushwa, siku zenu zinahesabika, kwani taarifa ya kamati ya kuchunguza vitendo hivyo vya rushwa katika Kikosi cha Usalama Barabarani, tayari nimeshapewa iko mezani kwangu inapumua," Lugola alisisitiza mkutanoni.

Katika hili, inaelezwa kuwa wananchi na watumiaji barabara, wana wajibu wa kuhakikisha wanaunga mkono kwa kuzingatia sheria za usalama barabarani.

Kila mtu anapaswa kuhakikisha kufuata sheria zilizowekwa za Usalama Barabarani, ili kuepuka ajali zinazopoteza maisha ya Watanzania wengi.

Takwimu zinaonyesha watembea kwa miguu 259 walitajwa kusababisha ajali za barabarani, ni wazi kuwa mtu mmoja mmoja anaweza kusababisha ajali ya gari na kupoteza maisha ya wengi.

Pia, inatukumbusha kuwa watembea kwa miguu ni chanzo cha ajali za barabarani ingawa watu wanaamini walioslama ni wale wanaotembea kuliko kutumia chombo cha moto.

Ni muhimu sasa wananchi wakatambua hata kama unatembea kwa miguu unaweza kuwa chanzo cha ajali ambayo inaweza kusababisha maisha ya Watanzania wenzako.

Kila Mtanzania na mtumiaji wa barabara ana wajibu wa kuwa mwangalifu kutembea kwa tahadhari na kuvuka barabara baada ya kujiridhisha.

Ni vyema watumiaji wa barabara kuacha tabia ya kujiamini kupita maelezo na kutumia eneo la pundamilia kama sehemu ya kufanya madaha au kuvuka wakati wowote bila kujali kuna gari karibu au laa.

Ni jukumu langu mimi na wewe kuhakikisha tunazuia ajali za barabarani na kuhakikisha tunazingatia alama zilizowekwa ili vifo vinavyotokana na ajali vipungue kama si kumalizika kabisa.

Juhudi hizi za serikali na jeshi la polisi zitazaa matunda kama jamii nasi tutaweka juhudi katika kulinda usalama wetu kwanza pindi tuwapo barabarani.

## BARUA/MJADALA

# Wauzaji maziwa wafuatiliwe

***Mhariri,***

*NISEME kwa kadri umri wangu ulivyo, nimebahatika kushuhudia vipindi vyote vitano vya uongozi wa nchi nikiwa na akili zangu timamu.*

*Jambo mojawapo ninalokumbuka likiendelea kuwapo leo hata kesho, ni msisitizo katika sekta ya kilimo, ambayo pindi inapotajwa, maana kuu inasimama hata kugusa sekta ya mifugo, kwani ni vigumu sana kuvitenganisha.*

*Usemi ambao umetawala sekta hizo "Kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi." Hapo kuna maana kubwa, ikizingatiwa lingine kuna wastani wa robo tatu ya umma wa Watanzania na ushee iko huko.*

*Hivyo, nami nabaki katika mtazamo kwamba jamii hiyo inapaswa kuungwa mkono.*

*Kuhusu ufugaji wa maeneo ya mijini, ambako nimeshuhudia pindi mifugo hiyo inapotibiwa na kupewa dawa, basi kunakuwapo ushauri, mathalan wale ng'ombe wanaokamuliwa maziwa, husimamishwa kwa muda, kama wiki moja maziwa hayo yanatakiwa yakamwagwe, kwani si salama kwa afya ya mnywaji.*

*Ni bahati mbaya sana, inapokuwapo sharti hilo kuna wamiliki wa ng'ombe hupendekeza kipaumbele cha kuendelea kuuza maziwa hayo ambayo si jambo jema kabisa kwa afya ya mnunuzi anayoyatumia.*

*Hali hiyo imewafanya hata watumiaji wengi kukimbilia mbadala wa maziwa ya kopo na mengine ya madukani, baadhi yakiwa ghali zaidi.*


*Itakuwa vyema kwa mamlaka za kiserikali zinazosimamia usalama wa vyakula na afya kwa jumla, kuanza kuchukua hatua kwa kushirikiana na jamii mitaani, kupitia elimu hata sheria, kukabili udhaifu huo usiokubalika.*

***Latifa Hamudi,***
***Makambako.***


**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**


# TB si tatizo kabisa, tujiulize kinachotukwaza nini hasa?




**Na Sabato Kasika**

INAKADIRIWA kuna wagonjwa 63,000 wa kifua kikuu (TB), wanaosajiliwa kila mwaka nchini. Pia, inasemekana kila mwaka watu milioni tisa duniani, huambukizwa ugonjwa huo.

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma, Dk. Beatrice Mutayoba, ni kwamba Tanzania imo katika nafasi za juu duniani kati ya nchi zenye wagonjwa wengi wa kifua kikuu.

Wataalam wa afya wanasema, TB ni ugonjwa hatari wa kuambukizwa, unaosababishwa na aina mbalimbali za bakteria zijulikanazo kama 'mycobacterium tuberculosis.'

Kifua kikuu kinaathiri mapafu, pia kinaweza kuathiri sehemu nyingine za mwili na husambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine, kupitia hewa wakati anapokohoa, kupiga chafya, au mate yake yakiwa hewani.

Hapa ndipo ninataka kujadili kidogo kuhusu maagizo yaliyowahi kutolewa na Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, kwenye maadhimisho ya Siku ya Kifua Kikuu Duniani, mwaka jana.

Mkuu huyo aliagiza kumkamatwa kwa mtu yeyote atakayetema mate ovyo barabarani na kutozwa faini kama ilivyo kwa wachafuzi wengine wa mazingira. Lengo, ni kukabiliana na maambukizi ya kifua kikuu.

Anasema katika kukabiliana na ugonjwa huo ni lazima kila mtu atekeleze wajibu wake, ikiwamo kukinga vinywa kwa kitambaa pindi anapopiga chafya au kukohoa, hususan kwenye maeneo ya mikusanyiko na vyombo vya usafiri wa umma, ambako kuna msongamano mkubwa wa watu.

Ni bahati mbaya, kwa baadhi ya watu ustarabu uimewapita kando, kwani wamekuwa wakikohoa na kutema mate ovyo au kukohoa na kupiga chafya, bila ya kufunika midomo, hali inayojemga mazingira ya maambukizi kwa wengine.

Iwapo jamii itaweka ustarabu huu unaoshauriwa, naamini itasaidia kupunguza ugonjwa huo hatari, hivyo agizo la Mkuu wa Wilaya Mjema, itafuatwa na viongozi wengine kwenye maeneo yao, ili kusaidia kuidhibiti TB.

Sote tukumbuke kwenye mkusanyiko wa watu, kila mmoja ana maradhi yake, sasa ikitokea mtu mwenye TB akatema mate ovyo, maana yake ni kwamba kuna uwezekano mkubwa wa kuambukiza wengine ugonjwa huo.

Lakini katika jamii tunayoishi, ndani ya maeneo mbalimbali, kumekuwapo mtindo wa kupuuzia maelekezo. Sasa hali hiyo ikiendelea, ni wazi tunarahisisha au kuruhusu TB kuendelea kujikita katika maisha yetu na madhara yake yako bayana.

Dalili za kawaida za TB ni kuwepo kikohozi sugu na watu kukohoa damu, homa, kutokwa na jasho usiku, kukonda, mtu asipotibiwa, inaua wengi.

Kuna msemo: "Kinga ni Bora Kuliko Tiba." Hivyo, kwa kuwa jamii inaelekezwa isiteme mate ovyo mitaani au kukohoa bila ya kufunika midomo na vitambaa, basi izingatie hilo.

Hili ni jambo la ustaarabu tu linaloweza kuepusha jamii na tatizo la kuambukizana na TB, kwa uzembe kama huo wa kutema mate ovyo au kutojifunika wakati wa kukohoa au kupiga chafya katika mkusanyiko wa watu.

Lakini kama baadhi ya watu wataendelea kuwa wabishi na kujifanya wanajua, itachukua muda mrefu kutokomeza ugonjwa huu ambao serikali imekuwa ikifanya kila jitihada za kuumaliza nchini.

Miongoni mwa jitihada hizo ni kuanzisha vituo vingi vya kutolea tiba ya ugonjwa huo huku dawa zikigawiwa bure ili Watanzania wote waliokumbwa nao waweze kunywa na hatimaye kupona.

Hatua hizo ni kuungwa mkono, kwa vile jamii imekuwa ikielimishwa na kutambua jinsi ugonjwa huo unavyoambikiza, kinachotakiwa kuzingatia ni kufuata maelekezo ya jinsi ya kuueopuka.

## KABWELA — NA FADHIL MOHAMMED



## Hatima ya Lema kujulikana leo

INATOKA UK. 3

alipewa hati ya wito kufika mbele ya Kamati ya Maadili Alhamisi ya wiki hii (leo).

Lema alidai kuwa tayari anajua kinachofuata dhidi yake na tayari ameshakata tiketi kurejea nyumbani Arusha kuendelea na shughuli nyingine.

"Jana (juzi) nilipokea barua ya kunitaka kwenda kwenye Kamati ya Maadili kesho (leo) saa nane mchana, lakini kwa bahati mbaya ndani ya Bunge leo (jana), Spika ameona ni bora amalizane na mimi kesho (leo)," Lema alisema na kueleza zaidi:

"Mimi nimwambie Mheshimiwa Spika, siogopi kumalizana naye, siogopi kufukuzwa Bunge, ninaogopa kumkosea Mungu katika kazi yangu ya ubunge.

"Leo (jana) Spika amekuja bungeni, kasema niende leo (jana) saa nane, nimeshajiandaa na ninaenda kuongeza kile ninachokiamini. Sitayumba, nitaongea kile ninachokiamini.

"Nimejiandaa kisaikolojia. Ninajua safari yangu ya kuwa Dodoma kwa miezi yote hii mitatu ya Bunge la Bajeti inaishia kesho (leo). Na nimeshafanya 'booking' ya safari yangu ya kurejea nyumbani Arusha ili nikaendelee na kazi zangu zingine."

**KILICHOMPONZA LEMA**

Wakati wa kikao cha Bunge juzi, kabla ya chombo hicho cha kutunga sheria kuridhia pendekezo la kumfungia Mbunge wa Kawe, Halima Mdee (Chadema) kuhudhuria vikao vya mikutano miwili kuanzia juzi, Lema alinukuu maneno yaliyomponza mbunge wa chama chake (Mdee) kisha akaunga mkono kuwa "Bunge ni dhaifu".

"Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama ninaweza kushawishi Bunge kuondoa adhabu ambayo imeshapendezwa na Mwenyekiti wa Kamati. Maneno yafuatayo ndiyo yanamfanya Halima apendekezewe adhabu kubwa kiasi hicho, nayanukuu;

'Kitendo cha CAG kusema kwamba hali si nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni cha kijasiri na nina imani wanaoongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu. Hawatafikiri kumwita kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu... 'Roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge, sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli, na mimi kama mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo'.

"Mheshimiwa, na mimi mbunge wa vipindi viwili, nathibitisha Bunge hili ni dhaifu," Lema alisema.

Kutokana na kauli hiyo, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliyekuwa anaongoza mjadala huo, alimtaka Lema kufika mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhojiwa.

# JPM aagiza makandarasi wa ovyo wasipewe kazi

INATOKA UK. 3

barabara. Huwezi kusubiri ujenzi wa barabara ya kilometa 50 kwa miaka mitatu," alisema.

Alisema kuna makandarasi ambao wamepewa kazi ya kujenga barabara na kila siku wako eneo la kazi, lakini kazi haimaliziki hawafai kuendelea kupewa miradi ya ujenzi.

"Kuja kwangu leo Mtwara, mkandarasi na Wizara ya Ujenzi mmeingia kwenye kumi na nane zangu. Wizara ya Ujenzi msimpe kazi yoyote mkandarasi huyu hadi atakapomaliza kazi hii. Tanzania siyo sehemu ya majaribio, ni sehemu ya kazi," alisema Rais Magufuli.

Kwenye hotuba yake, Rais Magufuli alieleza kutoridhishwa na ujenzi wa barabara hiyo.

"Nimefurahi kuona mradi huu umeanza kutekelezwa, napenda kukiri kwa dhati kabisa sijafurahishwa na kasi ya ujenzi wake. Mradi hauendi vizuri. Mkandarasi wa hapa tangu mwaka jana anahangaika na kilometa 50, angepewa kilometa 200 si angemaliza kwa miaka 200," alihoji Rais Magufuli.

Alisema rekodi ya mkandarasi huyo katika ujenzi wa barabara nchini siyo nzuri na alishangaa kupewa tena zabuni ya ujenzi wa barabara hiyo.

"Makandarasi wa ovyo ovyo ndiyo wanapewa kazi, huyu kandarasi hakufanya vizuri kwenye barabara ile ya Same-Mkumbara, ila kwa kuwa mlitangaza zabuni akashinda sasa ahakikishe hii barabara anaimaliza," alisema Rais Magufuli na kuongeza.

"Nikuombe mkandarasi ufanye kazi usiku na mchana, hatuwezi kusubiri barabara tangu mwaka 2017, 2018, 2019, watu hawajaona barabara, unachimba chimba mashimo tu. Tuta lenyewe umeweka asilimia 60, haiwezekani," alisema.

Rais Magufuli aliongeza kuwa kukamilika kwa barabara hiyo kutarahisisha usafiri pia kuchochea shughuli mbalimbali za kiuchumi. Alisema mkakati wa serikali ni kuufanya Mkoa wa Mtwara kuwa wa kimkakati na kitovu cha uchumi, hususani kwa mikoa ya kusini. Alisema miradi inayotekelezwa mkoani Mtwara ikiwamo upanuzi wa bandari (Sh. bilioni 137), upanuzi wa uwanja wa ndege (Sh. bilioni 50) pamoja na ujenzi wa barabara hiyo (Sh. bilioni 89.59) zimegharamiwa na serikali kwa makusanyo ya kodi.

Aidha, aliwataka wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Mtwara kuhakikisha wanasimamia zao la korosho ili waweze kupata ushuru.

Alisema endapo watahitaji ushuru wanatakiwa kuhakikisha wanasimamia vizuri zao hilo na kuhakikisha wakulima wanalipwa pesa nzuri.

# CAG afunguka kutengwa na Bunge

INATOKA UK. 2

hivyo kama limeamua kwamba halitafanya kazi naye ni vigumu kutofautisha CAG na ofisi.

"Ni vigumu sana kutofautisha mimi na ofisi kwa sababu Katiba inahitaji ofisi yangu na haihitaji Ofisi ya Mkaguzi, linahitaji tathmini kali ya watu wenye uelewa mpana kutazama athari zake ni zipi, tukifanya maamuzi ambayo hatujatazama athari zake inaweza kuwa tatizo kubwa zaidi badala ya ufumbuzi," alisema.

Kufuatia uamuzi wa Bunge kumeibuka utata wa namna Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo CAG ni bosi wake, itakavyotekeleza majukumu yake bila kulishirikisha Bunge.

Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, inamtaka CAG kuwasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa

Kwa mujibu wa Ibara hiyo, baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye mkutano wa kwanza wa Bunge utakaofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika mkutano huo kabla ya kupita siku saba tangu siku ulipoanza.

**MSEKWA ATOA NENO**

Akitoa maoni yake kuhusu msimamo wa Bunge kuhusiana na uamuzi dhidi ya CAG, aliyewahi kuwa Spika wa Bunge, Pius Msekwa (pichani), amesema walichokataa wabunge ni mtu ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na siyo ripoti ya ukaguzi wa mwaka wa fedha za ofisi yake.

Msekwa alisema kwa sababu amekataliwa CAG haina maana kwamba ripoti zitaachwa kujadiliwa na Bunge.

"Anayekataliwa ni CAG ambaye ni mtu na siyo ripoti, ripoti ni ya ofisi yake na idara ya CAG ina watu wengi waliofanya kazi ya kuandaa hiyo ripoti hakuandika yeye binafsi, hebu fikiria kama angejiuzulu leo ina maana hiyo ripoti angeondoka nayo?" alihoji.

"Kazi ameshaifanya na kuikamilisha, ameiwasilisha kwa Rais John Magufuli... ni wajibu wa Rais sasa kuipeleka bungeni ili ikafanyiwe kazi kama miaka yote," alisema Msekwa na kuongeza:



"Hapo tunatakiwa kutenganisha mtu na kazi ...Bunge limemkataa mtu kwa maneno aliyoyasena na kuliudhi Bunge na siyo kazi yake."

"CAG ataamua ni lipi kati ya hayo mambo mawili na uamuzi ni wake kusema mmeniona sifai naondoka ama kusema mmenionea naendelea na kazi," alisema Msekwa. Aidha, Msekwa alisema katika kipindi chake cha uongozi akiwa Spika halikuwahi kutokea tukio la aina hiyo la Bunge kukataa kufanyakazi na CAG.

"Wakati wangu hili jambo halikuwahi kutokea, kila jambo lina wakati wake kwa kuwa halijawahi kutokea haina maana halitatokea milele na milele. Hapana maisha ya binadamu yanabadilika badilika," alisema.

Aliongeza: "Kwa uzoefu wangu wa kazi naweza kusema sina uzoefu na tukio kwa sababu halijawahi kutokea wakati wangu, lakini limetokea sasa na limetokea kihalali."

Aidha, alisema Bunge lina madaraka ya kufanya hayo ambayo wameyafanya kwa sababu Bunge lina madaraka ya kusema hawana imani na Waziri Mkuu. "Kama wanaweza kusema hawana imani na Waziri Mkuu watashindwaje kusema hawana imani na kiongozi mwingine. Kwa hiyo hakuna shaka hawajatoka nje ya utaratibu," alisema Msekwa.

**Imeandikwa na Romana Mallya na Beatrice Shayo.**

# Hatima mali za DECI mwezi ujao

INATOKA UK. 2

biashara hizo zilizowafanya wapate fedha na mali hizo, katika kiapo chao hakuna ushahidi, ushahidi pekee upo katika kiapo chetu," alidai DPP.

Katika maombi ya msingi, DPP Mganga aliwasilisha maombi hayo mahakamani hapo, akiomba itoe amri ya kutaifishwa kwa mali za kampuni hiyo yakiwamo magari 11, nyumba na viwanja vinane na fedha ziwe nali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Katika maombi hayo, DPP anaiomba mahakama hiyo kutoa amri ya kutaifishwa na kuwa mali ya serikali, nyumba namba UKMMD/1237 iliyoko Mwembe Madafu, Ukonga, Dar es Salaam, kiwanja namba 651, kitalu 'M' kilichopo Forest area, Mbeya, nyumba iliyoko kiwanja namba 7, kitalu 'P' ikiwa na hati namba 033004/23 kilichopo mtaa wa Rufiji, Manispaa ya Mwanza.

Mali nyingine ni ardhi iliyoko katika kiwanja namba 2/283/2 kitalu "E" Mabibo, Kinondoni, Dar es Salaam, kipande cha ardhi ambacho hakijapimwa kilichopo kijiji cha Manyinga, Turiani, Mvomero, Morogoro na kiwanja namba 467 kilichopo kitalu "H" kikiwa na hati ya usajili namba 48170 kilichopo eneo la Tegeta, Dar es Salaam.

Pia nyumba iliyoko kiwanja namba MM/19/P kilichopo Manzese karibu na barabara ya Morogoro, Dar es Salaam na nyumba iliyoko katika kiwanja namba KND/MXS/MNM/Z ikiwa na leseni ya makazi namba KND 008337 Kinondoni, Dar es Salaam.

Magari ambayo DPP anaiomba mahakama kutoa amri ya kutaifishwa na kuwa mali ya serikali ni Toyota Premio namba T 132 AWJ, Toyota Land Cruiser namba T 480 AUP, Toyota Rav 4 namba T 274 ATQ, Toyota Mark II namba T 676 AYP, Subaru Legacy namba T 682 AUT, Toyota Ipsum namba T 850 AXY, Toyota Ipsum T455 ADM, Toyota Mark II T 186 AYX, Mitsubishi Pajero T 852 AAV, Toyota Lande Cruiser T 789 AUX na Nissan Terrano namba T 899 AYU.

Kadhalika, DPP anaomba mahakama kutoa amri ya kutaifishwa kwa fedha zilizoko benki katika akaunti namba 22601601056 iliyoko NMB, tawi la Msasani Sh. 12,503,068,647.89.

Fedha nyingine taslimu ni zilizoko katika akaunti namba 0001201000000194/1 iliyoko Dar es Salaam Community Bank (DCB), tawi la Uhuru ikiwa na Sh. 1,457,700,462.49 na fedha taslim zilizoko katika akaunti namba 021140019558 iliyoko Kenya Commercial Bank (KCB), tawi la Samora, Dar es Salaam, ikiwa n ash. 57,933,304.10.

Kupitia maombi hayo, DPP anaiomba mahakama itoe amri nyingine itakayoona zinafaaa.

## HABARI KITAIFA

# WFP kupambana utapiamlo watoto chini ya miaka 2

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Idara ya Elimu na Mafunzo ya Lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Sikitu Saimon, amesema Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) kupitia mradi wa Boresha Lishe, umepanga kugawa virutubishi mchanganyiko katika mikoa ya Dodoma na Singida kwa ajili ya kupambana na utapiamlo kwa watoto chini ya miaka miwili.

Sikitu alisema hayo wakati wa mafunzo ya matumizi ya virutubishi mchanganyiko kwa watoa huduma za afya wa mikoa ya Dodoma na Singida yanayofanyika kwa siku tatu jijini Dodoma kwa washiriki kutoka wilaya za Bahi, Chamwino, Ikungi na Singida Vijijini.

Alisema mafunzo hayo yanalenga kuwajengea uwezo watoa huduma katika vituo vya kutolea huduma ili waweze kuwasimamia na kuwaelekeza walengwa njia sahihi ya matumizi ya virutubishi hivyo kwa ajili ya kupambana na utapiamlo.

"Tanzania sasa tunakabiliwa na aina mbili za utapiamlo; utapiamlo wa virutubishi vilivyozidi na utapiamlo wa upungufu wa virutubishi. Aina ya kwanza ya utapiamlo inawakabili sana watu wazima, lakini hii aina ya pili inawakabili sana watoto wadogo chini ya miaka mitano. Athari ya utapiamlo kwa mtoto, huathiri ukuaji wake kimwili na kiakili, na matokeo yake hata shuleni tunapata wanafunzi wasiofundishika au wasioelewa," alisema.

Alisema wakati sahihi wa kupambana na utapiamlo kwa mtoto ni katika siku 1,000 za mwanzo ya maisha yake kwa kuhakikisha mama anapokuwa mjamzito anapewa lishe bora, na mtoto anapozaliwa kwa miezi sita ya mwanzo anyonyeshwe maziwa ya mama pekee na anapotimiza umri wa miezi sita hadi miaka miwili ni kuhakikisha anapewa chakula kilichoongezewa virutubishi mchanganyiko.

Ofisa lishe kutoka WFP, Neema Shosho, alisema kwamba mradi wa Boresha Lishe unatekelezwa katika wilaya nne za mikoa ya Dodoma na Singida ambazo ni Bahi na Chamwino kwa Mkoa wa Dodoma, Ikungi na Singida Vijijini. Alisema mradi huo unatekelezwa kwa muda wa miaka mitano kuanzia 2017 na utakamilika mwaka 2022 na awali mradi ulikuwa unagawa unga wa kutibu utapiamlo wa kadiri na unga lishe kwa wajawazito, wanawake wanaonyonyesha, na watoto wenye umri chini ya miaka miwili, zoezi lililokuwa linafanyika kila mwezi kwa mwaka mzima.

"Baada ya kufanyika tathmini na kubaini kuwa chakula kinachozalishwa na kaya katika maeneo ya mradi kinakuwa hakina virutubishi vya kutosha.




Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Afrika, Balozi Mwanaidi Maajar (wa pili kulia), akimpongeza Mkurugenzi Mtendaji mpya wa benki hiyo, Joseph Iha, katika hafla fupi iliyofanyika, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Samir Yassine na Meneja Mkuu wa Mikopo, Ellis Katwebaze. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Wataalamu wanolewa uandaaji miradi

**Na Mwandishi wetu,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya (TIB) kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeandaa mafunzo kwa watumishi 150 wa halmashauri kutoka mikoa mitatu ya Tanzania Bara kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kuandika miradi ili iendane na vigezo vya kibenki.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utoaji wa mafunzo hayo jijini Dodoma, Meneja wa Uendelezaji Biashara wa TIB, Joseph Chilambo, alisema kumekuwa na changamoto kubwa ya uandishi wa miradi na hivyo halmashauri nyingi kushindwa kupata mikopo ya miradi ya maendeleo.

"Mafunzo haya yatakwenda kuwajengea uwezo watumishi wa halmashauri katika uandaaji wa miradi ili iweze kukubalika kwa urahisi na benki au taasisi za kifedha kutoa mikopo hali itakayopelekea maendeleo katika halmashauri zetu nchini," alisema Chilambo.

Alisema uandaaji mzuri andiko la miradi linajenga imani kwa taasisi za kifedha na benki katika kutoa mikopo kwa wakati na kusababisha maendeleo kukua katika halmashauri husika ambapo mradi utakwenda kutekelezwa na uchumi kukua.

"Tunawafundisha mbinu na kanuni mbalimbali za uandaaji wa maandiko ya miradi ikiwamo ushirikishwaji wa watu wa taaluma tofauti katika kutengeneza andiko la mradi, kwa kuwa andiko lolote ni lazima lihusishe watu wa taaluma tofauti ili kutoa wigo mpana wa mawazo katika uandaaji wa miradi," alisema Chilambo.

Alifafanua kuwa andiko la mradi litakamilika kwa kushirikisha watu wa taaluma ya kiuchumi, kifedha, kijamii na kimazingira, kwa kufanya hivyo miradi mingi itakubalika na taasisi za kifedha na kupelekea upatikanaji wa mikopo itayotumika katika miradi husika na maendeleo katika halmashauri.

"TIB imekuwa ikishirikiana na halmashauri nchini katika kutoa mafunzo ya uandikaji wa miradi kwa kuwa miradi mingi imekuwa ikichukua zaidi ya miaka miwili kupitishwa na benki kutokana na kutokidhi vigezo vya benki husika," alisema Chilambo.

Katibu Tawala Mkoa wa Dodoma, Maduka Paul Kessy, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kwenda kufanyia kazi kwa uweledi, maarifa watakayopata yakawajenge katika kuandika miradi yenye kukubalika ili kuzifanya halmashauri ziinuke kimaendeleo.

## TADB yafagilia kiwanda nyama

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), imeahidi kuunga mkono kwa dhati wawekezaji na wadau wengine stahiki ili kiwanda cha kusindika nyama kinachotarajiwa kujengwa Ruvu, Mkoa wa Pwani kifanikiwe na kutoa mchango mkubwa katika sekta za ufugaji na viwanda.

Akizunguza na waandishi wa habari katika hafla ya utiaji siani makubaliano ya ujenzi wa kiwanda hicho kati ya Serikali na Kampuni ya NECAI ya Misri jijini hapa, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Japhet Justine, alipongeza makubaliano hayo na kusema ujenzi wa kiwanda hicho utakuwa ni kati ya chachu ambazo zimekuwa zikisubiriwa katika kuongeza minyororo ya thamani katika sekta ya ufugaji na kuinua maisha ya wafugaji makini wa Tanzania.

"Sisi tunapongeza na kukaribisha makubaliano haya kati ya serikali na mwekezaji kutoka Misri. Tunaiona hatua hii inalenga kuleta mageuzi makubwa kwa wafugaji hapa nchini. Tunalihakikishia taifa, serikali, mwekezaji na wafugaji kwamba tunaunga mkono kwa dhati hatua hii na tutaoa ushirikiano wa kipekee kuhakikisha kiwanda kinakuwa endelevu na kinanufaisha vilivyo wafugaji makini nchini," aliahidi Justine.

Alisema usindikaji nyama ni mingoni mwa minyororo ya thamani inayoupa maana ufugaji wa Tanzania na kuinua maisha ya mfugaji.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Ufugaji na Uvuvi, Prof. Elisante ole Gabriel, alieleza kuwa kuwapo kwa kiwanda hiki kutaibua mnyororo wa thamani utakaogusa maeneo matatu; wanyama walio hai, uzalishaji na uchakataji nyama na uongezaji wa thamani ya ngozi.

Uanzishaji wa kiwanda hicho utakuwa ni moja ya hatua muhimu katika kuinua pato la wafugaji na kuyafanya mazao ya sekta ya ufugaji kuwa ni malighafi ya moja kwa moja kwa viwanda nchini.

Serikali ya Rais John Magufuli inatekeleza kwa juhudi kubwa sera ya kuifanya Tanzania iwe na uchumi wa kati na wa viwanda ifikapo 2025.

# Ndugai aonya wabunge kubebesha watoto mizigo

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewatahadharisha wabunge kutotumia watoto kuwabebea mizigo sokoni jijini Dodoma kwa kuwa watakapokamatwa watatozwa faini ya Sh. 50,000.

Spika Ndugai alitoa kauli hiyo jana bungeni kwenye kipindi cha maswali na majibu, baada ya baadhi ya wabunge kuhoji udhibiti wa watoto wanaobeba mizigo hususan kwenye masoko.

Awali, katika swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Mgeni Jadi Kadika, alihoji serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha inaondoa tatizo la watoto wanaotoa huduma ya kubeba mizigo Dodoma na kupewa ujira mdogo na hufanya hivyo kwa kukosa haki za msingi kwenye malezi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Josephat Kandege, alibainisha kuwa huduma za ulinzi wa mtoto zinatekelezwa kupitia Sheria ya Mtoto Namba 21 ya Mwaka 2009.

Aidha, alisema tathmini imebaini kuwa watoto wengi wanaojihusisha na kazi ya kubeba mizigo masokoni ni matokeo ya umaskini uliokithiri kwa baadhi ya kaya, kuondokewa na wazazi wao kwa maambukizi ya Ukimwi, migogoro ya ndoa na ukatili dhidi ya watoto.

Alisema mkakati unaoelekezwa na serikali ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu haki za msingi za mtoto kupata elimu na malezi bora.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mtambile (CUF), Masoud Abdallah Salim, alisema bado kuna ongezeko kubwa sana la watoto wa mtaani katika Jiji la Dodoma likiwamo eneo la sokoni.

"Tuambie mkakati mahsusi wa kukabiliana na ongezeko hili, maana linatisha na wazazi wa watoto hawa wapo tunataka kujua mkakati wa kuhakikisha wazazi wa watoto hawa wanapatikana na kuchukuliwa hatua?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kandege alisema jitihada za makusudi zimefanyika ikiwamo wazazi kuunganishwa na wazazi wao.

"Ni wajibu wa jamii kwa jumla kuhakikisha watoto wanaenda shule na hawaishi kwenye mazingira magumu," alisema.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fatuma Toufiq, alihoji serikali ina mkakati gani wa kudhibiti watu wanaotumia watoto kuombaomba.

Naye Mbunge wa Kuteuliwa, Abdallah Bulembo, alihoji hatua gani zinachukuliwa kuondoa omba omba ili watalii waondokane na adha ya kunyang'anywa vitu jijini Dar es Salaam.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema katika sensa waliofanya wamebaini kuna watoto wa mitaani 6,000 na wengi wapo majiji makubwa.

Alisema jukumu la malezi ya watoto ni familia na inapotokea hakuna wa kuangalia watoto serikali huwachukua watoto hao.



Spika wa Bunge, Job Ndugai (kushoto) akizungumza na Spika wa Bunge la Misri, Dk. Ali Abdel Aal Sayyed Ahmed alipomtembelea Ofisini kwake Bungeni Jijini Dodoma jana. Spika wa Misri yupo nchini kwa ziara ya kuboresha mahusiano baina ya nchi hizi mbili.
**PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Bil. 200/- zalipwa wazabuni 2,000

JUMLA ya wazabuni 2,048 wamelipwa madai yao kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 199 tangu kutolewa tamko na Rais John Magufuli Januari 3, mwaka jana.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji tangu Rais atoe tamko kuwa wazabuni wote wanaidai serikali walipwe, wamelipwa wangapi.

Akijibu swali hilo, Dk. Kijaji alisema kati ya wazabuni hao waliolipwa 1,277 walihudumia sekretarieti za mikoa na 771 walihudumia wizara, taasisi na wakala wa serikali.

Alisema kati ya Sh. bilioni 199 ambazo zimetumika kulipa wazabuni hao, ambapo Sh. bilioni 3.72 zimetumika kulipa wazabuni waliotoa huduma kwa sekretarieti za mikoa na Sh. bilioni 195.3 kulipa wazabuni wa wizara, taasisi na wakala wa serikali.

Aidha, alisema madai hayo yalilipwa baada ya uhakikiki kufanyika na kulihakikishia bunge na wananchi kwa ujumla kuwa serikali itaendelea kulipa madai mbalimbali ya wazabuni kulingana na upatikanaji wa fedha sambamba na uhakiki wa madai husika.

"Ili kukamilisha zoezi la uhakiki kwa wakati, wazabuni wote wanaombwa kutoa ushirikiano, hususan kuwasilisha taarifa na vielelezo sahihi vya madai yao pindi wanapotakiwa kufanya hivyo," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema kuna baadhi ya makandarasi wamefanyiwa uhakiki lakini hawajalipwa huku wengine wakipata msongo wa mawazo.

"Je, serikali inatumia njia gani kuhakikisha wanawalipa makandarasi hao kwa wakati?" Alihoji.

Naibu Waziri huyo alijibu kuwa makandarasi wote watalipwa kulingana na upatikanaji wa fedha na kumtaka mbunge huyo kuwa na subira wakati mchakato ukiendelea.

## Agizo la JPM vijiji hifadhini lafafanuliwa

WIZARA ya Maliasili na Utalii imesema agizo la Rais John Magufuli la kuviondoa vijiji vyote 366 vilivyoainishwa kuwa na mgogoro na maeneo ya hifadhi, halimaanishi wananchi wameruhusiwa kuvamia maeneo hayo.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Constantine Kanyasu, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Chalinze (CCM), Ridhiwani Kikwete.

Katika swali lake, Kikwete alisema katika kikao cha kazi, Rais akiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alitoa maelekezo ya kutoondoa vijiji vilivyomo katika maeneo hayo.

"Je, tangazo hili linamaanisha kuwa wameruhusiwa kuendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo yao wanayoishi?" Alihoji.

Pia, alitaka kujua ni lini sasa serikali inarudi kushughulikia migogoro ya mipaka baina ya vijiji hivyo na hifadhi au tamko hilo maana yake wanavijiji wanaendelee kama hakukuwahi kuwa na mgogoro.

Akijibu swali hilo, Kanyasu alisema baada ya maelekezo ya Rais, kamati maalum iliundwa kwa lengo la kumshauri Rais namna bora ya kutekeleza agizo hilo.

"Kamati hii inaongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, wizara zingine zinazohusika ni Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Wizara za Maliasili na Utalii, Mifugo na Uvuvi, Tamisemi, Ulinzi, Kilimo na Maji na Umwagiliaji," alisema.

Hata hivyo, alisema jukumu la kamati litakapokamilika, taarifa itawasilishwa kwa Rais na maelekezo yatatolewa kwa wananchi.

Kufuatia kamati kukamilisha kazi yake, Wizara ya Maliasili itapitia upya mipaka ya hifadhi mbalimbali kwa kuzingatia ushauri wa kamati na maelekezo ya Rais na kazi hiyo itahusisha uwekaji vigingi katika mipaka hiyo.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Waliojikwamua kiuchumi Tasaf kuondolewa kupisha wengine

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

NAIBU Waziri Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, amesema wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini ambao wamejikwamua kiuchumi wataondolewa kwenye mpango huo ili kupisha wengine.

Mpango huo upo chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Akifungua mkutano wa kimataifa wa Transfer Project, unaoendelea jijini hapa na kuzishirikisha nchi zaidi ya 25, Mwanjelwa alisema, utaratibu wa kuwaondoa wanufaika hao unatarajiwa kuanza Juni mwaka huu.

Alisema kwa sasa kaya hizo zitatambuliwa kwa njia ya kielektroniki na mashine ya ramani (GPS) ili kubaini kaya ambazo hazistahili kuingizwa katika mpango huo na kuweka kaya zinazostahili.

Alisema Tasaf inataka kuona kaya hizo nazo zinapata maendeleo kwa kuondokana na umaskini. Alisema Tasaf ipo katika mchakato huo na imefikia asilimia 70 kwa Tanzania Bara na Visiwani, huku asilimia 30 ikifanyiwa maboresho. Alisema kaya zilizonufaika zitaondolewa katika mpango huo ili kuwezesha kaya nyingine maskini kujikwamua kiuchumi na kuondokana na umaskini. Naibu Waziri alisema mpango unaokuja utawezesha kaya maskini ziingie kwenye mpango huu wa kielektroniki na GPS badala ya ule wa zamani ambapo kaya hizo zilikuwa zikiandikwa kwenye daftari. Alisema hali hiyo ilisababisha kuwapo kwa malalamiko kuwa wasiostahili wameingizwa katika mpango huo wa kaya maskini kujikwamua kiuchumi. Katika hatua nyingine, amezipiga marufuku halmashauri zenye tabia ya kutumia fedha za kaya maskini kwa kuzielekeza kwenye miradi mingine.

Alisema kubadilisha matumizi ya fedha hizo kunawasababisha walengwa kushindwa kujikwamua kiuchumi kwa sababu fedha wanatengewa zinawafikia wakati ambao umeshapita.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Tasaf, Ladslaus Mwamanga, alisema Tasaf imefanya maandalizi ya kuwaondoa watu waliofanikiwa na kuingiza kaya maskini ili waweze kujikwamua kiuchumi na hivi sasa kuna wilaya ambazo wanafanyia majaribio ili kuondoa kaya zilizofanikiwa kiuchumi na kuingiza kaya maskini ili nazo ziweze kujikwamua.

Alisisitiza Tasaf inaanza kutambua kaya zilizobaki za asilimia 30 ili kuanza kuwaingiza kwa njia ya kielektroniki na GPS ili kubaini kama kuna upungufu wowote au la kwani awali walipofanya uandikishaji kwa njia ya daftari malalamiko kwa wananchi yalikuwa ni mengi.



Mwanzilishi wa kituo cha Light in Africa, Lynn Elliott (katikati), akipongezwa na viongozi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro juzi, kwa kuhudumia watoto yatima, wenye ulemavu na mahitaji maalum. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi walalamikia shirika kuwanyima tochi

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WAKAZI wa Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori Enduiment, (EWMA) wilayani Longido, wamelalamikia Shirika la Kijamii la Oikos kwa kushindwa kutekeleza makubaliano ya kuwapatia tochi maalum za kufukuza wanyamapori wakali.

Walisema shirika hilo limeshindwa kufanya hivyo licha ya kuchukua fedha kwa ajili hiyo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa jumuiya hiyo, Willium Kuyan, alisema hayo wakati akisoma taarifa fupi ya maendeleo kwenye kikao cha halmashauri kuu hapo jana.

Alidai Shirika la Oikos limeonekana kuwa na ujanja ujanja mwingi hasa katika mpango wa kuleta tochi walizokubaliana na ofisi hiyo kupitia fedha za wana jumuiya walizozichanga.

Alisema walikubaliana na Oikos kuleta tochi hizo kwa ajili ya kuwasaidia wafugaji na wakulima kipindi cha kilimo ili waweze kuwafukuza wanyama waharibifu na wale wakali wasiathiri mifugo wala mazao katika makazi ya jamii

Alieleza walikubaliana jamii ichangie nusu ya gharama na nyingine zitolewe na shirika hilo. Alisema watu zaidi ya 18 walichanga fedha kwa ajili ya kupata tochi hizo.

"Tulikubaliana 50-50, wananchi watoe nusu ya pesa na shirika nalo nusu, tulifanya hivyo kwa upande wa wananchi kati ya wananchi 18 kila mmoja alitoa Sh. 168,750, tukawakabidhi Oikos," alidai Kuyan.

Alisema jukumu hilo lilifanyika Septemba mwaka jana, lakini hadi sasa Oikos halijaleta tochi hizo na walipoulizwa walijibu wapo tayari kurejesha fedha za wananchi. "Tumefuatilia wanasema warudishe fedha za wananchi, nilikataa nikawaambia wanataka tujibu nini wananchi tutakapo wapelekea hizo fedha, tunachohitaji ni tochi," alidai Kuyan.

Hata hivyo, alisema wamekuwa wakisumbuliwa wananchi waliotoa fedha hizo, huku wakihisi jumuiya hiyo imekula fedha zao.

"Naomba Oikos watekeleze majukumu yao kama taratibu zinavyo waongoza," alisema. Kwa upande wake, ofisa anayeshughulikia migogoro na wanyamapori kutoka Oikos, Pascal Simon, alisema ni kweli walikusanya fedha hizo kwa wananchi 18 na zipo Oikos.

Alidai tochi hizo wameziagiza nchini China kuna taratibu za ulipaji wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (Vat) na usafiri, kwani shirika hilo ni miongoni wa NGO zinazolipa kodi hapa nchini. Akizungumza kwa njia ya simu na Nipashe alieleza walikusanya fedha hizo kwa jamii Novemba mwaka jana ila kutokana kuchelewa kiwandani tochi hizo zinatarajiwa kupatikana mwezi huu. Alikiri kukubaliana na jamii ambapo kila mhitaji wa tochi hizo alichangia nusu ya pesa huku shirika nalo likikubali kuchangia nusu.

Alisema tochi moja ina thamani ya Sh. 337,500.

# Mbaroni kwa wizi kichanga cha siku moja

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKULIMA na mkazi wa Kata ya Endakiso, Dori Joshua, (20) anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za kuiba mtoto mchanga wa siku moja aliyezaliwa Hospitali ya Mji wa Babati Mrara.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augustino Senga, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari jana.

Alisema mtoto huyo ni wa Hawa Singai, (39) aliyejifungua hospitalini hapo na kuruhusiwa.

Alisema wizi huo ulitokea Machi 31 saa 12 jioni katika mtaa wa Sinai uliopo Kata ya Maisaka.

Kamanda Senga alisema mama wa mtoto huyo, Hawa ni mkazi wa Sauna wilayani Kondoa, ambapo aliwaambia waandishi wa habari kuwa aliibiwa mtoto wake mara baada ya kuruhusiwa kutoka hospitali hapo.

"Alitoka nje ya geti akiwa na mtoto wake na mara akatokea dada ambaye kwa sasa ni mtuhumiwa na kumuomba amsaidie kumbeba mtoto kwa kisingizio cha kuwa yeye alikuwa anaelekea mjini Babati, hivyo walipanda usafiri wa bajaji, lakini baadaye alimwomba asimame ili akachukue fedha yake kwa mtu aliyemwachia maeneo hayo," alisema Senga.

Aidha, kamanda alisema mtuhumiwa huyo aliposhuka kwenye bajaji alishuka na mtoto huyo kwani mama wa mtoto alikuwa na mizigo mingine hivyo baada ya kushuka alitokomea kusikojulikana wakati akimwacha mama wa mtoto ndani ya bajaji.

"Hadi mama huyo aliposhtuka na kutahamaki mtuhumiwa alikuwa haonekani," alisema na kuongeza, "baada ya kupata taarifa polisi walifanya uchunguzi na mtuhumiwa huyo aliita usafiri wa pikipiki na kupelekwa kijijini kwao Endakiso, huku akiwa na kichanga hicho...tulimtafuta dereva pikipiki na baada ya kumpata alikiri kumbeba abiria huyo," alifafanua.

Senga alifafanua kuwa dereva bodaboda huyo aliwapeleka polisi mpaka alipomshusha abiria wake, askari polisi walifanya uchunguzi katika nyumba hiyo na majira ya saa 6:00 mchana mtoto alipatikana akiwa chumbani kwa mtuhumiwa huyo.

Alipofanyiwa mahojiano na polisi alikiri kuiba mtoto huyo kwa lengo la kumwonyesha mchumba wake ambaye siku nyingi amekuwa akimdanganya ana ujauzito ili ampatie fedha za matumizi na kiini cha tukio alisema ni kudanganya ili ajipatie kipato.

Kamanda aliitaka jamii hasa wanawake kutokumwamini kila mtu maana siyo kila mtu anayeomba kukusaidia anaweza kukusaidia kweli, wengine wanakuwa na nia ovu ambayo inalenga kutimiza maslahi yao.

Katika hatua nyingine polisi wanamshikilia muuguzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kiteto Mariam Juma, (49) kwa kosa la kupatikana na madini yanayodhaniwa kuwa ni ya moonstone kinyume cha sheria, ambapo tukio hilo limetokea Machi 27 majira ya saa 7:30 mchana huko maeneo ya Mafichoni kijiji cha Kibaya.

"Askari wakiwa doria walimkamata muuguzi wa Hospitali ya Kiteto akiwa na madini yadhaniwayo kuwa ya moonstone yapatayo 506 ambayo yalifanyiwa tathmini na kubainika yana thamani ya Sh. 55,760 na chanzo cha tukio hilo ni kujipatia kipato," alisema Senga.

Alitumia fursa hiyo kuwataka watu wote wanaohitaji kufanya biashara ya kuuza au kuchimba madini wafuate sheria ya madini ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza dhidi yao na kukwepa mkono wa sheria ili serikali iweze kupata mapato yake.







Mkurugenzi Mkuu wa Vodacom Tanzania, Hashim Hendi (wa pili kulia), akiwakabidhi Aron Heriel na Njopillay Millinga kutoka kampuni ya Fern Tanzania Ltd, tuzo ya Non Technology Over-all, wakati wa hafla ya kuwapongeza watoa huduma wa kampuni hiyo jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Usalama na Mazingira wa Vodacom, Karen Lwakatare. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Msekwa amteua Prof. Sife kuongoza MoCU

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Spika mstaafu wa Bunge la Tanzania, Pius Msekwa, amemteua Profesa Alfred Said Sife kukiongoza chuo hicho kwa muda ambao watakuwa wanamtafuta mkuu wa chuo mwingine atakayerithi mikoba ya Profesa Faustine Bee.

Msekwa alitangaza uteuzi huo jana, wakati akizungumza na wanataaluma na wanafunzi wa chuo hicho katika hafla fupi ya kumuaga Prof. Bee aliyeteuliwa kuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

"Inabidi niwaeleze wanachuo na wanataaluma kwamba kwa kuwa kiongozi wetu (Prof. Bee) ameondoka ni lazima tupate kiongozi mwingine, kwa sababu nafasi ya uongozi haiwezi kukaa wazi. Kuanzia leo hii (Aprili 2, 2019), nimemteua aliyekuwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (Taaluma), yeye ndiye aongoze chuo hiki kwa muda ambao tunamtafuta mkuu wa chuo mwingine atakayeshika mikoba ya Profesa Faustine Bee," alisema.

Kabla ya kutangaza uteuzi huo, Msekwa alisema ana uhakika kwamba mabega ya aliyekuwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Prof. Faustine Bee yanaweza kubeba mzigo aliotwishwa wa kukiongoza Chuo Kikuu cha Dodoma (Udom).

Katika ujumbe wake, Msekwa amemtakia kila lililo jema Prof. Bee huko anakokwenda, akisema wanajua kazi aliyopewa ni kazi kubwa zaidi, kwa sababu Chuo Kikuu cha Dodoma ni chuo kikubwa zaidi kuliko MoCU, kwa maana ya wingi wa watu wa wanafunzi na wafanyakazi.

"Kwa vile tunavyomfahamu tunahakika kwamba mabega yake yanaweza kubeba mzigo huo, kwa hiyo tumemuaga kwa heshima na ameahidi kwamba hatatusahau ila tukitaka kuchota busara zake, atakuwa tayari na sisi tumefurahi kupokea kauli yake hii," ameeleza Msekwa.

Akitoa nasaha zake katika halfa hiyo, Profesa Bee aliwaasa wanataaluma wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kuwa bado wana kazi kubwa ya kuwajengea uwezo wanataaluma wapya wanaoajiriwa, kwa sababu wanapoajiriwa wengi wao ni lazima wapate mafunzo katika tasnia ya ushirika na kwamba ni lazima waweke mkazo zaidi kwenye eneo hilo.

Ameeleza namna ya kuweka mkazo kwenye eneo hilo ni kufanya utafiti na angalao katika kila eneo la mfunzo kuwe na eneo la ushirika iwe ni ICT (teknolojia ya habari na mawasiliano) lazima azungumzie mambo ya ushirika, management (utawala), azungumzie mambo ya ushirika; na ukifanya hivyo watu wataanza kusoma literature (lugha) na wakisoma literature watajijengea uwezo na uelewa mpana zaidi katika tasnia hiyo.

"Hatuna budi kama chuo maana sisi sasa ni chuo pekee katika Afrika, tunafuatiwa na wenzetu Kenya, Kenya tayari wameanzisha Cooperative University of Kenya lakini hawatufikii kwa sababu wao wanazungumzia wanafunzi 1,000, sisi tuna wanafunzi 5,000. Lakini sisi tunaanza kutoa PhD (Shahada ya Udaktari wa Falsafa) ambayo ina maana lazima watu waanze kufanya research (utafiti zaidi) wao hawajafikia hiyo," alisisitiza Prof. Bee. Alisema wa Kenya wana shahada moja ya umahiri (masters degree), Tanzania ina shahada nne za umahiri na kwamba kwa hali hiyo tunakwenda mbele na hatuna budi kuongoza kwa mfano katika Afrika.

Profesa Bee, amekuwa mtumishi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kwa miaka 31 sasa na alifanya kazi ya kufundisha, kufanya utafiti lakini pia ameshiriki katika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya chuo hicho tangu kilipokuwa Chuo cha Ushirika Moshi, baadaye Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara Moshi na sasa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Anaondoka katika chuo hicho akiwa anakumbuka kwamba mwaka 2013, waliingia katika kushindanishwa Taasisi za Elimu ya Juu, chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ili kutafuta a Centre's of Excellence (kituo cha umahiri) na wao kuibuka kidedea na hatimaye mwaka huo huo tulitambuliwa kama kituo mahiri cha mafunzo ya ushirika na biashara ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

# Wenye ulemavu 154 wafichuliwa majumbani

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WATOTO 154 ambao walikuwa wamefichwa majumbani kutokana na kuwa na mahitaji maalum, wamegunduliwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, baada ya Idara ya Elimu Maalum kuendeshwa zoezi la ukaguzi maalum katika tarafa tano.

Akizungumza jana katika Shule ya Msingi Sanya Juu, wakati wa siku ya watu wenye usonji, Ofisa Elimu Maalum wa Wilaya hiyo, Rashid Rajab, alisema kwa mwaka huu idara hiyo iliendesha zoezi la ubainishaji wa watoto wenye mahitaji maalum kwenye tarafa zote za wilaya hiyo, ambapo watoto hao waligundulika kuwa na mahitaji maalum.

"Changamoto iliyopo ni kwamba wazazi na jamii nyingi wanaendelea kuwaficha watoto wenye mahitaji maalum. Watoto wenye mahitaji maalum ni pamoja na wenye usonji, hivi sasa tunayo shule moja ya wanafunzi wenye ulemavu ambayo ina wanafunzi 100," alisema.

Shule zinazohudumia watoto wenye mahitaji maalum ikiwamo usonji ni Naibili, Nuru, Sanya Juu na Faraja. Katika Shule ya Naibili tayari kuna watoto 17 wanaohudumiwa hapo na katika Shule ya Msingi Sanya Juu kuna watoto 24 na kitengo kipya katika Shule ya Nuru kuna watoto 22. Kwa mujibu wa Ofisa Elimu Maalum wa wilaya hiyo, Wilaya ya Siha inahudumia wanafunzi 146 wenye mahitaji maalum.

Akizungumza zaidi huduma hiyo katika maadhimisho ya Siku ya Usonji Duniani ambayo hufanyika kila Aprili 2, Ofisa Elimu ya Msingi wa Wilaya ya Siha, Rose Sandi, aliwaasa wazazi na jamii katika wilaya hiyo kutowabagua watoto katika suala la elimu.

Aliwataka wazazi na jamii kwa ujumla wake kuwapa elimu watoto wote katika familia bila ubaguzi wa jinsia, maumbile au uwezo wa watoto katika kuelewa na kuchanganua mambo mbalimbali.

Katika maadhimisho hayo, Mkurugenzi wa Shirika la Connects Autism Tanzania, GraceAnna Lyimo ambaye pia ni mwasisi wa KIWOCE Open School alisema usonji ni kitendo cha ubongo kuwa katika hali yenye upungufu fulani, ambapo dalili zake ni pamoja na kujitenga na jamii, kutopenda mabadiliko na kukosa uwezo wa kucheka na kutabasamu. Mpaka sasa usonji unaelezwa na wanasayansi duniani kwamba hawajagundua kisababishi sahihi.

# Kigogo UVCCM awashukia polisi

**Na Paul William,** ROMBO

NAIBU Katibu Mkuu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi Taifa (UVCCM), Dk. Galila Wabanhu, amewashukia askari polisi wa Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, akiwatuhumu kukamata waendesha pikipiki maarufu kama boda boda na kuwageuza mtaji.

Dk. Wabanhu amedai kuwa askari hao wanatengeneza pesa kupitia madereva hao wa bodaboda, huku wakijua kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Alitoa tuhuma hiyo jana, wakati akizungumza na wanachama wa CCM katika Wilaya za Rombo na Same ambako alifanya ziara ya maadhimisho ya jumuiya ya wazazi wa CCM.

"Wapo askari ambao wamekuwa wakijifanya kuzijua sheria zaidi kwa watu wanaoitwa waendesha bodaboda pekee yako na kujikusanyia mitaji kwa kuwakamata madereva hao, lakini askari hao hao wamekuwa wakizisindikiza pikipiki ambazo zinabeba dawa za kulevya aina ya mirungi kutoka nchi jirani na sasa imefika wakati hatupo tayari kuona viongozi wetu wanachafuliwa," alisema Dk. Wabanhu.

Wabanhu ambaye pia ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), kupitia Jumuiya ya Wazazi, ameweka wazi kuwa askari wanaodaiwa kufanya kazi hiyo ni wa Kituo cha Polisi Mengwe.

"Kwa asilimia kubwa askari wanaofanya hayo wanatoka katika Kituo cha Polisi cha Mengwe na wamekuwa wakiwanyanyasa wananchi, kiasi cha kuwafanya kuichukia serikali yao, huku wakitumia vibaya jina la kiongozi moja kwamba ndiye aliyewatuma kufanya hivyo," alisisitiza.

Naibu Katibu huyo alisema endapo vitendo hivyo havitakomeshwa kwa kuwawajibisha wale wote wanaofanya vitendo hivyo watapelekea Chama Cha Mapinduzi kutumia nguvu kubwa katika kuwashawishi wananchi ili kuiamini serikali yao inayowaongoza.

Mkuu wa Wilaya ya Rombo, Agness Hokororo, akizungumza katika mkutano huo alimwahidi Dk. Wabanhu kwamba atalianyia uchunguzi jambo hilo ili kulikomesha katika wilaya hiyo.

Hata hivyo, alipotafutwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Hamisi Issah, kuzungumzia tuhuma hizo aling'aka, huku akiwataka wananchi wanaowatambua askari hao kutoa taarifa polisi ili jeshi hilo liweze kuchukua hatua za kinidhamu kutokana na kuchafua jeshi hilo.

# ama



AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 17

**Sababu zinazochangia meno ya watoto kuoza, kutoboka**



Ukurasa 16

Mbinu mpya kukabili TB kupitia simu ya mkononi



Ukurasa 14

**Afungishwa ndoa, kisha ahamia 'leba' kujifungua**



## MJUE PROFESA KAISI

# Mwasisi wa MCH, mpambanaji wa tiba ya kinamama na uzazi

Ukurasa 19

## Afungishwa ndoa, kisha ahamia 'leba' kujifungua

**Indiana,** Marekani

MEYA wa Marekani na mgombea wa kiti cha urais ajaye, amewafungisha ndoa wapenzi waliokuja dakika za mwisho tu kabla ya kuelekea hospitali kupata mtoto kwa njia ya upasuaji

Pete Buttigieg, Meya wa Jjimbo la South Bend, Indiana, alisema wawili hao Mary and Gabe, walimkuta ndio amewasili ofisini saa 2.30 asubuhi na wakamuomba awafungishe ndoa kabla mtoto wao hajazaliwa.

Wafanyakazi wa Ofisi ya Meya, ndio wakawa mashahidi na walitumia vipande vya vitambaa( riboni) kama pete kwa kuwa hawakuwa na pete.

Baada ya kufunga ndoa, Mary alienda hospitalini saa 3.00 asubuhi kama alivyoagizwa na daktari na kujifungua salama mtoto mchanga wa kike.

"Mtoto Jade Katherine Jones amekuwa "mkazi mpya kabisa" wa South Bend," aliandiika Meya Buttigieg kwenye ukurasa wake wa Facebook.

"Ni nyakati kama hizi ambazo nitazikosa muda wangu wa umeya utakapokwisha ," aliandika alipotuma picha ya mtoto mchanga wa kike na akaongeza: "Hongera kwa wazazi na wanandoa wapya, na karibu Jade, katika dunia hii isiyoyadikika na nzuri!"

Mwezi Januari, Meya Buttigieg (37), alitangaza nia yake ya kugombea urais katika uchaguzi mkuu ujao wa Marekani mwakani, kupitia tiketi ya chama pinzani cha Democratic.

Iwapo atateuliwa, Buttigieg atakuwa mgombea wa kwanza aliyejitangaza wazi ni mpenzi wa jinsia moja kuwahi kuingia katika kinyang'anyiro hicho.



Meya Pete Buttigieg (katikati) akiwafungisha ndoa Mary na Gabe ofisini mwake. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# RC Shy: Mimba wanafunzi chanzo bodaboda, marufuku kuwapakia

• Nao wawanyooshea vidole wengine



Mkurugenzi wa Miradi kutoka shirika la Amref, Dk. Aisa Muya, akielezea namna ulivyo mradi wa afya ya uzazi kwa vijana na kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainabu Telack, akizungumza wakati wa kukabidhiwa mradi wa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana na kuzuia maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka Amref.

**Na Marco Maduhu,** Shinyanga

SHINYANGA ni miongoni mwa mikoa nchini, inayokabiliwa na tatizo kubwa la wanafunzi kukatishwa masomo, kwa sababu ya ujauzito na wengine kuolewa kwa ndoa za ututoni.

Kuna baadhi ya watu wamekuwa wakitupiwa lawama kila mara. Hapo kuna kundi la waendesha pikipiki za kukodisha, maarufu bodaboda, wakitajwa huwavizia na kuwapatia lifti pamoja na vitu vidogo, hatimaye kuingia nao kwenye uhusiano wa kimapenzi, ambao una kawaida ya kuishia kuwapa ujauzito na kuacha masomo.

Mambo yanayaotajwa kuchangia bodaboda kuwapata kwa urahisi wanafunzi, ni tatizo la umbali mrefu wa shule, ugumu wa maisha katika familia unaowakosesha mahitaji muhimu ya shule, watoto hao wanajikuta wakiingia kwenye vishawishi unaokomea kwenye ujauzito.

> **"Serikali inapokuwa inawakamata watuhumiwa ambao wamekuwa wakiwapatia ujauzito wanafunzi wakiwamo bodaboda.**

### MKAKATI WA MKOA

Moja ya mkakati ambao serikali mkoani Shinyanga imeuweka kwa ajili ya kukabiliana na vitendo vya bodaboda hao kuwatia mimba wanafunzi, ni kuwazuia kubeba wanafunzi kwenye pikipiki na atakayekamatwa anakiika maagizo hayo, atachukuliwa hatua za kisheria.

Zainabu Telack ni Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, anayetamka 'ameshachoka' kusikia kila mara badoboda wanalalamikiwa kuwatia mimba wanafunzi.

Katika agizo lake ni marufuku dhidi ya bodaboda hao kuwapakia wanafunzi wasichana, huku akitamka "atakayeonekana akamatwe."

"Tumechoka kusikia bodaboda wakiendelea kutia mimba wanafunzi na kuwakatisha masomo yao. Sasa dawa yao tunaanza kufanyia kazi nawapiga marufuku kubeba wanafunzi wa kike na wale ambao wanaegesha pikipiki zao jirani na shule waondolewe, ili tumuokoe mtoto wa kike kielimu," anasema Telack.

"Mkoa wetu wa Shinyanga kila mwaka umekuwa ukipanda nafasi za juu kitaluuma. Mwaka juzi, matokeo ya kidato cha nne tulikuwa wanane, lakini mwaka jana tumekuwa watatu, jambo ambalo ni la kujivunia. Tukimwacha mtoto huyo wa kike kumpigania taifa litakuwa la wajinga," ameongeza.

Telack anasema, mtu ukimwelimisha mtoto wa kike umejenga taifa bora, hivyo ni vyema wanafunzi hao wa kike wakalindwa kwa nguvu zote dhidi ya 'mafataki' ili vijana hao watimize malengo yao.

"Pia nawataka wanafunzi nao waachane na ngono wakiwa bado wadogo na kutopenda lifti kutoka kwa waaendesha bodaboda hao, bali watembee kwa miguu kwenda shule ili kujiepusha na vishawishi ambavyo vitakatisha ndoto zao," anasema.

### KUTOKA KWA WADAU

Mohamed Kahundi, ni Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, anatoa takwimu za mwaka jana za wanafunzi waliokatishwa masomo kwa sababu ya kupewa ujauzito, kwamba shule za msingi walikuwa tisa, sekondari 66 na kufanya jumla yao kuwa 75.

Stella Maganga ni mwanafunzi anayesoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Busangi, mkoani hapa, anayekiri kuwa bodaboda wamekuwa kikwazo kwa wanafunzi hasa wale wanaoishi umbali mrefu, pamoja familia zao kuwa na vipato duni, ambapo wamekuwa wakiwarubuni kuanza nao uhusiano wa kimapenzi.

"Mfano unakuta mwafunzi anatoka nyumbani kwao umbali mrefu na ukifika muda wa kurudi nyumbani, anaanza mawazo huku akiwa na njaa na hana pesa.

"Endapo akitokea bodaboda huyo na kuanza kumpatia usafiri na pesa ya kujikimu kula shuleni, lazima amkubali na kuanza kufanya naye mapenzi," anasema Maganga.

"Kinachopaswa kwa serikali licha ya kuzuia sisi kutobebwa na bodaboda hao, pia uweke mkazo wa kila shule ambazo zipo umbali mrefu zijengwe hosteli za wanafunzi wa kike, tuwe tunaishi hapo shuleni, ndipo itakuwa pona yetu. Tofauti na hapo, tutaendelea kupewa mimba tu, sababu ya mazingira kutokuwa rafiki kwetu," ameongeza.

### OFISA JAMII

Ofisa Maendeleo ya Jamii mkoani Shinyanga, Tedsoni Ngwale, anasema tatizo la wanafunzi kupewa ujauzito, limekuwa likionekana kwa jamii kuwa jambo la kawaida tu, kutokana na wazazi kuendekeza tabia ya mila na desturi zilizopitwa na wakati, kutopenda kumsomesha mtoto wa kike.

Anasema wanapowakamata watu, wakiwamo bodaboda wanaowapatia mimba wanafunzi, jamii pamoja na mabinti wana tabia ya kutokuwa tayari kutoa

AFYA

# RC Shy: Mimba wanafunzi chanzo bodaboda, marufuku kuwapakia



Bodaboda wa mjini Shinyanga, wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO.**

ushahidi mahakamani, hivyo watuhumiwa huachiliwa huru na kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo.

"Serikali inapokuwa inawakamata watuhumiwa ambao wamekuwa wakiwapatia ujauzito wanafunzi wakiwamo bodaboda.

"Jamii imekuwa haipo tayari kutoa ushahidi mahakamani pamoja na wahusika kuwakana watuhumiwa na kusababisha mimba shuleni kuendelea kuwapo," anasema Ngwale.

**MKURUGENZI**

Mkurugenzi wa Miradi kutoka shirika la Amref, wanaojihusisha na masuala ya afya, Dk. Aisa Muya, anasema baada ya shirika hilo kuona wasichana wengi wa Shinyanga wanakatishwa ndoto zao sababu ya ujauzito, imewalazimu kuanzisha mradi unaolenga kuwakomboa mabinti hao kielimu.

Anataja jina la mradi ni 'Dream Innovation Challenge Keeping Girls in School" unaotekelezwa katika shule 15 za sekondari katika Halmashauri ya Msalala, wilayani Kahama, una lengo la kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana na kuwakinga dhidi ya maabukizi ya virusi vya Ukimwi.

"Mradi wetu huu ulianza mwaka 2016 na unakoma rasmi Machi mwaka huu (mwezi uliopiata) na tunaukabidhi serikali. Tulikuwa tumejikita zaidi kutoa elimu kwa wanafunzi wa kike kujitambua, kuboresha huduma za afya, kutoa elimu kwa jamii kutambua umuhimu wa elimu na kusomesha watoto wa kike," anasema Muya.

"Wakati tulipokuwa tunataka kuutekeleza mradi wetu huu, tuliangalia katika mkoa wa Shinyanga, ni eneo gani sana wanafunzi wake wengi wanapewa ujauzito, ndipo tukaipata Halmashauri ya Msalala, ambayo ipo wilayani Kahama. Mwaka huo 2016 kulikuwapo mimba 79, (mwaka) 2017, zilikuwa 49 na kufanikiwa kupunguza hadi 38 mwaka jana," anaongeza.

Aidha, anasema wakati wanatekeleza mradi wao, baadhi ya changamoto walizokumbana nazo ni madereva wa bodaboda kuendelea kuwabebesha ujauzito wanafunzi.

Katoka hilo, Dk. Muya anasema, kuna baadhi ya wazazi kuwaozesha mabinti zao ndoa za utotoni na kuwahadaa wakidai wanachukua uhamisho wa mwanafunzi, kumbe wanaenda kuolewa.

**MWENYEKITI BODABODA**

Mwenyekiti wa Bodaboda wilayani Kahama, Idsam Mapande, anakiri kupokea agizo la Mkuu wa Mkoa, ingawaje anatumia kauli 'Kwa masikitiko' akidai wao siyo vyanzo vya mimba za wanafunzi peke yao.

Kiongozi huyo anaelekeza lawama pia kwa waendesha bajaji, wenye magari binafsi na , walimu, lakini anadau "mzigo wote wanaangushiwa bodaboda.' Ili kupata ukweli sahihi, anaomba kufanyike utafiti kuupata ukweli sahihi.

Mohamed Juma, ni Mwenyekiti Msaidizi wa waendesha bodaboda wa manispaa ya Shinyanga, anayesema suala la kuzuia bodaboda kubeba wanafunzi, siyo suluhu la wanafunzi kutopewa ujauzito, bali anashauri kutolewa elimu tu kwa bodaboda hao kuacha vitendo hivyo, sanjari na wanafunzi wenyewe kujitambua.

"Tunaomba uongozi wa mkoa, pale wanapokuwa kwenye vikao vyao vya elimu au afya, wawe wanatuhusisha na sisi ili tupate kuzungumza, siyo kila siku tunatupiwa lawama bodaboda.

"Ikiwa hatupigi mimba peke yetu, pia kuna magari ambayo yanatoa lifti kwa wanafunzi yakiwamo binafsi na suluhu ya haya yote ni elimu tu," anasema Juma.

"Agizo hili la mkuu wa mkoa tumelipokea kwa masikitiko sana. Wengine tuna mikataba na wazazi ya mwaka mzima kupeleka watoto wao shule. Sasa unapotuzuia unaweka wapi ajira zetu, naomba tu mheshimiwa aliangalie suala hili kwa mapana zaidi," anaeongeza.

Zainabu Juma, ni mzazi, anayeishi mkoani hapa, anaeleza kukubaliana na agizo hilo la Mkuu wa Mkoa, la kuzuia bodaboda kuwabeba wanafunzi wa kike.

Anasema, wao ndio wanaongoza kwa kuwapatia ujauzito wanafunzi na hata wafanyakazi wa majumbani, kutokana na kuwapatia usafiri wa bure na kuwahonga vipesa vidogo vidogo.

> "Mfano unakuta mwafunzi anatoka nyumbani kwao umbali mrefu na ukifika muda wa kurudi nyumbani, anaanza mawazo huku akiwa na njaa na hana pesa.




Mwanafunzi Annastazia Charles wa wilayani Kahama, akitoa ushuhuda namna elimu ya afya ya uzazi ilivyowasaidia kujitambua. **PICHA ZOTE: MARCO MADUHU**

AFYA

# Mbinu mpya kukabili TB kupitia simu ya mkononi



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, akizIndua kampeni ya wabunge mjini Dodoma, inayohusu kudhidibiti ugonjwa wa kifua kikuu, kwa kutia saini waraka maalum. **PICHA: MAKTABA.**

**Na Veronica Romwald**

KIFUA Kikuu (TB) imo katika magonjwa yanayotajwa na Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa ni hatari. Unatajwa kushika nafasi ya tisa kwa kusababisha vifo vingi duniani.

Takwimu za WHO za mwaka 2016 zinaonesha takriban watu milioni 10.4 duniani waliugua ugonjwa huo, watu milioni 1.7 walifariki dunia na watu milioni 4.3 hawakuweza kugundulika.


Yaani hao ni wale ambao walipata maambukizi ya ugonjwa huo lakini hawakuweza kubainika, waliendelea kuwapo katika jamii na kuendelea kuambukiza wengine.

TB ni ugonjwa unaoambukizwa kwa njia ya hewa na si kwa kugusana na mgonjwa wala kurogwa.

Ripoti ya WHO kuhusu ugonjwa wa TB ya mwaka 2017 inaeleza Tanzania ni miongoni mwa nchi 30 duniani zenye idadi kubwa ya wagonjwa wa TB.

Kulingana na Shirika hilo, inakadiriwa kila mwaka Tanzania inapaswa kuibua wagonjwa wapya wa TB 154,000.

> **Tunalenga pia kupambana na unyanyapaa kwa wagonjwa wa TB, ni suala linalotusumbua na ndiyo maana wengi wanaogopa kujitokeza kwenye matibabu.**




Hata hivyo, takwimu za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP) za mwaka 2017, zinaeleza jumla ya wagonjwa 69,818 wa TB waligundulika, asilimia 90 walitibiwa na kupona.

Ripoti hiyo ya NTLP ya mwaka 2017 inasisitiza wagonjwa hao waliofikiwa ni asilimia 44 pekee ikilinganishwa na idadi ya wagonjwa wapya wanaokadiriwa na WHO.

Hiyo inamaanisha kuna jumla ya wagonjwa wapya wa TB 84,000 ambao hawakufikiwa na bado wapo kwenye jamii wakiendelea kuambukizwa wengine.

Pamoja na hayo, ripoti hiyo inaeleza vifo vilivyotokana na ugonjwa huo mwaka 2017 vilikuwa 27,000 sawa na watu wapatao 70 kila siku.

### HATARI ILLIKO

"Hofu niliyonayo ni kwamba mgonjwa mmoja wa TB ambaye hajaibuliwa na kupatiwa matibabu mara moja, akiendelea kubakia kwenye jamii ana uwezekano wa kuambukiza watu wengine kati ya 10 hadi 20," anasema Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu.

Meneja Mpango wa NTLP, Dk. Beatrice Mutayoba, anasema kutokana na hali hiyo, ndiyo maana serikali kupitia Mpango huo wa NTLP, iliamua kubuni mbinu mpya itakayosaidia kuibua wagonjwa wapya wa TB yaani wale wasiojulikana.

### MBINU YENYEWE

Pengine nikuulize swali, Je! umewahi kufikiri kwamba ipo siku utaweza kujichunguza binafsi ugonjwa wa TB, kupitia simu yako ya mkononi?

Basi hilo linawezekana, kupitia mbinu hiyo iliyobuniwa na NTLP, kila mmoja sasa anaweza kujichunguza mwenyewe TB kwa kutumia simu yake ya mkononi, ni rahisi na huduma hiyo inatolewa pasipo malipo.

Dk. Mutayoba anasema huduma hiyo imepewa jina Tambua TB, inahusu jumbe fupi zinazotumwa kwa njia ya simu za mkononi zenye lengo la kuelimisha jamii kuhusu ugonjwa huu na kuhamasisha wagonjwa waliopo katika matibabu kuzingatia tiba.

Anasema wameona vema kutumia njia hiyo kwani ushindi dhidi ya magonjwa mbalimbali ikiwamo TB inahitajika ubunifu ikiwamo matumizi ya teknolojia.

"Teknolojia inatusaidia kuwafikia watu wengi kwa wakati na kwa gharama nafuu, hivyo ni matumaini yetu kwamba hatua hii itatusaidia kuwaibua wagonjwa ambao awali hatukuweza kuwapata," anasema.

Anaongeza: "Huduma hii ni matokeo ya jitihada za Mpango kushirikiana na kitengo cha elimu ya afya kwa umma na wadau mbalimbali katika kutokomeza TB ifikapo 2020.

### INAVYOTUMIKA

Dk. Mutayoba anasema huduma hiyo si tu kwamba itasaidia kuibua wagonjwa wapya wa TB kutoka asilimia 17 ya sasa hadi kufikia asilimia 84 ifikapo 2020 bali pia itasaidia kuibua wagonjwa wapya wenye maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

"Wale watakaogundulika wataanzishiwa dawa mara moja, lengo letu jingine ni kuongeza kasi ya uibuaji wa watoto wenye TB kutoka asilimia 10.6 ya sasa kufikia asilimia 15 ifikapo 2020," anasema.

Anafafanua: "Kuna malengo ya kidunia pia ya kutokomeza kifua kikuu ifikapo 2030, tunatakiwa tuwafikie angalau asilimia 90 ya wagonjwa wote wa tb na kuwaweka kwenye matibabu.

"Asilimia 90 ya pili tunatakiwa kuwafikia watu ambao ni makundi maalum yaani wale waliopo kwenye mazingira hatarishi kama wachimbaji wa madini, wagonjwa wa Ukimwi na wanaojidunga dawa za kulevya wafikiwe na kupewa matibabu.

"Asilimia 90 nyingine tunatakiwa kuhakikisha wagonjwa wote wa TB wanaogundulika wanatibiwa na kupona kabisa, lengo letu tunapenda kufikia asilimia 100," anasema.

Anasema Mpango mkakati wa NTLP unahimiza uhamasishaji na uhusiano kwa jamii, kwa ajili ya kufikisha elimu na huduma za TB, hivyo, kwa kutumia teknolojia hiyo ya mtandao kwa njia ya simu kwa ajili ya huduma ya TB, itasaidia kufikia lengo hilo.

"Kwa njia hii watu watapata ujumbe na tunaimani itatusaidia kukata ule mnyororo wa maambukizi katika jamii, kwa sababu asilimia kubwa ya Watanzania wana simu za mkononi, hii ni njia rahisi na nzuri ya kuwafikishia ujumbe, huduma hii inakwenda sambamba na miongozo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto," anasema.

Anaongeza: "Tunalenga pia kupambana na unyanyapaa kwa wagonjwa wa TB, ni suala linalotusumbua na ndiyo maana wengi wanaogopa kujitokeza kwenye matibabu.

"Wengi wanadhaniwa tayari wana maambukizi ya VVU jambo ambalo si kweli, teknolojia hii itasaidia kuwafikishia ujumbe sahihi wananchi," anasema.

### MWANZO WAKE

Mratibu wa Taifa wa Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma, Agatha Mshana, anasema walianza kwa kutengeneza wazo walilolifanyia kazi, kwa kushirikiana na asasi ya Path Tanzania na anafafanua: "Tukakutana na kutengeneza jumbe mbalimbali na kuwashirikisha wagonjwa wa TB, watoa huduma na wana jamii, wakazipitia na kutoa maoni yao kuziboresha."

"Baada ya hapo, jumbe hizo zikatengenezwa kwa ajili ya kuwekwa mtandaoni, tukafanya majaribio kwenye mfumo maalum," anasema.

Pia, anaeleza walikutana na watoa huduma katika ngazi za afya katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Kilimanjaro, Arusha, Geita na Mwanza na jumla ya walengwa 520 walipatiwa mafunzo na jinsi ya kuwasaidia wagonjwa kusajiliwa.

"Katika ngazi ya jamii, watoa huduma zaidi ya 200 wamepatiwa mafunzo. Wakati tunatengeneza jumbe, tuliainisha makundi saba, na kila moja limetengenezewa jumbe zake, jumla ya jumbe 800 zimetengenezwa," anasema.

Agatha anasema, mtu yeyote anaweza kutumia huduma hiyo kwa kujichunguza binafsi, akipiga katika baadhi ya simu za mkononi, wakifuata maelekezo waliopewa

> **Baada ya hapo, jumbe hizo zikatengenezwa kwa ajili ya kuwekwa mtandaoni, tukafanya majaribio kwenye mfumo maalum.**

### DK. NDUNGULILE

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, anasema hivi sasa wizara kupitia NTLP inatekeleza mpango mkakati wa miaka mitano, unaoisha mwaka ujao.

Anasema, lengo ni kupunguza maambukizi ya TB nchini kufikia asilimia 20 na idadi ya vifo vyake kwa asilimia 35.

"Mkakati huu unaendana na mkakati wa dunia wa kutokomeza TB wa mwaka 2016 - 2035 (Global END TB Strategy), unaolenga kuhakikisha huduma za TB zenye ubora wa hali ya juu, zinapatikana kwa wote ikizingatia usawa, jinsia na makundi hatarishi.

"Lengo namba 7.2 la Mpango Mkakati, huo linasisitiza haja ya kutumia mbinu za uraghibishi, mawasiliano na uhamasishaji jamii katika kukuza matumizi ya huduma za kudhibiti TB na maambukizi ya mseto wa TB na VVU," anabainisha.

Anasema, maendeleo ya kiteknolojia yameleta fursa mpya ya kutumia ubunifu kama mojawapo ya mbinu hizi ikijumuisha matumizi ya teknolojia ya mitandao ya simu kuongeza uelewa wa jamii kuhusu magonjwa mbalimbali ikiwamo huo wa TB, hasa namna gani ya kujikinga ili kuyaepuka.

# Sababu zinazochangia meno ya watoto kuoza, kutoboka

AFYA ya kinywa ni muhimu, hata kwa mtoto mchanga ambaye hana meno kinywani mwake.

Ingawa meno ya mtoto mchanga huanza kuonekana katika umri wa miezi sita, mzazi anashauriwa kuanza kusafisha kinywa chake siku chache baada ya kuzaliwa, kwa kufuta fizi zake kwa kitambaa kisafi.

Pia, inahimizwa matunzo yaendelee hadi meno ya mtoto mchanga yaanze kuonekana, kwani yanaweza kupata maambukizi endapo kinywa hakitatunzwa vyema.

Hatari ni kwamba, wakati yanaota yanaweza kuanza kutoboka, hivyo ni vizuri mtoto akazoeshwa usafi wa kinywa na meno

Kuanza kutunza meno ya mtoto tangu anapokuwa mchanga, huweza kumkinga na kutoboka kwa meno na magonjwa mengine ya kinywa kwa miaka mingi.

Ushauri mwingine ni pindi mtoto anapozaliwa, taya zake zikiwa zimeshabeba meno yote 20 ya utotoni, anapaswa kuanza kusafishwa kinywa chake, ukiwa ni mwendelezo wa usafishaji fizi kwa kitambaa baada ya kuzaliwa.

Meno ya mbele ya utotoni, huweza kujitokeza miezi sita baada ya mtoto kuzaliwa, ingawa kuna baadhi ya watoto huchelewa kuota meno mpaka miezi 12 au 14.



Mtoto akipiga mswaki wenye dawa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Inatakiwa mpaka mzazi ajiridhishe kuwa mwanawe anaweza kupiga mswaki mwenyewe ndio amuache, vinginevyo aendelee kumsaidia kupiga mswaki mara mbili kwa siku, kwa kutumia mswaki wa watoto na dawa ya meno yenye madini ya floraidi.

Mtoto wenye umri chini ya miaka mitatu, ama wazazi au walezi wanatakiwa waanze kumpigisha mswaki mara tu meno yanapoanza kutokeza kinywani.

Mswaki huo unatakiwa uwe mdogo na dawa ya meno yenye madini ya floraidi, yenye ukubwa wa punje ya mchele.

Upigaji huo wa mswaki unapaswa kufanyika kwa umakini, asubuhi baada ya kifungua kinywa na usiku kabla ya kulala.

Mzazi anatakiwa ahakikishe mtoto hamezi dawa ya meno inayotumika wakati wa kusafisha kinywa na meno, bali mtoto huyo aiteme yote na kusukutua kwa maji safi.

Kwa watoto wa umri wa kati ya miaka mitatu mpaka sita wakati wa kupiga mswaki, mzazi anatakiwa ahakikishe dawa ya meno inayotumika ina madini ya floraidi na ukubwa wa punje ya harage.

Kwa kawaida, meno ya utotoni yanapoanza kujitokeza miezi sita mpaka mwaka mmoja baada ya kuzaliwa, baadhi ya watoto huvimba na kuhisi maumivu kwenye fizi.

Inashauriwa, hali hiyo inapotokea, mzazi apitishe taratibu ama kidole au kitambaa kisafi, ili kutuliza hali hiyo.

Watoto wengi wafikapo umri wa miaka mitatu huwa na meno yote 20 ya utotoni.

**• Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za mtandao.**

AFYA

# Mabinti wanavyokombolewa kutoka utoro shuleni utokanao na hedhi

- Wanavikosa vipindi 84 kila mwaka
- Wapata uhuru kupitia mbadala mpya



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mundemu wilayani Bahi wakitengeneza pedi za asili. **PICHA: PAUL MABEJA**

**Na Paul Mabeja,** Dodoma

WASICHANA shuleni katika sehemu nyingi bado wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika kufikia masomo yao. Hapo panatajwa katika sura ya jumuisho la uhaba wa mabweni, umbali wa shule, pia vifaa na vyumba vya kujihifadhia wakati wanapokuwa katika hedhi.

Inaelezwa, hilo la hedhi ni tatizo linalochangia utoro mkubwa kwa mabinti shuleni na wataalamu wa afya na jamii, wanakadiria hedhi inachangia mwanafunzi wa kike wanakosa wastani wa siku 84 za masomo kwa mwaka.

Hiyo inaelelezwa ni sawa na vipindi 756 vyenye dakika 40 kila kimoja. Jumla ya dakika zinazopotea ni 30,240.

Wasichana wanakosa elimu wanayostahili, kwa sababu ya kukosa mazingira rafiki ya vyoo na usafi wakati wa hedhi shuleni au vyuoni.

**MAFUNZO WANAYOPEWA**

Kutokana na hali hiyo, shirika la Plan International kupitia mradi wake wa Usafi wa mazingira (UMATA), wanaendesha mafunzo juu ya hedhi salama kwa mabinti shule za msingi mkoani Dodoma.

Kupitia mradi huo, wanafunzi wanapatiwa mafunzo pamoja na taulo laini (Pedi) na vifaa kwa ajili ya kutengeneza Pedi za asili kwa ajili ya kujisitiri.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Mundemu, wilayani Bahi mkoa wa Dodoma, Zahiya Mbuva, anasema

> **"Zamani tulikuwa tunatoroka na kurudi nyumbani, lakini hivi sasa yupo mwalimu ambaye anatusaidia kila tunapokuwa katika hedhi.**

upatikanaji wa taulo laini na uwepo wa vyumba vya kuhifadhia wasichana katika shule zao, kumesaidia kuongeza mahudhurio ya wasichana shuleni.

Anasema mradi huo, umetoa mafunzo ya kuwasaidia wasichana, wanapokuwa katika hedhi, pia wanapatiwa vifaa vya kutengeneza pedi kwa watoto wa kike.

"Awali utoro kwa watoto wa kike ulikuwa mkubwa sana. Wanafunzi wa kike walikuwa wakitoroka vipindi kila wanapoingia katika hedhi, lakini toka kuanza kwa huu mradi, mambo yamebadilika. Wanafunzi wanajieleza kwa walimu wao na kupatiwa masaada,"anasema Mwalimu Zahiya

Anasema kuwapo chumba cha kujihifadhia wanafunzi wa kike, kilichojengwa maalum, kimekuwa msaada mkubwa kwao katika kuwahudumia.

"Hivi sasa, badala ya mtoto kukimbilia nyumbani, anachokifanya sasa ni kwenda katika chumba cha kujihifadhia ambacho kinakuwa na vifaa vyote kama pedi, maji na sabuni na baadaye kurudi darasani kuendelea na masomo kama kawaida,"anaeleza mwalimu.

**MWANAFUNZI ANENA**

Mwanafunzi wa darasa la saba, Paulina Majengo, anakiri kupatiwa mafunzo ya kujihudumia wakati wanapokuwa katika kipindi cha hedhi.

Anasema, pamoja na mafunzo hayo, pia wamejifunza namna ya kutengeneza pedi za asili wanazotumia na wanafunzi wenzake, tofauti na ilivyokuwa awali.

"Zamani tulikuwa tunatoroka na kurudi nyumbani, lakini hivi sasa yupo mwalimu ambaye anatusaidia kila tunapokuwa katika hedhi,"anasema Paulina.

Mwanafunzi Coretha Tarimo, anaiomba serikali kuwasaidia vifaa vya kujihifadhi wanapokuwa katika hedhi, pamoja na elimu iendelee kutolewa katika maeneo mbalimbali, ili jamii iweze kubadilika.

**MRATIBU USAFI**

Mratibu wa Mradi wa Usafi wa Mazingira wa shirika hilo, Rachel Stephen, anasema kupitia mradi huo wanatoa elimu juu ya hedhi salama kwa wanafunzi wa kike wa shule za msingi mkoani Dodoma.

Anasema, sababu kuu zilizochangia kuanza kutolewa mafunzo hayo, ni kutokana na watoto wa kike katika maeneo mbalimbali, kuendelea kupoteza vipindi kila wakati, wanapongia katika msimu wa hedhi.

"Sisi tunavunja ukimya kwa jamii kwa kutoa elimu, ili waweze kutambua kuwa suala la hedhi siyo kitu cha kificho tena, bali wasichana wanatakiwa kuwekewa mazingira mazuri, ili waweze kujisitiri wakati wanapokuwa katika hedhi,"anasema Rachel.

Anataja baadhi ya njia wanazotumia ni pamoja na kuwanunulia vifaa kama vile pedi na kuvigawa katika shule mbalimbali zilizopo katika mradi huo.

Aidha, Rachel anasema, kwa upande wa walimu wamewawezesha kwa mafunzo mbalimbali kuelewa undani wa hedhi, ili wawasaidie watoto kujihifadhi kila wanapokuwa katika hali hiyo, wakitumia vifaa vilivyoko katika maeneo yao.

"Wanaweza kutumia hata vipande vya kanga ambavyo vinapatikana katika maeneo yao na kuviboresha, ili kuweza kutengeneza pedi watakazotumia, ili kuweza kujistili na kuendelea na masomo badala ya kutoroka na kurudi nyumbani,"anasema.

Anasema vifaa hivyo vya asili vinavyotengenezwa

vina uwezo wa kukaa hata kwa saa tatu, hivyo mwanafunzi ana uwezo kushiriki vipindi, pasipo shaka. Kwa mujibu wa Rachel, ni mradi unaoleta mabadiliko katika jamii, kwa kuzipatia elimu ya hedhi kwa wasichana na watu wamekuwa wakibadili mitazamo yao, tofauti na awali.

"Watoto hawa tunaowafundisha shule, wanakwenda kuambukiza hata dada zao kule nyumbani pamoja na jamii kwa ujumla, kwani hivi sasa wanaelewa kuwa hedhi siyo suala la siri tena, hata kinababa hivi sasa wanashiriki katika kuwawezesha watoto, kupata vifaa vya kujihifadhi," anasema.

**CHANGAMOTO**

Anasema, pamoja na mafanikio hayo, lakini bado zipo changamoto mbalimbali, ikiwemo mila zilizopo katika jamii ambao wanawake wengi wanafundishwa kuwa suala la hedhi ni la siri sana.

"Hivyo, walimu wenyewe kama wanaona kuwa hedhi ni suala la siri sana. Hata ukienda kuwafundisha juu ya kuwasaidia watoto wanapokuwa katika hedhi inakuwa ni vigumu kukuelewa" anasema.

Anataja changamoto nyingine, ni upatikanaji wa vifaa hasa katika maeneo vijijini, shule nyingi hazina vyumba vya kujihifadhia kwajili ya watoto wa kike wanaoingia katika hedhi zao kila mwezi.

Rachel anaongeza kuwa, changamoto nyingine ni upatikanaji maji katika shule pamoja na sababu imekuwa kikwazo kwa wasichana, wakati wanapokuwa katika hedhi zao, hivyo wengi wao hutoroka masomo kwenda nyumbani kwa ajili ya kujihifadhi.

**WAZAZI WA KIUME**

Mratibu huyo anatoa wito kwa kinamama, kutoliona suala la hedhi kama kitu cha aibu, bali wawafundishe mabinti wao, namna sahihi ya kujihifadhi na kuwawezesha kupata vifaa vya kujihifadhia.

Juma Mazengo (65 ) ni mkazi wa kijiji cha Mchito wilayani Bahi, mkoa wa Dodoma, anasema wazazi wa kiume wanatakiwa kushirikiana na wake zao kuwasaidia watoto wakati wanapokuwa katika hedhi, ili washiriki vyema masomo yao.

AFYA

MJUE PROFESA KAISI

# Mwasisi wa MCH, mpambanaji wa tiba ya kinamama na uzazi

Na Beatrice Moses

- Alileta ‘Ultra Sound’ ya kwanza nchini
- Alibuni wakunga Newala, vitabu vyao
- Mwezeshaji likizo ya uzazi kwa wote

WATU wenye afya bora ni mtaji kitaifa. Ni msingi wa kisera, kwa sababu serikali kupitia wataalamu na wadau wa afya, inaunganisha nguvu kuhakikisha magonjwa, ajali na mengine mabaya kiafya yanadhibitiwa. Lengo ni kuhakikisha usalama wa wananchi.

Mara baada ya uhuru wa nchi mwaka 1961 hadi mwaka 1990, wizara inayohusika na afya, ilitekeleza huduma za afya nchini, bila ya kuwapo sera rasmi ya taifa ya afya.

Wakati huo mwongozo wa nchi ulikuwa kupambana na maradhi, ujinga na umaskini. Hivyo, mipango yote ya sekta ya afya ililenga kupunguza maradhi na vifo kwa kutumia rasilimali zilizopatikana.

Inaelezwa na wadau wa sekta ya afya, kwamba sera rasmi ya afya iliitayarishwa na kupitishwa mwaka 1990. Katika mtazamo wa jumla uliopo, wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano, wanapewa kipaumbele kutokana na sababu mbalimbali za upekee, wa usalama wao kiafya.

**SAFARI YA MCH**

Hapo ndiko kwenye kliniki ya kinamama na watoto (MCH), ambayo imeenea kila mahali nchini.

Ni vigumu kutaja au kuzungumzia mfanikio hayo yote, pasipo kuhuasisha jina muhimu na maarufu la Profesa Malise Kaisi, mtaalamu bingwa wa uzazi na magonjwa ya wanawake, aliyeacha alama za nyayo zake katika eneo la tiba ya hospitalini, katika maeneo tofauti tangu zama za miaka 1960.

Pia, mtaalamu huyo amekuwa katika iliyokuwa Shirika la Afya Muhimbili (sasa Hospitali ya Taifa Muhimbili) na Chuo Kikuu cha Afya na Tiba (MUHAS), alikoshika chaki na kugawa ujuzi wake.

Katika eneo hilo, Profesa Kaisi, ameshughulikia kwa kina afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, akikumbukwa kwa mchango wake katika uanzishwaji mafunzo ya ukunga na huduma ya mama na mtoto vijijini, hivyo ikachochea uwepo wa kliniki za mama na mtoto.

**AKUMBUKIA MTWARA**

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni jijini, Profesa Kaisi, anarejea kipindi alichokuwa Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mtwara mwanzoni mwa miaka ya 1970, kulikuwapo vifo vingi vya kinamama, kutokana na huduma duni za afya.

Profesa Kaisi anasema, kulikuwapo maeneo yenye vita kama wilayani Newala, kulitengwa vijiji vya ulinzi, ambako kulikuwa mbali na mjini, hivyo vilikuwa katika hali ngumu katika huduma za afya.

“Niliamua kujenga uhusiano wa mawasiliano ya karibu na wanajeshi, ili kwamba wakiona dharua wawasiliane nami kwa ‘radio call’ na huku wakisaidia jinsi ya kuwaleta wagonjwa mjini,” anaeleza Profesa Kaisi.



Profesa Malise Kaisi. **PICHA: BEATRICE MOSES**

> **Yule daktari alikwenda kumfuata kuomba ushauri, akamwambia mbona Daktari Kaisi ameshaandika?**

“Hali hiyo ilinifanya nijiulize mambo mengi, ikiwamo kutafuta namna nzuri ya kuwasaidia wajawazito na watoto. Niliandika barua ya kuomba ruhusa ya kuandaa mafunzo ya kupata wasaidizi wa huduma za afya hasa uzazi,” anasema.

Mtaalamu huyo anasema alijibiwa na wizara kupitia Muuguzi Mkuu, ambaye wakati huo alikuwa raia wa Afrika Kusini, aliyemkataza kuanzisha mafunzo hayo, yakiwa na ujumbe wa kumpiga marufuku.

Profesa Kaisi, anasimulia kwamba majibu hayo hayakumkatisha tamaa, akatumia mtazamo mbadala wa kuwasilisha wazo lake kwenye mkutano wa Kamati ya Utendaji ya Mkoa.

“Niliwaeleza hali halisi kwamba siyo nzuri na naamini mafunzo hayo ninayokusudia kuyatoa, yatasaidia kupunguza idadi ya vifo, kwa kuwa tutaboresha huduma ya awali ya afya ya mjamzito na watoto wanaozaliwa.

“Nilijua kiongozi yule amekataa kwa kuwa hajui kinachoendelea vijijini, maana anaishi Dar es Salaam, nikawaomba wanitengee fedha za mafunzo hayo,’ anaeleza.

**ABUNI MAFUNZO, KITABU**

Anasema, kamati ya mkoa ilikubali ombi lake na kumpatia fedha na anasema hakukumbuki kiasi chake, akaandaa mikataba maalum kabla kwa wanafunzi, pindi hajaanza kuwafundisha.

”Nikajipanga vyema kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo, ikiwamo kuwasainisha mikataba kuwa watakaohitimu, hawatekwenda kufanya kazi hospitali, isipokuwa watakwenda vijijini kusaidia kuwahudumia wajawazito na watoto wanaozaliwa vijijini,”anasema.

Anasema wakati huo mikoa ya Mtwara na Lindi ulikuwa mmoja, hivyo alichagua wasichana watano kutoka Masasi, Mtwara, Newala, Lindi, Kilwa, Nachingwea ambazo ndizo zilikuwa wilaya za mkoa huo.

Miongoni mwa mambo aliyowafundisha, ni kutambua afya ya mama na mtoto; mfumo wa utoaji huduma maalum kwa wanawake walio katika umri wa uzazi na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

Anaeleza mafunzo aliyowapa, aliwafundisha kutambua vidokezo hatari kwa wanawake na watoto, chanjo, kutoa elimu ya uzazi salama, mbinu shirikishi za udhibiti wa magonjwa ya watoto na lishe bora.

Profesa Kaisi anasema, mafunzo hayo aliyaendesha na alifuatilia utekelezaji wake kwa hatua, yaliyoonyesha matokeo mazuri kama alivyokusudia.

Anasema, ni mafanikio yaliyomfanya aandike kitabu cha ukunga kitwacho ‘Utunzaji wa Watoto Vijijini’ ambacho kwa namna ya kipekee, kilipokewa na kutumika zaidi nchini Kenya.

Bingwa huyo anasema, kupitia matazamo huo, aliamua kuwashirikisha madaktari wa mikoa mingine kwa kuwaandikia barua, lakini katika mtazamo wa kushangaza, anasema hakuna aliyejibu.

Profesa Kaisi, pia aliandika Wizara ya Afya kwa mara nyingine, akiiomba serikali iruhusu kufanyika mafunzo hayo kwa mikoa yote nchini, wakati huo zilikuwa nane.

Anabainisha kuwa wazo hilo lilifika kwa kiongozi husika wizarani, ambaye licha kulikubali, hakupenda lionekane limetoka kwa Mtanzania, akamtafuta daktari Mwingereza, aliyefanya kazi mkoani Tanga, akamtaka aandikie barua ya mafunzo kama hayo ya Profesa Kaisi.

“Barua niliyoipeleka wizarani nilimpa pia na mwalimu aliyeni-

INAENDELEA UK.20

AFYA

# Mwasisi wa MCH, mpambanaji wa tiba ya kinamama na uzazi



Mkunga katika Hospitali ya Rufani ya Temeke, jijini Dar es Salaam, akimuelimisha mama aliyejifungua mtoto kabla ya wakati (njiti), jinsi ya kumhudumia. Huduma za aina hizo,ndizo sehemu za ndoto za Profesa Kaisi tangu zama za utumishi wake. **PICHA: BEATRICE MOSES.**

**INATOKA UK.19**

fundisha udaktari (Chuo Kikuu) Makerere nchini Uganda," anasimulia Profesa Kaisi na kuongeza: "Yule daktari alikwenda kumfuata kuomba ushauri, akamwambia mbona Daktari Kaisi ameshaandika? Akamwonyesha andiko langu, naye akanitafuta,"

Anasema licha ya kukutana na kukubaliana na yule daktari kwamba washirikiane kufanikisha jambo hilo, alilazimika kumfuata yule kiongozi wizarani. Huku akikerwa kile anachokiita 'dharau kwake' anadokeza mazungumzo yao:

"Nilimfuata na kumwambia kuhusu jambo alilolifanya kupindua wazo langu lionekane kuwa limetoka kwa mzungu. Alikuwa na kiburi, nikaondoka zangu."

Anasema kuwa hata hivyo wazo lake hilo lilifika katika Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) na Shirika la Afya Duniani (WHO), mradi huo ukawa mkubwa, licha ya kwamba chuki nazo ziliongezeka .

"Nilianza kupata safari mfululizo wiki mbili Dar es Salaam, wiki mbili Geneva. Nilifanyiwa fujo kubwa, lakini mwisho wa yote nashukuru Mungu kwamba nilifanikiwa huduma za vituo vya afya ya mama na mtoto," anasema.

Anaeleza kuwa alichaguliwa kuwa msimamizi vituo vya mafunzo ya afya ya mama na mtoto vilivyoanzishwa na akawa anaenda kufuatilia hadi ujenzi wake, katika maeneo ya Kahama na Mwadui mkoa wa Shinyanga, Morogoro na Tukuyu, mkoani Mbeya.

> "Nikifikiria jambo kubwa nililofanya katika udaktari wangu ni hilo kwenda kuhakikisha kuwa kinamama waliopo vijijini wanapata huduma za afya kupitia MCH.

Profesa Kaisi anasema, baada ya kukamilika vituo hivyo, kitabu kilichotumika awali katika mafunzo hayo ni tungo yake ya 'Ukunga na Utunzaji wa Watoto Vijijini.

"Nikifikiria jambo kubwa nililofanya katika udaktari wangu ni hilo kwenda kuhakikisha kuwa kinamama waliopo vijijini wanapata huduma za afya kupitia MCH," anasema.

Anasema, baada ya kujifunza kutoka nchi zilizoendelea aliona umuhimu wa kuelimisha jamii kuhusu matunzo mazuri ya watoto wanaozaliwa kabla ya wakati na kuondoa fikra potofu dhidi yao, pia wazazi.

"Niliandika kitabu 'Mtoto Asiye Riziki' kilikuwa na kurasa 24. Niliandika kuonyesha kuwa kuna njia ya kuwaokoa wale watoto, ili waendelee kuishi. Hiyo ilikuwa mwaka 1975, kilitumika kufundishia kwenye elimu ya watu wazima, walikuwa wanasoma kama hadithi hivi," anasema.

Profesa anasema, pia aliandika kitabu kiitwacho 'Magonjwa ya Wanawake' ikiwa na ufafanuzi kuhusu mengi kama magonjwa ya fistula, kansa na kilikuwa na kurasa 80.

"Humo niliandika mengi, ikiwamo ukomo wa hedhi kwa mwanamke, hatua ambayo inaogopwa na wanawake kadha. Kitabu kilipendwa na kilielimisha watu wengi, ambao walikuwa wanadanganywa kuhusu magonjwa ya wanawake ikiwamo usafishaji wa kizazi," anasema.

Mbali na hiyo, Profesa Kaisi, anasema hata matumizi ya vipimo vya Ultra Sound, ndiye alikuwa wa kwanza kuzileta nchini mwaka 1977, alipokuwa akifundisha katika Kitivo cha Tiba cha Chuo Kikuu cha Dar e Salaam.

Kwa mujibu wa Profesa Kaisi, kifaa hicho alipatiwa zawadi kutoka nchini Uholanzi, alikokuwa masomoni kwa miezi mitano na ndicho kikawa kinatumika hospitalini Muhimbili.

Pia, anasema, hata kipimo cha uchungu wa uzazi nacho ndicho cha kwanza alichopewa ughaibuni alikoenda mafunzoni na kurejea, lakini kiliharibika mapema, kutokana na hali ya hewa joto na mazingira duni ya kuhifadhi.

### LIKIZO YA UZAZI

Anaeleza kuwa mwaka 1971 alijikuta analazimika anaukosoa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), kutokana na hatua yao ya kushawishi wanawake walioolewa pekee, ndiyo wapewe likizo ya uzazi kama 'zawadi.'

Profesa Kaisi anasema, aliiona hatua hiyo kuwa ni ya kibaguzi, kwa kuwa watoto wote wana haki sawa ya kulelewa, hivyo likizo kuwa zawadi kwa walioolewa ingesababisha watoto waliozaliwa na wanawake wasioolewa, kunyimwa haki ya kulelewa vyema.

"Niliamua kuandika barua ya wazi kwenye gazeti la Tanzania Standard, hoja zangu ziliwavutia wengi ikiwamo Mhariri. Niliitwa na kupewa tuzo ya shilingi 20,"anasema.

Anaeleza kuwa uongozi wa gazeti hilo ulikwa na kawaida ya kutoa zawadi kila wiki kwa mwandikaji wa barua yenye hoja iliyo na manufaa kwa jamii.

"Niliipinga, kwa sababu likizo ni haki ya mtoto kutuzwa siyo kwa mama pekee. Ukishaweka ubaguzi wa namna hiyo, unamwadhibu mtoto, kwa sababu mama yake hajaolewa," anasema.

Baada ya barua hiyo, ulitangazwa uamuzi na serikali ulioagiza kwamba, likizo ya uzazi inakuwa kwa wanawake wote, bila ya kujali kama ameolewa au la.

Ni msimamo wa kiserikali unaoendelezwa hadi sasa, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, katika hotuba ya bajeti ya wizara hiyo ya mwaka 2017/2018 aliyoiwasilisha bungeni, alibainisha upatikanaji wa huduma inayofikiwa na wanawake wote.

Waziri alieleza kuwa huduma hiyo inapaswa kuwafikia kabla ya ujauzito, wakati wa ujauzito na wakati wa kujifungua hadi wiki sita baada ya kujifungua, kwa kuwa ni mhimili muhimu wa kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

"Hata hivyo, tatizo la vifo vitokanavyo na uzazi bado ni changamoto, tafiti zilizofanyika nchini mwaka 2015 zinaonyesha kwamba, vifo vitokanavyo na uzazi havijapungua. Takwimu zinaonesha idadi ya vifo ni 556 kwa kila vizazi hai 100, 000," anasema.

Alieleza kuwa, katika kuimarisha huduma za Afya ya Uzazi na Mtoto nchini, wizara imeandaa mpango mkakati unaotekelezwa kuanzia mwaka 2016 hadi 2020.

Waziri Mwalimu, anasema mpango huo unalenga kuboresha afya ya uzazi, watoto na vijana pamoja na kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi kufikia 292 kwa kila vizazi hai 100,000 ifikapo mwaka 2020.

"Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imezingatia maeneo makuu matatu, ambayo ni huduma ya uzazi wa mpango, huduma wakati wa ujauzito na huduma wakati wa kujifungua," anasema.

• ***Usikose sehemu ya pili Alhamisi ijayo, ikianisha undani wa utaalamu wake, hasa kwa afya ya kinamama.***





# Waipongeza serikali kwa kutimiza wajibu wake

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wameishukuru serikali kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ya maji katika wilaya hiyo kwa madai kuwa utekelezaji huo unasaidia kuwaondolea wananchi changamoto.

Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya hiyo, Noel Chiwanga, alisema maeneo mengi ya wilaya hiyo yalikuwa yanakabiliwa na changamoto nyingi za maisha miaka ya nyuma, lakini kwa sasa serikali imeonyesha nia ya kuzitatua.

Alisema katika Mji Mdogo wa Makongolosi wananchi walikuwa wanakabiliwa na changamoto ya maji, lakini kwa sasa serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kuchimba kisima kirefu cha maji kwa ajili ya wakazi wa mji huo.

Alisema mbali na mradi huo pia kuna mradi wa Bwawa la Matwiga ambalo linakusudiwa kuwanufaisha wananchi zaidi ya 50,000 wa vijiji 16 ambalo lilikuwa linasuasua lakini sasa hivi serikali imeshatoa maelekezo maalumu ya kukamilisha.

"Tunaishukuru serikali kwa utekelezaji wa ilani yetu katika maeneo mbalimbali ndani ya wilaya hii, tulikuwa tunakabiliwa na changamoto nyingi sana, wananchi walikuwa wameanza kupoteza matumaini ya kupata maji kwenye Bwawa la Matwiga, lakini Waziri Mbalawa ameyafufua," alisema Chiwanga.

Vilevile aliishukuru serikali kwa kuendelea kusogeza huduma za afya kwa wananchi kwa kujenga vituo vya afya na zahanati kikiwamo Kituo cha Afya cha Chalangwa ambacho ni bora.

Kwa upande wake Katibu Mwenezi wa CCM wa wilaya hiyo, Antigon Kawishe, alisema kwa sasa chama hicho kinaendelea na zoezi la kupeperusha bendera za chama kwenye makazi ya viongozi ili wananchi wakitambue vizuri chama hicho.

Alisema wakati wa zoezi hilo pia wanawahamasisha wananchi kuiamini serikali yao kwa kuwafafanulia mambo mbalimbali ambayo yanatekelezwa kwenye maeneo hayo.

Aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali wa chama na serikali kuwafafanulia mambo mbalimbali yanayofanywa na serikali yao ikiwamo mambo anayoyafanya Rais Dk. John Magufuli.

# Wakulima hupoteza asilimia 30 ya mazao yao kila mwaka

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

WAKULIMA wilayani Mbozi wanapoteza zaidi ya asilimia 30 ya mazao wanayostahili kuvuna kila mwaka kutokana na udongo wa mashamba yao kuwa na tindikali nyingi.

Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo (Tari) Uyole cha mkoani Mbeya, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema utafiti ambao wameufanya kwenye mashamba ya wakulima wilayani Mbozi unaonyesha ardhi hiyo kuwa na tindikali nyingi ambayo ni kati ya 4.2 na 5.7 katika kipimo cha PH.

Dk. Bucheyeki alisema kuwa kiwango hicho cha tindikali kwenye ardhi ni kikubwa ambacho hakiruhusu mimea ya mazao kufyonza vizuri virutubisho kutoka kwenye udongo hata kama wakulima watatumia ipasavyo mbolea na kufuata kanuni zote za kilimo bora.

"Kwa muda mrefu wakulima wamekuwa wakipata mazao duni sana na imefikia hatua kwamba sasa hivi mkulima anapata chini ya tano moja ya mahindi kwenye hekta moja, sababu ni nyingi mojawapo ni upungufu wa rutuba kwenye udongo, lakini sasa hivi tena tumegundua kwamba kuna tatizo la udongo umekuwa mchachu, yaani asidi imeongezeka kwenye udongo," alisema Dk. Bucheyeki. Alisema baada ya kubaini tatizo hilo walianza mradi wa kutibu udongo huo kwa kutumia chokaa ambayo kitaalamu inasaidia kupunguza ama kuondoa kabisa tindikali kwenye udongo.

Alisema mradi huo umeonyesha mafanikio makubwa baada ya kuweka chokaa kwenye mashamba kadhaa ya wakulima na kuhamasisha matumizi sahihi ya mbolea.

Mmoja wa watafiti, Johnson Mtama, alisema kuwa wameanza kutoa elimu kwa wakulima namna ya kudhibiti tindikali kwenye mashamba yao kwa kutumia mashamba darasa ambayo yanawapa wakulima maarifa hayo kwa vitendo.

Alisema katika utoaji wa elimu hiyo, wanalima mashamba mawili katika eneo moja, ambapo shamba moja wanaliwekea chokaa na lingine haliwekewi chokaa na kisha mashamba yote yanahudumiwa kwa kuwekewa mbolea ipasavyo na mahitaji mengine kwa usawa. Alisema katika mashamba ambayo yaliwekewa chokaa, mazao yameonekana kuwa mazuri na bora zaidi kuliko yale ambayo hayakuwekewa chokaa na wakulima kwa kuliona hilo wameanza kuhamasika kuweka chokaa kwenye mashamba yao ili kudhibiti tindikali.

Mtama alisema kuwa katika shamba lenye ukubwa wa ekari moja mkulima anatakiwa kuweka mifuko 12 ya chokaa na akisha weka mara moja hatakiwi kuweka tena kwa kipindi cha miaka minne na baada ya hapo anapaswa kuwaita wataalamu kwa ajili ya kupima kiwango cha tindikali kwenye udongo wa shamba lake kwa ajili ya kumpa maelekezo mengine.

Baadhi ya wakulima wilayani Mbozi, wamekiri kupungua kwa mavuno hasa ya mahindi kwenye mashamba yao licha ya kutumia mbolea na kufuata kanuni zote za kilimo bora, lakini hawakujua sababu za kupungua kwa mavuno.

Jonas Mwashambwa ambaye ni mkulima wa mahindi katika kijiji cha Iwalanje, Kata ya Magamba wilayani Mbozi, alisema kuwa elimu ya kudhibiti tindikali ambayo wameanza kupewa na watafiti wa kilimo imeanza kuwapatia manufaa kutokana na mazao yao mwaka huu kustawi vizuri na kuonyesha kila dalili ya mavuno kuongezeka mara dufu katika msimu huu wa kilimo.

"Elimu hii sisi tunaona ina manufaa makubwa sana kwetu, kwa kuwa baada ya kujifunza kwenye shamba darasa tunaihamishia kwenye mashamba yetu na kwa kweli msimu huu tunaona mazao yetu yana mabadiliko makubwa na tunaweza kupata mazao mengi ikilinganishwa na miaka mingine," alisema Mwashabwa.



Wafanyakazi wa Benki ya DTB Tanzania, wazazi wa watoto wenye usonji na wakazi wa jiji, wakiungana katika matembezi ya hisani ya kilomita 4 ya kuadhimisha Siku ya Usonji Duniani yaliyoandaliwa na Kituo cha Autism Therapy and Behaviors Learning, jijini Dar es Salaam jana, yakiwa na lengo la kuelimisha jamii kuhusu mafunzo na malezi ya watoto wenye usonji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wananchi washauriwa ufugaji nyuki kuongeza kipato

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wameshauriwa kutumia fursa ya uwepo wa misitu kufuga nyuki ili kujiingizia kipato kitakachowafanya wajikwamue kiuchumi pamoja na kulinda mazingira yasiharibiwe. Ushauri huo ulitolewa jana na Meneja Msaidizi wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Innocent Lupembe, alipokuwa anazungumza na Nipashe kwenye ofisi za taasisi hiyo zilizopo Airport jijini Mbeya.

Alisema kwa sasa mazao ya nyuki hasa asali yana soko kubwa duniani kutokana na kuwa na matumizi mengi, hivyo akawataka wananchi wanaoishi kwenye maeneo yaliyo jirani na misitu kuchangamkia fursa hiyo.

Lupembe alisema ofisi yake mbali na kufanya kazi ya kulinda misitu, pia inawaelimisha wananchi njia mbalimbali za kuhifadhi na kunufaika na misitu hiyo.

Aliwataka wananchi wanaotaka kujifunza zaidi kutembelea ofisi za taasisi hiyo pamoja na maofisa maliasili wa halmashauri zao ili kujifunza namna ya kunufaika na soko la asali duniani pamoja na kulitumia zao hilo kama chakula.

"Sisi tunatoa elimu kwa wananchi ili wazijue faida za uwepo wa misitu kwenye maeneo yao, kwa sasa tunawahimiza zaidi kutumia misitu hiyo kufuga nyuki ili wazalishe asali na kuiuza ili wajiongezee kipato, lakini pia asali ni chakula," alisema Lupembe.

Hata hivyo aliainisha baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Mbeya ambayo yana misitu inayofaa kwa ufugaji wa nyuki kuwa ni pamoja na iliyopo Chunya na Mbarali.

Aliwataka kuacha kuitumia misitu kwa ajili ya kupata kuni na mkaa pekee kazi ambazo zinachangia uharibifu wa mazingira na kupelekea mabadiliko ya tabia nchi.


Vilevile Lupembe aliwataka wananchi kupanda miti kwenye makazi yao ili wajipatie kivuli, kuni na matunda na hivyo kusaidia pia kutunza mazingira.

Baadhi ya wananchi wakiwamo viongozi wa mila waliiomba serikali kusimamia kwa ukaribu misitu ili kuepuka uharibifu wa mazingira utakaopelekea kupotea kwa vyanzo vya maji.

Mwenyekiti wa Machifu jijini Mbeya, Chifu Rocket Mwashinga aliiomba serikali kuwashirikisha viongozi wa mila kwenye uhifadhi wa mazingira kwa madai kuwa wao ndio wapo karibu zaidi na wananchi na wanasikilizwa.

Alisema baadhi ya misitu ambayo inasimamiwa na machifu iko vizuri na hakuna mtu anayeruhusiwa kuingia kufanya kitu chochote isipokuwa kwa ruhusa ya machifu wenyewe.

Mwashinga alisema endapo serikali itawashirikisha kwenye zoezi hilo, wao wana sheria zao za kimila za namna ya kuwajibishana, hivyo akaomba pia washirikishwe kwenye utoaji wa elimu.





# Askari Magereza anaswa akiwa na nyara za serikali akisaka mteja

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma linawashikilia watu watatu kwa makosa mbalimbali akiwmo askari wa Jeshi la Magereza, Cosmas Ndasi wa Gereza la Msalato kwa kudaiwa kukamatwa na nyara za serikali meno ya tembo vipande sita.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma (SACP) Gilles Muroto, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa.

Muroto alisema wanashikilia watu watatu kwa kujihusisha na makosa mbalimbali ikiwamo kupatikana na nyara za serikali, kughushi na kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu.

Alisema katika tukio la kwanza Aprili 1, mwaka huu, majira ya saa 12 jioni mtaa wa Kilimani jijini hapa, alikamatwa askari Magereza mwenye namba A 8070 Sajenti Cosmas Ndasi (51) wa Gereza la Msalato akiwa na vipande sita vya meno ya ndovu.

Muroto alisema idadi hiyo ya vipande sita vyenye uzito wa kg 13 alivyokutwa navyo ni sawa na tembo watatu waliouawa ili kupatikana nyara hizo. Kamanda huyo alisema mtuhumiwa alikamatwa na akiwa na vipande hivyo vyenye thamani ya Sh. milioni 103. 5 akiwa amevificha kwenye mfuko kumsubiri mteja kufanyabiashara.

Aidha, alisema katika tukio la pili wamemkamata Mohamed Hamisi, kwa kudaiwa kujipatia mali kwa njia ya udanganyifu ambayo ni magari mawili aliyoyachukua Mikocheni mkoani Dar es Salaam mwaka 2017.

Alisema mtuhumiwa alijipatia magari hayo mawili ambayo ni Toyota Land cruiser V 8 yenye namba za usajili T 366 BRX na gari nyingine ni Toyota Noah yenye namba za usajili T 581 DKS na magari yote yana rangi nyeusi.

Aliongeza kuwa mtuhumiwa alijitambulisha kwa mmiliki wa magari kuwa yeye ni Ofisa Usalama wa Taifa na anayahitaji magari hayo kwa ajili ya kazi maalum, ambapo aliandika mkataba wa kukodi magari hayo na alipoyapata alitoweka nayo hakuyarejesha hadi alipokamatwa na Jeshi la Polisi Dodoma Aprili1, mwaka huu.

Muroto alisema mtuhumiwa huyo aliyatumia magari hayo kujipatia fedha kwa watu mbalimbali kwa kukodisha na kuyaweka dhamana na wakati mwingine aliweza kukopa fedha kisha kulitelekeza gari.

Alisema jeshi hilo linaendelea na utaratibu kwa mtuhumiwa pamoja na magari kupelekwa jijini Dar es Salaam alikoshtakiwa ili afikishwe mahakamani kujibu tuhuma dhidi yake.

Alitaja tukio la tatu kuwa ni Machi 26, mwaka huu, jeshi hilo lilimkamata Ambokile Mwampulo (32) kwa kujifanya Ofisa wa Usalama wa Taifa na kujipatia Sh. 950,000 kwa kuwadanganya watu kuwa atawatafutia ajira katika Idara za Usalama wa Taifa.

Alisema mtuhumiwa alipokamatwa na jeshi hilo alipekuliwa nyumbani kwake eneo la Ndachi jijini hapa na kukutwa na nakala 15 za vyeti vya watu, barua tatu za maombi ya ajira za watu tofauti pamoja na nakala ya leseni moja.

Kamanda Muroto alisema serikali inautaratibu wake na mfumo wa kutoa ajira kwa watu, hivyo aliwataka wananchi kujihadhari na matapeli wa aina hii ambao wanatumia vibaya majina ya taasisi za serikali na kuwaibia.



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, akionyesha meno ya tembo yaliyodaiwa kukamatwa nayo mmoja wa askari wa Jeshi la Magereza, Cosmas Ndasi wa Gereza la Msalato, jijini Dodoma, mtuhumiwa alikamatwa na meno sita eneo la Kilimani, akisubiri mteja aje kuyanunua.
**PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waombwa ushirikiano kuangamiza mazalia ya mbu

**Na Peter Mkwavila,**

DODOMA

OFISA Afya wa Jiji la Dodoma, Abdallah Mahia, amewataka wakazi wa jiji hilo kutoa ushirikiano kwa wataalamu wa afya wanaofanya kazi ya kupuliza dawa ya kuangamiza mazalia ya mbu katika maeneo mbalimbali.

Mahia aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na zoezi hilo linaloendelea jiji hapa la upuliziaji wa dawa kwa ajili ya kuangamiza mazalia ya mbu.

Alisema kuwa baadhi ya wakazi wa jiji hilo wamekuwa na imani potofu kuwa dawa hiyo inayopulizwa kwa ajili ya kuangamiza mazalia ya mbu inaweza kuwasababishia kutopata watoto, jambo ambalo siyo kweli.

Alisema kinachohitajika kwa wananchi ni kutoa ushirikiano utakaowezesha zoezi hilo kufanikishwa ili kila mkazi aweze kupata huduma hiyo ambayo hutolewa bure ikiwa ni agizo kutoka serikalini.

"Ninachowaomba wakazi wa jiji kuondokana na imani potofu hiyo na badala yake watoe ushirikiano kwa wataalamu wangu wa afya ili waweze kuwafikia na hatimaye mazalia hayo ya mbu tuyatokomeze," alisema.

Alisema kuwa mpaka sasa jumla ya lita walizotumia kwa ajili ya upulizaji ni 10,500 na bado zoezi hilo linaendelea, kwa kiasi kikubwa ugonjwa wa malaria umepungua kwa utafiti uliofanyika na Wizara ya Afya mwaka 2017.

"Tuliangalia katika magonjwa 10 yanayoambukizwa na wadudu akiwamo mbuu yameshuka hii ni kwa utafiti uliofanyika na Wizara ya Afya ya mwaka 2017 na kwa Jiji la Dodoma ina asilimia 0.8 na eneo ambalo limefanikisha kwa kuwatokomeza mbu," alisema.

Hata hivyo aliwataka watendaji wa kata kuendelea kutoa elimu itakayowezesha zoezi hilo kwenda na wakati ili kila eneo liweze kupatiwa huduma bila ubaguzi wowote.

# Serikali yaombwa kumulika huduma za kiroho

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

SERIKALI kwa kushirikina na viongozi wa dini imeombwa kuziangalia kwa jicho la pili huduma za kiroho ambazo zimekuwa zikiibuka kama uyoga bila kuwa na usajili wala vibali vya kufanya kazi hiyo katika maeneo mbalimbali nchini.


Ushauri huo ulitolewa na Mwinjilisti wa Kitaifa, Festo Machela wa Kanisa la Angalikan Dayosisi ya Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusiana na huduma za kiroho zinazoibuka ambazo hazina usajili wala vibali vya kufanya kazi hiyo.

Mwinjilisti huyo alisema kuwa pamoja na serikali kutoa uhuru wa kuabudu kuna ulazima wa kuziangalia huduma hizo kwa jicho la pili kwa kuwa uwezekano mkubwa wa kuwapotosha Watanzania kutoshirika maendeleo.

Aliwaomba viongozi wa dini pamoja na waumini kuendelea kuiombea serikali pamoja na watendaji wake ili zoezi la kubaini wapotoshaji hao liweze kukomeshwa.

"Hivi sasa hapa nchini kuna watumishi wanaojifanya ni watu wa Mungu, lakini mafundisho yao ni kinyume badala ya kuwahimiza Watanzania kufanya kazi na kulipa kodi, wao wamekuwa wakihamasisha waumini watoe mali zao kwa hao watumishi kwa kuwadanganya kuwa watabalikiwa," alisema.

Aliwataka waumini kutoa ushirikiano pindi wanapowaona watu ambao wanatoa mafundisho ambayo hayana misingi na faida kwa ajili ya kuleta maendeleo ya taifa na siyo kuliacha suala hilo kwa serikali.





Mkuu wa Idara ya Mikopo kwa wajasiriamali wa Benki ya Stanbic, Farha Mohamed, akizungumza wakati wa semina ya siku moja ya kuwajengea uwezo wanahabari iliyoandaliwa na benki hiyo jijini Dar es Salaam. Benki hiyo imejikita katika kudumisha ushirikiano na waandishi wa habari pamoja na kuwawezesha kukua katika tasnia yao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yaombwa kuweka mikakati kuinua wajasiriamali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Ajira Zanzibar, Ali Suleiman Ameir, amesema serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwanyanyua kiuchumi wajasiriamali ili kuweza kukabiliana na tatizo la ukosefu wa ajira.

Aliyasema hayo jana katika kiwanja cha kumbukumbu Kisonge wakati alipokuwa akifunga maonyesho ya kwanza ya kazi za wajasiriamali yalioandaliwa na Mtandao wa Tamaduni za Kijamii Zanzibar.

Alisema kuanzishwa kwa mfuko wa uwezeshaji, idara ya programu za uwezeshaji na vituo vya kuwaendeleza wajasriamali kumesaidia baadhi ya wananchi hususan vijana kupata mbinu mbadala za kujiajiri.

"Hivi sasa vijana wengi wamejiajiri katika ujasiriamali baada ya kuona kuwa wanakabiliwa na changamoto ya ajira," alisema.

Aidha, aliwataka wajasiriamali hao kutovunjika moyo kutokana na matatizo madogo yanayojitokeza na badala yake wazidishe juhudi ili kuweza kufikia malengo waliojipangia ya kujikomboa na umaskini.

Mkurugenzi huyo aliwataka wananchi kuthamini bidhaa za wajasiriamali wa ndani badala ya bidhaa kutoka nje ya nchi wakati bidhaa hizo zinapatikana nchini. Naye Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji Zanzibar, Omar Said Ameir, aliwataka wamiliki wa vyombo vya habari kuwaunga mkono wajasiriamali kwa kuzitangaza bidhaa wanazozizalisha ili ziweze kufahamika na kupata soko la uhakika la ndani na nje ya nchi.

Alieleza kuwa vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika kuwainua wajasiriamali na kuwatangaza ili bidhaa zao ziweze kutambulika. Kwa upande wake Mwenyekiti wa Mtandao wa Tamaduni za Kijamii Zanzibar, Ameir Abdallah Ameir, alisema wajasiriamali wanakabiliwa na matatizo mbalimbali kama vile uhaba wa fedha, vifungashio na kukosa soko la uhakika wa kuuzia bidhaa wanazozizalisha.

# Waziri awapa neno walimu wakuu

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema walimu wakuu ndiyo wenye jukumu la kusimamia kazi za wenzao ili kuleta maendeleo katika sekta ya elimu nchini.

Akizungumza wakati akimtambulisha Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Simai Mohamed Said, kwa walimu wakuu wa Shule za Sekondari za Unguja, alisema kuna baadhi ya walimu wamekuwa wanaendelea kuwatoza fedha wanafunzi kwa visingizio mbalimbali hali ambayo serikali ilipiga marufuku suala hilo.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haitowafumbia macho walimu wenye tabia hiyo na kuwataka walimu wakuu kuwafuatilia walimu hao ili kutimiza azima ya serikali ya kutoa elimu bure kwa wote.

Alisema pesa zinazotolewa na serikali ni kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anapata haki yake ya elimu bure kuanzia maandalizi, msingi hadi kidato cha nne kama inavyoeleza Sera ya Elimu ya Mwaka 2006.

Aidha, waziri huyo alisema shule zinaweza kuendeleza miradi ya uzalishaji mali na sio mwalimu kumchangisha mwanafunzi kwa malengo ya kupata elimu.

Akizungumzia suala la kambi kwa wanafunzi kwa ajili ya maandalizi ya mitihani, aliwataka walimu wakuu kuhakikisha kuwa kambi zinazoshughulikia wanafunzi lazima kuwapo walimu wasimamizi na pamoja kuhakikisha kambi zote zinakuwa na mazingira mazuri ya kuridhisha.

Waziri huyo aliwataka walimu wanaosimamia kambi hizo za wanafunzi kuhakikisha wanawatenganisha wanafunzi wa kike na kiume, ili kuepusha vishawishi vitakavyoweza kuwaharibia masomo yao.

Naye Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohammed Said, aliwataka walimu kutovunjika moyo kutokana na ugumu wa kazi na badala yake kuwa na uzalendo wa kujitolea ili kuleta maendeleo katika elimu.

Alieleza kuwa wizara itaendelea kushirikiana na walimu pamoja na wazazi ili kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi unaongezeka na kuzitokomeza zero Zanzibar katika mitihani ya taifa.

# Masheha watakiwa kuzingatia maadili ya uongozi

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MASHEHA wa Mkoa Mjini Magharib wametakiwa kuzingatia mafunzo ya uongozi na maadili waliyopatiwa ili kuleta mabadiliko ya uongozi ndani ya jamii.

Akifunga mafunzo kwa masheha hao yaliyoandaliwa na uongozi wa mkoa huo, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo viongozi hao.

Alisema matokeo ya mafunzo hayo yatapimwa kutokana na mabadiliko ya kiutendaji wa viongozi hao katika kusimamia na kutekeleza sheria, kanuni na dhana ya maendeleo ya jamii kwa ujumla.

Aidha, Shamata alieleza kuwa masheha ni viongozi muhimu kutokana na kuwa ndio ngazi ya kwanza ya serikali hivyo wanapaswa kuwa waadilifu, waaminifu na kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni za utumishi wa umma.

Naibu Waziri huyo alisema haipendezi kuona kiongozi wa serikali anakosa kuwa na maadili, hivyo aliwakumbusha masheha hao kuacha kufanyakazi kwa mazoea.

Naye Mkuu wa Mkoa Mjini Magharib, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa mkoa wa kuwajengea uwezo watendaji wake ili kuongeza uaminifu kwa jamii wanayotumikia.

Alieleza kuwa anaamini mafunzo hayo yatakapotolewa kwa viongozi wengine wa mkoa yataongeza ushirikiano kati ya serikali na wananchi kwa kuwa yamelenga kuimarisha uaminifu na uadilifu wa viongozi hao wa ngazi ya awali katika jamii.

Ayoub aliwataka masheha hao kuyatumia kikamilifu mafunzo yaliyoyapata ili kuona mabadiliko makubwa yatapatikana katika utendaji wa kazi na kuimarisha huduma kwa wananchi.

Kwa upande wao masheha hao, walisema mafunzo hayo yamewasaidia kuelewa masuala mbalimbali ya uongozi na utekelezaji wa kazi zao na kuahidi kuyafanyia kazi kikamilifu.

# Hatimaye Rais wa Algeria ajiuzulu

**ALGERS, Algeria**

RAIS wa Algeria, Abdelaziz Bouteflika, amekabidhi barua yake ya kujiuzulu, akiachia madaraka wakati kukiwa na maandamano makubwa dhidi yake baada ya miongo miwili ya uongozi wake.

Baada ya taarifa hizo, sauti za honi za magari zilisikika mjini Algiers kabla ya watu waliobeba na kupeperusha bendera za nchi hiyo kutoka majumbani na kumiminika mitaani wakishangilia habari ya kujiuzulu kwa Rais Bouteflika.

Akitumia televisheni ya kitaifa nchini humo, Bouteflika aliliambia rasmi baraza la katiba juu ya hatua ya kumaliza muda wake wa uongozi kama rais wa taifa hilo.

Bouteflika alisikika akisema hatua aliyoichukua anatumai itatoa nafasi kwa Algeria kusonga mbele na kuwa na mustakabali mwema.

Algeria kwa sasa inapitia kipindi cha mpito baada ya Rais Bouteflika kujiuzulu na masuala juu ya nini kitafuata kwa taifa hilo tajiri kwa gesi na mshirika wa Magharibi katika kupambana na ugaidi yameanza kuibuka.

Baraza la kikatiba lililo na wanachama 12 nchini Algeria lilitarajia kukutana jana ili kuthibitisha hatua ya kujiuzulu kwa Bouteflika.

Kituo cha Televisheni ya Taifa kilimwonyesha kiongozi huyo akimkabidhi rasmi barua yake ya kujiuzulu rais wa baraza hilo, Tayeb Belaiz.

Katiba ya Algeria inasema rais akifariki dunia au kujiuzulu baraza la katiba ni lazima lithibitishe kabla ya mabunge yote mawili kukutana, spika wa bunge kuteuliwa kama rais wa mpito kwa siku 90, wakati uchaguzi mkuu ukiandaliwa.

Hivyo, Abdelkader Bensalah aliye na miaka 77 mshirika wa Bouteflika ambaye ndiye spika wa bunge la sasa nchini Algeria ndiye atakuwa rais wa mpito wa nchi hiyo.

Marekani imepongeza hatua ya Rais Bouteflika kujiuzulu na kusema mustakabali wa Waalgeria kwa sasa utaamuliwa na wa Algeria wenyewe.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, Robert Palladinol, alisema masuala juu ya namna mipango yote itakavyoendeshwa baada ya Rais Bouteflika kujiuzulu itaamuliwa na watu wa taifa hilo.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Yves Le Drian, alisema hatua ya Rais Bouteflika inafungua ukurasa mpya na muhimu katika historia ya Algeria.

Rais huyo wa zamani wa Algeria mwenye miaka 82 aliyeshutumiwa kwa muda mrefu kung'ang'ania madaraka, amekumbana na shinikizo kubwa la kutakiwa ajiuzulu baada ya kutaka kuwania muhula wa tano madarakani licha ya kutoonekana hadharani tangu mwaka 2013 alipougua kiharusi.

*DW*

# Wamalawi waishio Afrika Kusini waomba kurudishwa nyumbani

**JOHANESSBURG, Afrika Kusini**

BAADHI ya raia wa Malawi wanaoishi mjini Durban nchini Afrika Kusini, wameomba kurudishwa nyumbani, hatua hiyo imekuja baada ya kushambuliwa na raia wa Afrika Kusini.

Uvamizi wa raia hao wa kigeni ulisababisha wananchi wa Malawi wapatao 300 kuyakimbia makazi yao.

Makazi yao yalivamiwa na biashara zao kuharibiwa na wenyeji, suala ambalo limeikasirisha serikali ya Afrika Kusini na kuwataka maofisa wa usalama kuwakamata na kuwachukulia hatua waliohusika.

Wiki iliyopita, Rais wa Afrika Kusini, Cryril Ramaphosa, alishutumu ghasia hizo za mashambulizi dhidi ya wageni, na kutoa wito kwa taasisi za kiusalama kuwakamata wanaotekeleza vitendo hivyo.

Alisema kuwa ghasia hizo ambazo zimekuwa zikiwalenga raia wa Malawi na wengine kutoka nchi za Afrika katika Jimbo la Kwazulu Natal ni suala la kujutia hususani katika kipindi hiki ambacho taifa hilo lilikuwa linaadhimisha miaka 25 tangu uchaguzi wa kidemokrasia ufanyike nchini humo.

Wimbi la raia wa Afrika Kusini kuwavamia wageni kutoka mataifa mengine ya Afrika, limeendelea kuzua wasiwasi nchini humo.

Juzi, watu watatu walifariki kufuatia maandamano yanayolenga maduka, ambayo mengi yanamilikiwa na wageni.

Takribani watu 50 walitafuta hifadhi katika kituo kimoja cha polisi wakati kundi la vijana wasio na kazi walipowashinikiza kutoka katika nyumba zao usiku.

*RFI*



Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, akiongoza moja ya ibada. **PICHA: REUTERS**

# Papa asema ni halali wanawake kutaka usawa kanisani

**ROMA, Italia**

KIONGOZI wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis, amesema wanawake wana madai halali ya kutaka usawa katika kanisa.

Aliyasema hayo katika waraka wake mrefu uitwao 'Yesu bado yuko hai' na kwamba kanisa linalowasikiliza vijana linapaswa pia kuyazingatia madai halali ya wanawake juu ya haki na usawa.

Alieleza kuwa kanisa lina jukumu la kutoa mafunzo mazuri zaidi kwa wanaume na wanawake wenye uwezo wa kuongoza.

Waraka huo uliotolewa kwa ajili ya vijana wa Wakatoliki wa leo, inatokana na mkutano wa maaskofu uliofanyika mwezi Oktoba mwaka jana, ambapo maaskofu hao walijadili njia bora ya kuwahudumia vijana, ambapo suala la utashi wa haki zaidi kwa wanawake lilikuwa la kipaumbele.

Katika azimio lao, maaskofu walitoa wito kutaka wanawake wapewe nafasi za uongozi na mamlaka ya kushiriki katika kupitisha maamuzi ya kanisa.

Katika hati yake, Papa Francis alisema kanisa linapaswa kuiangalia historia yake na kutambua kwamba pamekuwapo na udikteta wa wanaume, utumwa wa aina mbalimbali na unyanyasi wa kingono.

Akizungumza na waandishi habari juu ya kutozingatiwa suala la mashoga katika hati ya Papa Francis, mwandalizi wa mkutano wa maaskofu, Kadinali Lorenzo Baldsseri, alieleza kuwa baba mtakatifu amekiri katika hati yake kwamba hawezi kuandika upya kila kitu.

Katika waraka wake, Papa Francis alihamasishwa na mapendekezo muhimu zaidi yaliyotolewa kwenye mkutano wa maaskofu.

Papa Francis alitoa wito wa kuleta mageuzi ya haraka kwenye shule za wakatoliki na mafunzo ya ukasisi.

Kuhusu udhalilishaji wa kingono, Papa Francis pia alitoa wito wa kuung'oa mfumo wa mamlaka ambao umekuwa unatumika ndani ya kanisa uliowezesha uhalifu huo kutendeka.

Alisema mbegu ya ufisadi inatokana na uroho wa mamlaka, ukosefu wa mdahalo, uwazi, maisha ya undumilakuwili na pia inatokana na utovu wa imani na udhaifu wa kimawazo.

Aliwataka waumini kuwakemea makasisi wanaotaka kujiburudisha kwa kuwadhulumu vijana na kuwakumbusha wajibu wao kwa Mungu na kwa watu wao.

*DW*

# Udhalilishaji wanafunzi tishio shule za msingi

**Na Waandishi Wetu, KAHAMA**

ZAIDI ya wanafunzi 20 wa Shule ya Msingi Nyasubi katika Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wameripotiwa kufanyiwa matukio ya udhalilishaji, huku wengine wakifanyiana wenyewe kwa wenyewe.

Vitendo hivyo vimetajwa kuwa ni ubakaji, unajisi na ulawiti.

Katika matukio hayo ilidaiwa kuwa mtoto wa shule ya awali alinusurika kubakwa na mtu asiyejulikana baada ya kukutwa na wasamaria wema akiwa ameshavuliwa nguo ili kufanyiwa kitendo hicho.

Wasamaria wema walimkuta mtoto akiwa katika nyumba ambayo haijaisha akiwa hana nguo na kuamua kumchukua hadi shuleni kwao na kumkabidhi kwa mwalimu mkuu wa shule hiyo.

Ilielezwa kuwa mwalimu huyo alichukua jukumu la kumpeleka hospitali kwa ajili ya uchunguzi na kubainika alikuwa bado hajaingiliwa.

Mkuu wa shule hiyo, Robisita Adolph, alitoa taarifa hiyo katika kikao maalumu cha shule kilichojumuisha wazazi, walimu pamoja na watu wa dawati la jinsia kutoka Jeshi la Polisi, kilichoitishwa na kamati ya shule ili kujadili tatizo hilo ambalo limeibuka shuleni hapo la wanafunzi kufanyiwa vitendo vya ulawili, ubakaji na unajisi.

Alisema, kuna mtoto wa miaka minne aliyekuwa akitoka nyumbani kwenda shuleni na kukutwa njiani akitembea mwendo wa kunyong'onyea huku kinyesi kikimtoka na alipoulizwa alisema kuwa, aliitwa na vijana waliokuwa katika jengo ambalo halijaisha na kumfanyia vitendo hivyo.

Hata hivyo, Adolph alisema, pamoja na kumwita mzazi wa mtoto huyo kwenda shuleni kwa ajili ya kuambiwa tukio lililompata mwanawe, mzazi huyo hakuitikia wito huo. Alisema baadhi ya wazazi wanaogopa aibu wanaporipotiwa matukio ya watoto wao.

Kuhusu ulawiti, alisema shule ilifanya uchunguzi na kuwabaini watoto 15 walioalawitiwa, kati yao 12 walionekana wakihusika na vitendo hivyo kwa njia moja au nyingine, na tisa walikutwa na uzoefu wa kujamiiana, mmoja akiwa tayari sugu katika masuala hayo.

Alisema kuwa mtoto huyo ambaye ameshakuwa sugu yuko darasa la saba.

Aidha, alisema watoto hao walibainika baada ya wenzao kutoa ushirikiano katika ofisi za Ustawi wa Jamii walipokuwa wakihojiwa.

Ofisa wa Dawati la Jinsia kutoka Jeshi la Polisi Kahama, Koplo Njile, alisema kuwa watoto zaidi ya 20 wana madhara ya kulawitiwa, huku kesi nyingi za matukio hayo ni kutoka katika shule hiyo na shule za msingi Kilima, Korogwe na Mhongolo.

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka kila siku kutokana na wazazi kutofika shuleni kufuatilia maendeleo ya watoto wao na badala yake wakiwaachia majukumu hayo walimu ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa na kazi nyingi.

Mwenyekiti wa Serikali za Mtaa wa Nyasubi, Alphonce Mayunga, aliwaomba wazazi kuandika majina ya wamiliki wa nyumba zote ambazo hazijamaliziwa ujenzi ili waitwe na wazikamilishe kwa wakati kumaliza matatizo hayo.

Mmoja wa wazazi ambaye mwanawe alifanyiwa vitendo hivyo (jina linahifadhiwa), alisema mwanawe ni mwathirika wa vitendo hivyo na kuongeza kuwa anasikitika kwamba amezaa mtoto wa kiume na ameguzwa mtoto wa kike. "Sidhani kama atabadilika kwa urahisi."

"Mimi nina mtoto wa kiume ambaye naye amefanyiwa vitendo hivyo anasoma darasa la saba na alikuwa na akili sana darasani, lakini sasa kuna mabadiliko makubwa sana na niligundua baada ya kumvua nguo na kubaini kuwa ameshaharibika sana sehemu zake za haja kubwa," alisema.

*Imeandaliwa na Shaban Njia na Mohab Dominick

## Bei ya petroli, dizeli yapaa

**Na Gwamaka Alipipi**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Ewura), imetangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli ambazo zimeanza kutumika jana.

Taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Ewura, Nzinyangwa Mchany kwa vyombo vya habari ilieleza kuwa bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya petrol na dizeli yaliyoingizwa nchini kupitia bandari ya Dar es Salam zimeongezeka ikilinganishwa na toleo lililopita.

Ilieleza kuwa mwezi Aprili, bei za rejareja za petroli na dizeli zimeongezeka kwa Sh. 49 kwa lita sawa na ongezeko la asilimia 2.34 na Sh. 61 kwa lita sawa ongezeko la asilimia 2.87.

Kwa mujibu wa jedwali lililotolewa na Ewura, mafuta ya petroli kwa Jiji la Dar es Salaam ni Sh. 2,147 kwa lita, dizeli Sh. 2,192 na mafuta ya taa Sh. 2,096 kwa lita.

Kwa Mkoa wa Arusha, mafuta ya petroli ni Sh. 2,192 kwa lita, dizeli ni Sh. 2,196 kwa lita, mafuta ya taa Sh. 2,286 kwa lita.

Mkoa wa Mwanza, mafuta ya petroli ni Sh. 2,297, dizeli Sh. 2,342, na mafuta ya taa ni Sh.2,247.

"Ewura inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo zinapatikana pia kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba *152*00# na kisha kufuata maelekezo, kwa mujibu wa sheria za mafuta ya mwaka 2015 bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. Ewura itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa ya mafuta," ilieleza taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi bei hizo zisivuke bei kikomo.

Kadhalika, ilieleza vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana, huku yakionyesha bei hizo, punguzo, vituo vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika.




Mkurugenzi Mtendaji wa Dodoma Builders Expo 2019, Tatenda Nyawo (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maonyesho ya wadau wa sekta ya ujenzi yanayotarajiwa kufanyika Juni 7-8 mwaka huu, jijini Dodoma. Kushoto ni Mkuu wa Biashara, Rose Kilembe na mratibu wa maonyesho hayo, Albert Makoye. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Serikali kufanya utafiti ukubwa athari za usagaji, ushoga

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

BUNGE limeelezwa hadi sasa serikali haina takwimu za hali ya usagaji na ushoga nchini.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Katika swali lake, alibainisha kuwapo masuala ya kunajisi na ubakaji kwa watoto pamoja na mapenzi ya jinsia moja kukithiri nchini na kuongezeka siku hadi siku na kuhoji serikali haioni umuhimu wa kufanya utafiti wa kina na kuona athari zinazoendelea kuikumba jamii katika suala zima la usagaji.

"Je, ni lini serikali itaanza kuandaa sheria ya kuwaadhibu wanawake wanaoharibu vijana wa kiume chini ya umri wa miaka 18, kuwafunza na kuwaharibu watoto wetu wa kike katika masuala ya usagaji," alihoji. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri alisema Sheria na Kanuni ya Adhabu sura ya 16 inakataza vitendo vilivyo kinyume na maadili ikiwamo mapenzi ya jinsia moja,

Hata hivyo, alisema hadi sasa serikali haina takwimu za hali ya usagaji na ushoga nchini, hivyo inaona umuhimu wa kufanya utafiti wa kina kuhusu masuala ya mapenzi ya jinsia moja ikiwamo usagaji kubaini ukubwa wa athari za suala hilo.

"Pindi utafiti utakapofanyika, serikali itaangalia uwezekano wa kuzifanyia marekebisho na kuboresha sheria zilizopo ili kukabiliana na suala hilo," alisema.

Pia alisema serikali inatambua kuwa sheria peke yake haitoshi kutatua suala hilo, hivyo inaendelea kutoa elimu kuhusu malezi chanya yanayozingatia maadili ya kitanzania.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VINAUZWA, VIWANJA VINAUZWA CHANIKA** mita 100 kutoka stendi mpya ya Chanika. Umeme upo Bei kuanzia Mil.2. Kwa Mawasiliano: 0714 187555/ 0755 288879

## NAFASI ZA KAZI


**NAFASI ZA KAZI UALIMU /** certificate au diploma /english/ mathematics /SST na science 0656490706/0655628640


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311



## PASSPORT IMEPOTEA



**GEOFREY MASHAURI MFINANGA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB304604** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 08 Januari, 2009. Mwisho wa matumizi ya Passport hii ilikuwa tarehe 07 Januari, 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi **AR/RB/2871/019.**

25148502

## KUPOTEA KWA VYETI



**Jumaa Mustapha** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0672/0202** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2014 katika shule ya Sekondari Mkwakwani na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S2278/0570** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2017 katika Shule ya Sekondari Macechu.

**Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: TAN/RB/1943/2019**

115155602

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISACK LAZARO CHISUNGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA CROWN yenye namba za usajili T414 DPA. Chassis namba **GRS1800032574.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **OB/RB/2858/2019.**

115156001

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 03/04/2019

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya IJUMAA tarehe 05/04/2019 kampuni ya **WULKAN ENG** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **NAMANGA kuelekea MERERANI** gari hilo lenye namba za usajili: **T827 BCN, T741 CPB, T985 ABJ.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   - Urefu -mita 17
   - Upana -mita 3.0
   - Kimo -mita 3.2
3. Njia itakayotumika **NAMANGA hadi MERERANI** kupitia **MBUGUNI ROAD** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115156802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya Mwanzo …KAWE

Usimamizi wa mirathi……… 33………2019

Ombi la **CHEMPHAEY ABDALLAH MAGANGA** Kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu JUMA ABDALLAH MAGANGA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 17/04/2019.Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo ya **JUMA ABDALLAH MAGANGA.** Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe …..

Mahakama ya Mwanzo:
Kinondoni Kimara,Sinza,Ilala,Temeke
Mbagala,Ukonga,Kigamboni,Buguruni

115155502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MAULID JAPHET** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA RAUM yenye namba za usajili T466 DLM. Chassis namba **NCZ200101624.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: **KJN/RB/1560/2019**.

115155901

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Fredolin Mbelwa Eustace** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari ya usajili yenye wa namba **T529 BPL,** chasis namba MCU250053124, engine namba IMZE1267545.

Yeyote atakaeipata atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa: OB/RB/3214/2019**

115155401


*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*

*Tupigie 0767 223 311*

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# UNITED, LEICESTER ZAMWANIA TIELEMANS

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United itachuana na Leicester katika kuwania saini ya Youri Tielemans katika kipindi cha majira ya joto baada ya kiungo huyo kuwa kwenye orodha ya wachezaji wake inaotaka kuwasajili.

Mchezaji huyo wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, ambaye yuko kwa mkopo kwenye Uwanja wa King Power, ameonyesha uwezo mzuri tangu alipojiunga na Foxes Januari mwaka huu, amefunga bao moja na kutengeneza nafasi nne za magoli.

Brendan Rodgers ameweka wazi kwamba anataka kumpa mkataba wa kudumu Tielemans katika kipindi cha majira ya joto mwaka huu, lakini sasa atatakiwa kupambana na United kuwania saini ya kiungo huyo.

Gazeti moja la Ubelgiji liitwalo, Het Laatste limeandika kuwa Kocha, Ole Gunnar Solskjaer anajiandaa kumsajili nyota huyo wa zamani wa Anderlecht, ambaye thamani yake imetajwa kuwa ni pauni milioni 40.

Tottenham imetajwa pia kuonyesha nia ya kumsajili, Tielemans, ambaye atairuhusu Monaco kumweka sokoni wakati wa dirisha la usajili litakapofunguliwa tena.

Tayari Leicester imeshaanza mazungumzo na klabu hiyo ya Ligue 1 na inajipanga kumtumia, Adrien Silva, kama sehemu ya kufanikisha usajili wa mchezaji huyo.

"Ni mchezaji chipukizi ambaye ana kipaji cha hali ya juu. Lakini kila siku huwa naheshimu kuwa ni mchezaji halali wa Monaco. Nina hakika tutafanya mazungumzo baina ya klabu hizi mbili.

"Ni mchezaji ambaye ningependelea kuendelea kufanya naye kazi. Ni mchezaji ambaye anazidi kuimarika."




# KATI YA COURTOIS AU NAVAS KUUZWA

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid inaweza kumuuza golikipa wake,Thibaut Courtois au Keylor Navas katikati ya mwaka baada ya kocha Zinedine Zidane kusema kuwa klabu yake itakuwa na uhakika wa kipa namba moja msimu ujao.

Zidane pia ametetea uamuzi wake wa kutowapanga makipa hao wawili katika mechi ya Ligi ya Soka ya Hispania Jumamosi, na badala yake akampanga mtoto wake mwenye umri wa miaka 20, Luca na hivyo kucheza mechi yake ya pili akiwa katika kikosi cha kwanza cha Madrid.

Courtois alinunuliwa kutoka Chelsea katikati ya mwaka jana, licha ya Navas kushinda tuzo ya Kipa Bora ya UEFA baada ya kuiwezesha Real Madrid kutwaa Kombe la Ligi ya Mabingwa wa Ulaya.

Baadaye Santiago Solari aliumuamini zaidi Courtois katika kipindi cha miezi minne alichofundisha Madrid lakini Navas, ambaye ni chaguo la Zidane, alirejea katika kikosi cha kwanza katika mechi ya kwanza ya Mfaransa huyo dhidi ya Celta Vigo mwezi uliopita.

"Kwa sasa kuna makipa watatu bora na tutamaliza nao msimu," alisema Zidane katika mkutano na waandishi wa habari.

"Lakini nawahakikishia msimu ujao hakutakuwa na mjadala kuhusu kipa, nawaambieni sasa. Itakuwa bayana kabisa."

Kupandishwa kwa Luca Zidane ambako hakukutegemewa kulitokana na Courtois kuumia wakati akiichezea Ubelgiji katika mechi ya kimataifa, huku Navas alikuwa amefanya mazoezi siku moja tu baada ya kurejea kutoka Costa Rica.

Lakini uamuzi huo unamaanisha kuwa Zidane anaamini kuwa mtoto wake, ambaye alijiunga na Madrid akiwa na umri wa miaka sita wakati baba yake akisakata soka, yuko tayari kupambana kupata nafasi katika kikosi hicho.

"Luca yuko hapa kwa sababu ya uwezo," alisema Zidane. "Amekuwapo hapa kwa miaka 16. Kama watu watataka kuendelea kuzungumzia mambo binafsi, sijali."

# Unai: Ozil hana mfano wake

**LONDON, England**

KIUNGO wa Arsenal, Ozil Mesut hivi sasa ameonekana kuwa lulu baada ya kuonyesha kiwango bora dhidi ya Newcastle United.

Kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu uliopigwa Jumatatu, Arsenal iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 na kupanda hadi katika nafasi ya tatu.


Kiwango chake kimemkuna kocha wake Emery Unai ambaye amemtaja ni mmoja wa wachezaji wenye uwezo mkubwa.

Emery alisema Ozil alikuwa injini ya Arsenal katika mchezo huo wa Ligi Kuu na alichangia ushindi wa mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Emirates.

Kauli ya Emery imekuja baada ya muda mrefu kumweka benchi nyota huyo wa zamani wa Real Madrid tangu alipotwaa mikoba ya Arsene Wenger.

Ozil aliyefunga mabao matano katika mechi 26 alizocheza Arsenal, amekuwa katika hali ngumu ndani ya klabu hiyo baada ya kushutumiwa mara kwa mara na mashabiki kwamba hana kiwango bora.

"Mesut Ozil amecheza jinsi nilivyotaka, ndiye mchezaji bora wa mechi. Napenda kila mchezaji acheze kwa kiwango bora na Mesut ameonyesha ubora na kutusaidia kupata ushindi," alisema kocha huyo wa zamani wa Paris Saint Germain.



Kocha huyo alisema kiungo huyo alionyesha kipaji cha soka na alimfurahisha kwa namna alivyokuwa akitawala mchezo huo.

Ozil ameanza mara tatu katika mechi tangu Desemba 26. Emery alisema licha ya kupata ushindi huo, Arsenal ina kibarua kigumu kupambana na miamba mingine ya Ligi Kuu England Tottenham Hotspurs, Chelsea na Manchester United.

## HABARI MICHEZO



# KLOPP:
## UNITED NI KLABU YENYE BAHATI

**LIVERPOOL, England**

LICHA ya kwamba mchezo wa marudiano wa mashindano ya Kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora kati ya PSG dhidi ya Manchester United kuwa gumzo kwa penalti ya dakika za mwisho, wengi walishangazwa na uwezo wa mashetani wekundu hao kupindua matokeo ugenini.

Mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye dimba la Old Trafford ambao ni uwanja wa nyumbani wa United, ulishuhudiwa wakipoteza kwa mabao 2-0, hivyo baada ya kwenda ugenini jijini Paris wakashinda magoli 3-1.

Na ushindi huo ukaitupa nje ya mashindano PSG, watu wengi walishangazwa na matokeo hayo.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp ni moja kati ya watu walioshangazwa na ameweka wazi hisia zake hizo akihojiwa na Canal Football kwa kusema kuwa huo ni mchezo dhidi ya timu isiyokuwa na bahati aliowahi kuuangalia katika maisha yake kwa maana PSG walitawala katika mechi zote mbili.

"Moja kati ya michezo iliyokosa bahati ambayo nimewahi kuiangalia ni (PSG vs Man United) kiukweli, niliiangalia ile mechi, kiuhalisia ilikuwa haiwezekani (PSG) kupoteza walikuwa wazuri katika michezo yote miwili," alisema Klopp.



## MESSI, RONALDO WAONGOZA KULIPWA FEDHA NYINGI

**MADRID, Hispania**

WAKATI ligi mbalimbali barani Ulaya zinaelekea kumalizika, jarida la France Football limetoa orodha ya wanasoka watano wanaolipwa 'mkwanja mrefu' zaidi Ulaya kwa msimu wa 2018/2019.

Katika orodha hiyo, wametajwa wachezaji hao ambao wameingiza kitita kikubwa zaidi kutokana na mishahara yao pamoja na bonasi na matangazo.

Nahodha wa Barcelona, Lionel Messi ndio anashika namba moja kwenye orodha hiyo, akiwa ameingiza kiasi cha euro milioni 130 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 336.

Nyota wa Juventus, Cristiano Ronaldo ameendelea kushindana na Messi ambaye wamekuwa wakichuana viwanjani kwa muda mrefu, kwani yeye anashika nafsi ya pili kwa kuingiza euro milioni 113 ambazo ni sawa na zaidi ya Sh. bilioni 292.

Mshambuliaji wa Paris Saint Germain, Neymar inawezekana mkataba wake wa ubalozi wa QNB unampa mkwanja mrefu, kwani ameingiza kiasi cha euro milioni 91.5 ambazo sawa na zaidi ya Sh.bilioni 236 na anashika nafasi ya tatu.

Antoine Griezman, mshambuliaji tegemeo wa Atletico Madrid, amefanikiwa kuingia kwenye orodha hiyo na kushika nafasi ya nne na ameingiza kiasi cha euro milioni 44 ambazo ni sawa na zaidi ya Sh.bilioni 113.

Gareth Bale wa Real Madrid ndio anahitimisha katika orodha hiyo kwa kufanikisha kuingiza kiasi cha euro milioni 40.2 ambazo ni zaidi ya Sh. bilioni 103.

## Bale agoma kuondoka Madrid

**MADRID, Hispania**

MSHAMBULIAJI, Gareth Bale anasema kuwa ataendelea kubakia Real Madrid baada ya kumalizika kwa msimu huu, licha ya kuwapo kwa sintofahamu ya hatima yake ndani ya Bernabeu.

Wakati nyota huyo raia wa Wales amekuwa akipambana kuziba pengo lililoachwa na Cristiano Ronaldo, lakini kumekuwa na tetesi kwamba anajiandaa kurejea katika Ligi Kuu England katika kipindi cha usajili majira ya joto, wakati Madrid ikijipanga kukijenga upya kikosi chake.

Uamuzi wa Madrid kutaka kukijenga upya kikosi chake unatokana na klabu hiyo kutokuwa na msimu mzuri mwaka huu.

Manchester United inatajwa kuwa moja ya klabu zinazohitaji saini ya mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 29, lakini kwa mujibu wa jarida ya Marca limeandika kuwa Bale hana mpango wa kumaliza mwaka wake wa sita katika jiji hilo la makao makuu ya Hispania.

Mkataba wa Bale unatarajiwa kumalizika katika kipindi cha majira ya joto mwaka 2022 na imetaarifiwa kwamba mshambuliaji huyo amesema hataki kuondoka Bernabeu katika kipindi kinachokuja cha usajili.

Hata hivyo kumekuwa na lawama kwamba Rais wa Real Madrid, Florentino Perez, amekuwa akielezwa juu ya changamoto ya ubaguzi anayokutana nayo pamoja na nafasi ya kucheza na kutimiza majukumu aliyonayo ambayo yataamua hatima yake.

Mshambuliaji huyo ameshinda mataji 14 akiwa na klabu hiyo ya Hispania na alikuwapo katika kikosi cha ushindi kilichochukua kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya katika mchezo wa fainali dhidi ya Liverpool.

Bale aliweka wazi kuwa tayari alishafikia uamuzi kuhusu hatima yake tangu kipindi cha majira ya joto kilichopita lakini kurejea kwa Zinedine Zidane katika nafasi yake ndiye atakayeamua kama ataendelea au ataondoka ndani ya kikosi hicho cha Madrid.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: KUMALIZA TOP 4 EPL NI NGUMU

● ● ● Sasa United inahitaji pointi 15 katika mechi zake sita zilizosalia...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amekiri kuwa nafasi ya timu yake kumaliza katika nafasi nne bora kwenye Ligi Kuu England ni ndogo baada ya kufungwa mabao 2-1 na Wolverhampton Wanderers juzi Jumanne.

Scott McTominay alifunga bao lake la kwanza kwa United kuiwezesha kuwa mbele, lakini Diogo Jota akasawazisha kabla ya Chris Smalling kujifunga na kuwafanya mashetani wekundu hao kuondoka kwenye dimba la Molineux wakiwa mikono mitupu.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Solskjaer alisisitiza kuwa, United bado inaweza kumaliza kwenye nne bora, lakini itakuwa ngumu baada ya kupoteza mchezo wa juzi.

Alisema: "Kufungwa ni kupoteza pointi tatu. Tulijua kabla kuwa ili tufikie nafasi ile tulihitaji kupata pointi 15. Tunahitaji mechi tano kupata pointi hizo 15.

"Tunatakiwa kuangalia mbele namna gani tutaweza kufikia nafasi hiyo. Nilisema kwamba tulihitaji pointi 15 kutoka mechi saba. Sasa ni pointi 15 kutoka mechi sita.

"Hatuna muda wa kupoteza mechi nyingi. Ni ngumu kwa upande wetu, lakini tuna timu nzuri, hivyo itakuwa ni ngumu kwa timu ambayo itacheza dhidi yetu."

United ilikosa nafasi ya kuwapiku Arsenal na Tottenham Hotspur katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, na badala yake imebakia nafasi ya tano.

Wako pointi sawa na kikosi cha kocha Mauricio Pochettino kilichopo nafasi ya nne, lakini United imecheza mechi moja zaidi.

Kama Chelsea iliifunga Brighton and Hove Albion jana Jumatano, United watashuka hadi nafasi ya sita kwenye msimamo, na itapitwa pointi nne kwenye nne bora.

## KWA UFUPI

### BALE: SIONDOKI MADRID
MSHAMBULIAJI wa Real Madrid na Timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale amemweleza mtu wake wa karibu kuwa hana mpango wa kuondoka Bernabeu katika dirisha la usajili wa kipindi cha majira ya joto. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 29 anahusishwa na tetesi za kurejea Tottenham, huku pia Manchester United ikimwinda. ***(Marca, via Inside Futbol)***

### ZIDANE "KUMBEBA" BALE
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane, bado hajaamua kama mshambuliaji wa timu hiyo, Gareth Bale ataondoka klabuni hapo, alisema hatima ya mshambuliaji huyo itajulikana mwishoni mwa msimu huu. ***(Mirror)***

### VARANE HATAONDOKA- ZIDANE
KOCHA Zidane amekanusha uamuzi wa beki wake Mfaransa, Raphael Varane (25) kuwa anaondoka Real. Kocha huyo amesema kuwa anajua kama Varane anatakiwa na Manchester United: "Sitaikubali Madrid ambayo haitakuwa na Varane." ***(Marca)***

### VARANE KUIFILISI UNITED
REAL Madrid itahitaji kulipwa kiasi cha pauni milioni 429 kwa klabu yoyote itakayotaka kumsajili beki wake wa kati Mfaransa, Raphael Varane. Dau hilo limetajwa katika mkataba wake. ***(Goal.com)***

### COURTOIS KUUZWA
KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane ameweka wazi kuwa atamuuza golikipa wa zamani wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Thibaut Courtois (26), katika kipindi cha majira ya joto. ***(Mirror)***

### UTD, SANCHO KITAELEWEKA
MANCHESTER United imemtaja winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho ndio mchezaji namba moja itakayemsajili katika kipindi cha majira ya joto katika malengo ya kujiimarisha na iko tayari kulipa dau la zaidi ya pauni milioni 100 ambalo litahitajika ili kupata kinda huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Independent)***

### PEDRO AGOMBEWA
INTER Milan na AC Milan zote zimeonyesha nia ya kumsajili winga Mhispania wa Chelsea, Pedro ambaye ana umri wa miaka 31. ***(Express)***

### BARELLA ANUKIA ARSENAL
ARSENAL ilituma wakala wake kwenda kumwangalia kiungo wa Cagliari na Timu ya Taifa ya Italia, Nicolo Barella (22) katika mechi dhidi ya Juventus iliyochezwa juzi usiku. ***(Star)***

### FELIX AGOMBEWA ULAYA
REAL Madrid na Juventus zimewaacha mbali Manchester United na Manchester City katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Benfica na Timu ya Taifa ya vijana ya Ureno ya umri chini ya miaka 21, Joao Felix (19). ***(Sun)***

### HAMMERS WAMTAKA ALLARDYCE
KOCHA Sam Allardyce amesema kuwa hajatuma maombi ya kutaka kuifundisha West Brom, licha ya jina lake kupewa nafasi ya kwanza kurithi mikoba ya Darren Moore. Kocha huyo wa zamani wa England mwenye umri wa miaka 64 amesema milango ya mazungumzo iko wazi. ***(Express and Star)***

### TIELEMANS SOKONI
MANCHESTER United nayo imeingia katika vita ya kuwania saini ya kiungo wa Leicester na Ubelgiji, Youri Tielemans (21), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu hiyo akitokea Monaco. ***(HLN, via Leicester Mercury)***

### MOURINHO AFUNGUKA
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Jose Mourinho amesema kuwa ugomvi wake na kiungo wa Ufaransa, Paul Pogba ulianza baada ya kumkataлия kusafiri na gari lake la kifahari la Rolls Royce na kumtaka atumie basi la timu. ***(Manchester Evening News)***

## HABARI MICHEZO

# PIERRE LIQUID SHANGWE TUPU BUNGENI DODOMA

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

MSANII wa vichekesho, Peter Mollel, maarufu Pierre Liquid, jana aliibua shangwe bungeni jijini hapa baada ya kutambulishwa kwa wabunge.

Pierre Liquid ambaye amejizolea umaarufu kutokana na mtindo wake wa uigizaji wa kuongea kama mlevi, alifika bungeni kwa mwaliko wa Mbunge wa Viti Maalum, Mariam Ditopile (CCM).

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'maswali' bungeni jana asubuhi, Spika wa Bunge, Job Ndugai, aliyekuwa anaongoza kikao, alimtaka Ditopile amtambulishe mgeni wake huyo akidai kuwa yeye hamfahamu.

"Nina mgeni lakini simfahamu, naomba nimpe heshima Mheshimiwa Mariam Ditopile atumie dakika moja kumtambulisha maana simfahamu," Spika Ndugai aliagiza.

Akimtambulisha Pierre Liquid, Ditopile alisema ni Mtanzania, mzalendo mjasiriamali wa samani anayepatikana Chang'ombe, ni mpenda burudani na ana kijiwe kinachoitwa Liquid.

"Ndugu Pierre ni maarufu na kwa kauli zake ambazo huwafurahisha watu na hata kama una msongo wa mawazo, anauondoa, hakika Mheshimiwa Spika utabaki kuwa kileleni, utakuwa juu.

"Lakini mzalendo huyu kutokana na uzalendo ambao ameuonyesha, kina Mzee Majuto leo tunawaenzi kutokana na usanii, kina Mr. Bean ni mabilionea kutokana na kipaji cha vichekesho."

Wakati wote ambao Ditopile alikuwa anamtambulisha Pierre bungeni, mgeni wake huyo alikuwa amesimama na kujipinda kwa mtindo wake wa "kubaki kileleni".

Mbunge huyo aliliambia Bunge kuwa Pierre ni mmoja kati ya watu waliojitoa kuleta hamasa kwa timu ya taifa ya soka 'Taifa Stars' kushinda 3-0 dhidi ya Uganda mwezi uliopita.

"Ndugu Pierre karibu sana bungeni, Magufuli utabaki kuwa juu utabaki kileleni," Spika Ndugai alisema.

Muda mfupi baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali' na Spika kuahirisha shughuli za Bunge hadi leo, Pierre alikutana na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa nje ya Ukumbi wa Bunge na kuahidiwa na kiongozi huyo wa nchi kupatiwa tiketi ya ndege ili afuatane na Taifa Stars kwenda Misri katika michuano ya Kombe la Afrika (Afcon).

Waziri Mkuu alimtaka msanii huyo kuendelea kuiunga mkono Taifa Stars kwa kuisema vizuri.

Baada ya mazungumzo hayo ya muda mfupi na Waziri Mkuu na kupiga picha na kiongozi huyo, wabunge na wafanyakazi wa Bunge walionekana wakitaka kupiga picha na msanii huyo kwenye Viwanja vya Bunge.



Wachezaji wa Azam FC, Frank Domayo (kushoto) na Nicholas Wadada wakishangilia moja ya bao walilofunga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara, dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza juzi. Azam FC ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

## MSIMAMO LIGI KUU BARA

| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1.YANGA | 28 | 21 | 4 | 3 | 45 | 19 | 67 |
| 2.AZAM | 29 | 18 | 8 | 3 | 48 | 18 | 62 |
| 3.SIMBA | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4.LIPULI | 31 | 11 | 11 | 9 | 26 | 26 | 44 |
| 5.KINONDONI MC | 30 | 9 | 14 | 7 | 32 | 22 | 41 |
| 6.MTIBWA SUGAR | 29 | 12 | 5 | 12 | 30 | 23 | 41 |
| 7.TZ PRISONS | 30 | 9 | 11 | 10 | 24 | 25 | 38 |
| 8.COASTAL UNION | 30 | 8 | 14 | 8 | 27 | 30 | 38 |
| 9.MBEYA CITY | 29 | 10 | 7 | 12 | 30 | 32 | 37 |
| 10.ALLIANCE | 30 | 9 | 10 | 11 | 23 | 30 | 37 |
| 11.MWADUI | 31 | 10 | 6 | 15 | 35 | 39 | 36 |
| 12.KAGERA SUGAR | 29 | 8 | 12 | 9 | 23 | 27 | 36 |
| 13.JKT TANZANIA | 31 | 8 | 12 | 11 | 18 | 26 | 36 |
| 14.MBAO | 31 | 9 | 9 | 13 | 19 | 32 | 36 |
| 15.STAND UTD | 31 | 10 | 6 | 15 | 29 | 40 | 36 |
| 16.RUVU SHOOTING | 31 | 8 | 11 | 12 | 27 | 37 | 35 |
| 17.SINGIDA UTD | 30 | 8 | 9 | 13 | 20 | 31 | 33 |
| 18.NDANDA | 28 | 8 | 9 | 11 | 17 | 29 | 33 |
| 19.BIASHARA UTD | 29 | 7 | 9 | 13 | 21 | 29 | 30 |
| 20.AFRICAN LYON | 31 | 4 | 10 | 17 | 19 | 39 | 22 |

# Aussems, Bocco washinda tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA ya timu ya Simba ya jijini Dar es Salaam imeendelea kung'ara baada ya kocha wake Mbelgiji, Patrick Aussems, kuteuliwa kuwa Kocha Bora wa mwezi Machi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Aussems amekuwa mshindi wa tuzo hiyo inayotolewa kila mwezi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) baada ya kuisaidia timu yake kufanya vema kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko katika hatua za lala salama. Kocha huyo ameiongoza Simba kupata ushindi katika mechi 10 mfululizo za ligi hiyo, kabla ya matokeo ya jana jioni walipokuwa wanaikabili JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro.

Mbelgiji huyo ambaye atapata zawadi ya Sh. milioni moja alikuwa anashindana na Abdul Mingange wa Azam FC pamoja na Zuberi Katwila wa Mtibwa Sugar.

Pia mshambuliaji wa Simba na nahodha, John Bocco ameteuliwa kuwa Mchezaji Bora wa Machi wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2018/2019.

Bocco ameshinda tuzo hiyo baada ya kuwazidi washambuliaji wengine wawili ambao ni, Donald Ngoma wa Azam FC na Jaffari Kibaya kutoka Mtibwa Sugar. Tuzo ya Kocha Bora mwezi uliopita ilichukuliwa na Kocha, Adolf Rishard wa Tanzania Prisons ya jijini Mbeya ambaye naye alipa ushindi wa mechi tano mfululizo na kuiondoa kwenye janga la kushuka daraja, ikiwa ni muda mfupi baada ya kujiunga na 'Maafande' hao.

Pia mshambuliaji wa Simba Mnyarwanda, Meddie Kagere alifanikiwa kuibuka kidedea katika tuzo ya Mchezaji Bora wa mwezi na kuzawadiwa kitita cha Sh. milioni moja kutoka kwa wadhamini wa tuzo hizo.

# JKU, Mlandege nguvu sawa Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

VINARA wa Ligi Kuu Zanzibar 'Maafande' wa JKU wamejikuta wakilazimishwa sare ya bila kufungana na Mlandege katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa juzi jioni kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Mechi hiyo ilionekana kuwa na ushindani tangu dakika za awali kwa kila upande kufanya mashambulizi, lakini pongezi zinatakiwa kwenda kwa mabeki wa klabu zote mbili.

Licha ya sare hiyo, JKU imeendelea kubaki kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 67 wakati Mlandege yenye pointi 59 wakisalia katika nafasi ya saba.

Baada ya kumalizika kwa mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Mlandege, Abdulhamid Rashid, alisema timu yake ilicheza vizuri katika dakika zote za mchezo huo licha ya kutopata bao.

Rashid alisema kuwa washambuliaji wake wanahitaji kuongeza bidii katika mechi zinazofuata ili waweze kuvuna pointi na wakifanya hivyo watakuwa wametimiza vema majukumu yao ya uwanjani.

**"Wachezaji wamefanya vizuri, walikuwa wanafika katika lango la wapinzani na kujaribu kufunga lakini haikuwa bahati yetu leo (juzi) kupata ushindi, lakini naamini mchezo unaofuata ambao tunakutana na Mafunzo tutapambana ili kuhakikisha tunaondoka na pointi tatu," alisema Rashid.**

Katika mechi ya mapema, Polisi walipata pointi tatu baada ya kuifunga Malindi bao 1-0, katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Mau Ze Dong, huku KVZ wakipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Jang'ombe Boys na Mwenge ikiwafunga Kizimbani bao 1-0 katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Michezo
Alhamisi Aprili 4, 2019
Nipashe



Solskjaer: Kumaliza Top 4 EPL ni ngumu HABARI UK 30



Beki wa Manchester United, Ashley Young, akimfanyia faulo iliyozaa kadi nyekundu, straika wa Wolverhampton Wanderers, Diogo Jota (aliyeangushwa), katika mechi ya Ligi Kuu England iliyochezwa kwenye Uwanja wa Molineux juzi usiku. Wolves ilishinda mabao 2-1.
**PICHA: MTANDAO**

# SIMBA: MUZIKI SASA KWA TP MAZEMBE

## ●●● Wafurahia mvua kusaidia kuahirishwa mechi dhidi ya JKT Tanzania, yarejea Dar usiku kumaliza...

**Na Isaac Kijoti, MOROGORO**

MVUA kubwa iliyonyesha kwa takriban saa moja kuanzia majira ya saa tisa alasiri mkoani hapa jana, imekuwa faraja kwa Simba inayokabiliwa na mechi ngumu ya hatua ya robo fainali dhidi ya TP Mazembe itakayochezwa Jumamosi.

Jana Simba ilitarajiwa kuikaribisha JKT Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu kwenye Uwanja wa Jamhuri, lakini mchezo huo ukashindwa kufanyika kutokana na baadhi ya sehemu uwanjani kutuama maji.

Akizungumza uwanjani hapa, baada ya mchezo huo kuahirishwa Katibu wa Chama cha Soka Mkoa wa Morogoro (MRFA), na Mkuu wa Kituo hicho, Charles Mwakambaya, alisema wameamua kuahirisha mechi hiyo kutokana na maji kutuama uwanjani.

Mwakambaya alisema wangeweza kuamua mechi hiyo ichezwe kesho, lakini kutokana na Simba kukabiliwa na mechi ya kimataifa dhidi ya TP Mazembe muda kikanuni hautaruhusu.

"Kwa mujibu wa kanuni kabla ya mechi nyingine timu inatakiwa ipate saa 72 ili kujiandaa na mechi nyingine, hivyo, ikichezwa kesho (leo) muda hautaruhusu kutokana na Simba kukabiliwa na mechi Jumamosi.

"Tumeshauriana na TFF pamoja na viongozi wa timu zote, Simba na JKT Tanzania kutokana na mazingira ya uwanja yaliyopo nje ya uwezo wetu, tukakubaliana kuiahirisha hadi itakapopangiwa tarehe nyingine," alisema Mwakambaya.

Hata hivyo, mashabiki wa Simba waliosafiri kutoka Dar es Salaam walifurahi sana kuahirishwa kwa mechi hiyo kwa kuwa timu yao itapata muda wa kutosha kujiandaa kuivaa TP Mazembe.

"Klabu awali iliandika barua TFF kuomba mechi hii isogezwe mbele, lakini ikakataliwa sasa Mungu amejibu maombi yetu, TP Mazembe lazima itakufa tu," alisema shabiki maarufu anayeingia na viporo uwanjani.

Simba iliondoka jana kurejea Dar es Salaam kujiandaa na mechi hiyo ya kimataifa.

"Kocha amesema tuondoke leo leo (jana), ili kurudi Dar kujiandaa na mechi ya Jumamosi," alisema Mratibu wa Simba, Abass Ally.

Hata hivyo, Simba itashuka uwanjani Jumamosi ikiwa na morali wa kushinda mechi zake 10 mfululizo za Ligi Kuu, huku TP Mazembe yenyewe ikitoka kuchezea kichapo cha bao 1-0 Jumamosi dhidi ya Saint Etoi Lupopo kwenye Ligi Kuu ya Kongo. Juzi, Jumanne TP Mazembe ilikuwa ishuke tena uwanjani kucheza mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Renaissance, lakini mchezo huo ukaahirishwa ili kuipa nafasi ya kujiandaa kuivaa Simba.

Awali Kocha wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems pia alilalamika kuhusu kucheza mechi hiyo ya jana dhidi ya JKT Tanzania, na uongozi kuandika barua Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuomba kuahirisha ili kutoa nafasi ya maandalizi lakini ilikataliwa.

# Yanga, Ndanda mechi ya kisasi

**Na Mwandishi Wetu, MTWARA**

TUKO tayari kupambana. Hiyo ndiyo kauli ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ndanda FC unaotarajiwa kuchezwa leo kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona mkoani hapa.

Hata hivyo Yanga itaendelea kuwakosa nyota wake wawili wa kikosi cha kwanza akiwamo nahodha, Ibrahim Ajibu ambaye ni majeruhi na beki Abdallah Shaibu 'Ninja' anayetumikia adhabu ya kufungiwa mechi tatu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema kuwa wachezaji wamejiandaa kukabiliana na ushindani kutoka kwa wenyeji wao kwa sababu wanajua ugumu wanaokutana nao katika mechi zote za ugenini.

"Tuko katika mapambano ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu, na vile vile tunaendelea na mashindano ya Kombe la FA, mechi zote kwetu ni muhimu na tunaingia tukiwa na mbinu zisizofanana, lakini tunajua tunachokihitaji," alisema Zahera.

Aliongeza kwamba vita ya ubingwa iko wazi kutokana na wapinzani wao, Simba na Azam FC bado wana idadi kubwa ya mechi za viporo na katika soka lolote linaweza kutokea.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Soka Mtwara (MTWAREFA), Athumani Kambi, amesema kuwa maandalizi ya mchezo huo yamekamilika na kinachosubiriwa ni timu itakayofanya vema kuondoka na ushindi.

Kambi aliwaomba mashabiki wa soka wa Mtwara na mikoa ya jirani kujitokeza kushuhudia mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na rekodi za nyuma, kila timu hizo zinapokutana. Ligi hiyo inatarajia kuendelea tena Jumapili kwa Mbao FC kuwakaribisha Azam FC kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

Yanga yenye pointi 67 ndio inaongoza katika msimamo wa ligi hiyo ikifuatiwa na Azam FC wenye pointi 62, wakati Simba ambao ni mabingwa watetezi wako katika nafasi ya tatu, lakini wamecheza mechi pungufu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >